# Nipashe

Ijumaa Januari 13, 2023 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

ISSN 0856 • Na. 0581189

www.ippmedia.com

MWANGA WA JAMII

The Guardian digital

nipasheTZ nipasheTZ nipasheTZ 0745 700710

LIKE & FOLLOW US



Mikutano itumike kuibua uozo, udhaifu

Ukurasa 13

BUFE

IJUMAA JANUARI 13, 2023 Nipashe

BIASHARA, UCHUMI NA FEDHA

BOSI MKUU AJIGAMBA: Licha ya mtikisiko wa Covid 19, UTT yang'ara katika miradi yote ya fedha nchini

Ukurasa 12

MIAKA 59 YA MAPINDUZI SMZ

Waziri aeleza mageuzi kuhamia uvuvi biashara, jinsi boti 500 zilivyozinduliwa

Na Christina Mwakangale

INAPOTIMIA miaka 59 tangu yalipotokea Mapinduzi Matukufu Zanzibar, sasa Serikali ya Mapinduzi Zanzibar (SMZ), kupitia Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Rais Dk. Hussein Ali Mwinyi, sasa imejikita kwenye kuimarisha uchumi, kupitia rasilimali inayokizunguka kisiwa hicho, bahari.

Uchumi wa Bluu utokanao na matumizi ya bahari na rasilimali zake, hapo unaangukia katika mazao ya samaki, mwani mafuta na gesi, ambako ndiko nguvu zinaelekezwa na serikali ya SMZ, kwa kipindi cha muda mfupi, kati na mrefu.

Waziri wa Uchumi na Uvuvi Zanzibar, Suleiman Masoud Makame, katika mazungumzo na kituo cha televisheni ya ITV, anasema SMZ imelenga kuwa na maendeleo endelevu kupitia rasilimali hiyo na ndio dhana na mkakati uliopo, akisema awali utambulisho wa azma hiyo ulikuwa haujaeleweka ipasavyo.

"Wakati ikinadiwa dhana ya uchumi wa buluu, ilikuwa haijaingia katika vichwa vya watu. Kwa kiasi kikubwa, serikali kupitia Rais Dk. Hussein Mwinyi, imekuwa ikizungumzia kwenye mikutano yake mingi, lakini wizara nayo tumeanza.

"Wizara ya Uchumi na Uvuvi katika fedha zile za Uviko-19, nayo ilipata Sh. bilioni 36.5 na tumeanza kuwawezesha wavuvi, wakulima wa mwani, wafugaji samaki, matango bahari na tumetenga utengenezaji wa boti 1,077.

"Namna tunaenda kutumia bahari kiuchumi kuendeleza wavuvi, wafugaji wa mazao ya baharini. Ndani ya miaka mitano 2020 hadi 2025, lengo ni kuzalisha ajira 300,000, lakini tutazalishaje ajira ni kupitia sekta ya uchumi," anasema Waziri huyo.

Anafafanua kuwa, mikakati iliyoko ni kuzikabili changamoto ambazo ni matumizi mabaya ya uvuvi baharini, akisema kati yake boti 577 zitakuwa za kisasa za kutunza mazingira, ambazo zitakuwa na kiongoza meli au GPS, pamoja na kitafuta samaki ('fish finder'), ili kuwaongoza wavuvi kubaini palipo na samaki wengi.

KILIMO BAHARI

Anasema kwenye kilimo cha mwani, changamoto iliyoko ni soko, mitaji na taaluma na kwamba hivi sasa elimu imetolewa kwao kuwawezesha wakulima hao kupata mkopo nafuu usio na riba, kwa kuwapatia boti 500 kwa jumla ya vikundi 500 vya Unguja na Pemba.

"Kwa mila, silka na desturi za Kizanzibari, utakapotoa mikopo ambayo ina 'interest' ndani yake, wale wengi wangeogopa kuchukua mkopo. Pia, tumeanza ujenzi wa kiwanda kikubwa cha zao la mwani, ambacho kitasarifu zao la mwani," anasema Makame.

Lingine analolizungumzia, ni hadi sasa zao hilo linatengeneza bidhaa nyingi, ikiwamo chakula, mbolea, dawa, kinywaji, pia mapambo na kwamba matarajio yaliyoko sasa, ni bei ya kilo moja ya unga inaongezeka na kufikia kati ya Sh. 5,000 hadi 10,000 kutoka Sh. 700 ya awali. Hata hivyo hakufafanua ni lini.

"Mkulima sasa atakuwa hana wasiwasi na kiwanda hiki kimependisha thamani ya zao, kwa muda mrefu tumekuwa tukisafirisha bidhaa zetu nje kwa bei ndogo, lakini ikifanyiwa uchakataji hapa inakuza thamani," anasema Makame.

VIWANDA VYA DAGAA

Waziri Makame anasema, zao la dagaa kwa miaka kadhaa limekuwa likisafirishwa kwa tani nyingi kwenda nchi jirani, ikiwamo Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo (DRC), ingawa uvunaji wake umekuwa wa kienyeji.

"Ujenzi wa kusarifu samaki umeanza. Zanzibar tunajivunia uwepo wa dagaa ingawa tumekuwa tukiuza 'locally' (kienyeji), kwenye soko la Congo, sasa viwanda hivi vitawezesha dagaa kuwaandalia kabisa, ukifika nyumbani ni kufungua na kuanza kula na ugali wako. Tunaongeza thamani ya mazao ya bahari, kipato na uchumi," anaeleza.

Pia, waziri huyo mwenye dhamana na uvuvi, anaeleza kuwa mwelekeo wa sasa wa uvuvi ni kweye bahari kuu kwa kutumia boti ya kisasa, akisema bahari ambayo ndio chanzo kikuu cha uchumi, itabeba utalii.

WANUFAIKA MIKOPO

Makame anawataja watakaonufaika na mikopo hiyo tajwa, ni wavuvi wadogo ambao awali walienda bahari ni kurudi nyumbani wakiwa na kitoweo kidogo kwa ajili ya mboga, pasipo kusalia cha ziada walau cha kuuza kiasi

"Mikopo hii tunaratibu na benki, kwa kuangalia vigezo; kweli ni mvuvi, anaweza kufanya shughuli hii, atarejesha fedha? Boti ambazo tumezichonga za mita saba zipo 300 na zote zina jokofu na kila moja inabeba watu watano.

"Kwa boti hizi kwenye 'field' (eneo la kazi baharini) kunafanyika kazi, wanaweza kwenda watu 5,000 hawa wakirudi na samaki watatoa ajira kwa watu takribani 70,000 za moja kwa moja. Watakuwa wanakatakata samaki wanaoenda kuwauza," anasema Makame.

Anafafanua, lengo la serikali pia ni kuweka kwenye uhifadhi wa samaki, mara baada ya kuwavua, kwa kuwapo majokofu makubwa yenye uwezo wa kuhifadhi samaki kilo 600 na barafu 400.

Makame anasema, kuna mchakato wa kutafuta mafuta na gesi yanayochukua muda mrefu na ulianza kutathminiwa tangu zama za miaka ya 1950 na kwamba, zipo nyaraka za majibu zilipokelewa mwaka jana, waliona viashiria vya uwapo rasilimali hiyo.

Anasema, kwa hivi sasa uhamasishaji uko katika watu kujiajiri na kwamba kuna wanawake 80 waliojikita kwenye uchuuzi wa buluu, wamekwishanufaika kwenye sekta hiyo, akitoa wito kwa vijana wengine nao wajiajiri.

Boti mojawapo ya uvuvi, iliyozinduliwa na Rais mstaafu Dk. Ali Shein mtangulizi wa Dk. Hussein Mwinyi, katika zama za uongozi wake. PICHA:MTANDAO.

UKURASA 11

SUPA JACKPOT

TZS. 1,065,505,647

KWA TZS. 1000 TU!

SCAN HAPA KUPAKUA APP YETU!

SportPesa.CO.TZ

PIGA *150*87#



UKURASA 3

## Morani wadaiwa kushambulia, kujeruhi viongozi CCM

MIAKA 59 MAPINDUZI

UKURASA 2

# Mwinyi ajivunia amani, mshikamano





Kamanda wa Polisi Kikosi cha Reli, ACP Sebastian Mbutta, akizungumza kuhusu vifaa mbalimbali na lita 700 za mafuta ya dizeli, vilivyokamatwa vikiwa vimeibwa na wahalifu katika maeneo ya mradi wa ujenzi wa reli ya kisasa (SGR), kipande cha Mwanza-Isaka. **PICHA: IDDA MUSHI**

## Vifaa vya SGR vilivyohujumiwa vyakutwa vimetelekezwa

UKURASA. 18

## Mkaguzi wa Polisi afariki dunia akiruka ukuta gesti

UKURASA 2

MICHEZO KAMBI YA SIMBA DUBAI IMENOGA UK.24 MAONI, KATUNI UK.6



Makamu wa Rais, Dk. Philip Mpango, akipanda mti aina ya Mdodoma kandokando ya barabara ya Dodoma – Morogoro, eneo la Ihumwa, jijini Dodoma jana, wakati akiongoza zoezi la upandaji miti kusherehekea maadhimisho ya Miaka 59 ya Mapinduzi Matukufu ya Zanzibar. Habari Uk. 5. **PICHA: OMR**

# Mwinyi ajivunia amani, mshikamano

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

WAKATI Zanzibar ikiadhimisha miaka 59 ya Mapinduzi ya mwaka 1964, Rais wa Zanzibar, Dk. Hussein Ali Mwinyi, ameeleza mafanikio yaliyopatikana katika serikali anayoiongoza ambayo yametokana na hali ya amani, umoja na mshikamano.

Rais Mwinyi aliyasema hayo juzi wakati akizungumza na waandishi wa habari kuhusu sherehe hizo ambazo kwa mwaka huu, zimesherehekewa kwa fedha kuelekezwa kwenye miradi ya sekta ya elimu.

Alisema kuwapo kwa amani na utulivu nchini kumewezesha serikali kupata mafanikio ya kuridhisha katika ukuaji wa uchumi kutokana na kuongezeka kwa uwekezaji, usafirishaji wa mazao ya karafuu na mwani, ujenzi wa miundombinu na uimarishaji wa huduma za jamii zikiwamo elimu na afya.

Alisema kiwango cha ukuaji wa uchumi hadi mwaka 2021 kilikuwa wastani wa asilimia 5.1 ambao ni mkubwa ikilinganishwa na asilimia 1.3 kwa mwaka 2020.

"Kasi ya mfumuko wa bei imeendelea kudhibitiwa kwa mwaka 2022 hadi kufikia asilimia 5.08 na kuendelea kubaki kwenye tarakimu moja. Serikali imekuwa ikiendelea kuchukua hatua mbalimbali za kudhibiti kasi ya mfumuko wa bei ili wananchi waendelee kupata huduma kwa gharama nafuu kwa kufidia na kutoa bei elekezi kwa bidhaa muhimu," alisema.

Alisema hadi Desemba, mwaka jana serikali ilitoa Sh. bilioni 21.525 kudhibiti ongezeko la bei za mafuta nchini.

### UKUSANYAJI MAPATO

Alisema mafanikio makubwa yameendelea kupatikana katika ukusanyaji wa mapato na katika mwaka 2021/2022 mapato ya ndani yalikuwa Sh. bilioni 908.61 ikilinganishwa na Sh. bilioni 712.42 mwaka 2020/2021.

### UWEKEZAJI

Hadi Januari 2023 jumla ya miradi yenye thamani ya Dola za marekani bilioni 3.26 215 imesajiliwa na Mamlaka ya Kukuza Vitega Uchumi Zanzibar (ZIPA), ambayo itatoa fursa za ajira 13,000.

"Vile vile, ZIPA imeweza kusajili miradi ya uwekezaji katika visiwa 16 vidogo yenye thamani ya Dola za Kimarekani 377,500,000," alisema Rais Mwinyi.

"Hadi mwishoni mwa mwezi Desemba, 2022, kupitia fedha za ahueni ya UVIKO-19, serikali imetoa jumla ya mikopo 2,625 yenye thamani ya Sh. 16, 828,133,520.17, kwa wananchi Unguja na Pemba," alisema.

Kwa mujibu wa Rais Mwinyi, mradi huo wa vituo vya wajasiriamali hadi sasa umegharimu Sh. 16,034,499,894 na wajasiriamali 6,800 wa makundi mbalimbali watanufaika moja kwa moja kwa kupata sehemu za kudumu za kuendeshea biashara zao.

### AJIRA

Katika kukabiliana na changamoto ya ajira hasa kwa vijana, alisema serikali katika kipindi cha miaka miwili imeanza kuchukua hatua mbalimbali ikiwamo kuanza kuajiri katika sekta za afya na elimu.

"Jumla ya nafasi za ajira 1,029 zimetolewa kwa mwaka 2021/2022. Aidha, vibali 2,355 vimeshatolewa na Tume ya Utumishi na hivi sasa hatua mbalimbali za kuajiri watumishi hao wapya zinaendelea," alisema.

### MIUNDOMBINU

Dk. Mwinyi alisema mafanikio makubwa yamepatikana pia katika ujenzi wa miundombinu, ikiwamo viwanja vya ndege, barabara na utekelezaji wa dhamira ya serikali ya kuziimarisha bandari.

Kazi za ujenzi wa barabara za ndani kwa kiwango cha lami zenye urefu wa km 275 inayofanywa na Kampuni ya ASER inaendelea katika maeneo mbalimbali nchini.

### ELIMU

Sekta ya elimu, serikali imefanya juhudi kubwa kuiimarisha kwa kuzingatia umuhimu wake kwa maendeleo ya taifa na ustawi wa mwananchi kwa lengo la kuondoa msongamano wa wanafunzi madarasani na kuimarisha mazingira ya kujifunza na kufundishia.

Alisema, kwa mwaka mmoja uliomalizika, serikali imejenga jumla ya shule mpya za ghorofa tisa, Unguja na Pemba pamoja na madarasa 811 mapya yakiwamo yale yaliyoanzishwa kwa nguvu za wananchi.

Aidha, alisema serikali imejenga vyoo 1,693 na kukarabati shule 24 za zamani, shule zote mpya zimepatiwa vifaa vya kusomea pamoja na madawati, ili kuwawezesha wanafunzi kujifunza katika mazingira yaliyo bora.

### MAJI

Alisema kwenye sekta ya maji kipindi cha miaka miwili, serikali imechimba jumla ya visima 102 kati ya hivyo 64 ni vya mradi wa Exim Bank, wenye lengo la kuimarisha upatikanaji wa huduma za majisafi na salama katika maeneo mengi ya Mkoa wa Mjini Magharibi.

Alisema visima 38 vimechimbwa kupitia mradi wa ahueni ya UVIKO - 19, kati ya hivyo 19 vimekamilika.

"Ujenzi wa matangi 10 ya kuhifadhia maji yenye ujazo wa lita milioni moja kwa kila moja umefikia wastani wa asilimia 70 na ujenzi wa vibanda 52 vya kuhifadhia mitambo ya pampu uko katika hatua za mwisho," alisema.

### UMEME

Kwenye umeme, alisema serikali ilifanya uamuzi wa kuwapunguzia wananchi gharama za kuunganisha huduma ya umeme kutoka Sh. 442,000 hadi Sh. 200,000.

Alisema katika kipindi cha miaka miwili jumla ya wateja wapya 71,458 sawa na asilimia 86 ya lengo la kuwaungia wateja 83,400 walipata huduma hiyo.

# Mkaguzi wa Polisi afariki dunia akiruka ukuta gesti

**Na Cynthia Mwilolezi,**
ARUSHA

MKAGUZI wa Polisi aliyekuwa akifanyakazi wilayani Arumeru Stewart Kaino (47), amefariki dunia baada ya kuruka ukuta wa gesti na kuchomwa na kitu chenye ncha kali kichwani.

Taarifa za awali kutoka kwa shuhuda wa tukio hilo aliyeomba jina lake lihifadhiwe, zimedai kuwa Kaino aliingia katika nyumba hiyo majira ya saa sita usiku akiwa na mwanamke mmoja ambaye jina lake halikuweza kupatikana.

Alisema aliandikisha katika kitabu cha wageni na kupewa chumba na kisha kuingia na mwanamke huyo, akiwa ameshika begi dogo la mgongoni na redio ya mawasiliano aliyokuwa nayo mkononi.

Alisema majira ya saa tisa usiku alitoka ndani ya chumba hicho na kumuacha mwanamke huyo akiwa amelala.

Alidai kuwa alikwenda nyuma ya nyumba hiyo na kuruka geti akiwa na lengo la kumtoroka mwanamke huyo ndipo alipoanguka na kuchomwa na kitu chenye ncha kali kichwani.

Taarifa zinadai baada ya mlinzi kusikia kishindo alienda katika geti hilo na kumkuta akiwa ameanguka chini akivuja damu nyingi kwenye paji la uso na kutoa taarifa polisi na majira ya alfajiri walifika na kukuta ameshapoteza maisha.

Alidai askari polisi walipekua begi la marehemu na kukuta chupa ya bia, chips, redio ya mawasiliano, simu mbili ikiwamo ya mwanamke huyo na vitu vingine.

Kamanda wa Polisi Mkoa wa Arusha, Justine Masejo, alithibitisha kutokea kwa tukio hilo na kudai Jeshi la Polisi lilipokea taarifa Januari 8, mwaka huu majira saa 8:30 usiku.

Alisema taarifa hiyo ilieleza kuna mtu alifariki nje ya nyumba ya kulala wageni iliyopo Kata ya Levolosi jijini humo.

"Baada ya kupata taarifa hizi askari wangu walienda eneo la tukio na kukuta mwili ambao waliutambua kuwa ni Mkaguzi wa Polisi, Stewart Kaino (47) anayefanya kazi wilayani Arumeru," alisema.

Aidha, alisema jeshi hilo linaendelea na uchunguzi wa kubaini mazingira ya kifo hicho.

Mwili wa marehemu umesafirishwa kwenda kwao Bukoba kwa ajili ya maziko.

HABARI KITAIFA

# Morani wadaiwa kushambulia, kujeruhi viongozi CCM

**Na Cynthia Mwilolezi,**
ARUSHA

KUNDI la vijana 30 wa jamii ya kifugaji ya Kimasai maarufu Morani linatuhumiwa kuwashambulia kwa kipigo na kuwajeruhi viongozi saba wa Chama Cha Mapinduzi (CCM), Kata ya Engaruka, Wilaya ya Monduli, mkoani Arusha, baada ya kuwatuhumu kutaka kupora ardhi.

Vijana hao wanaodaiwa kuwa wakazi wa Kijiji cha Engaruka Juu, wanadaiwa kuwavamia na kuwashambulia kwa mikuki na mawe viongozi hao na baadhi yao kukimbizwa Hospitali ya Rufani ya Mkoa wa Arusha ya Mount Meru na kulazwa kutokana na kuumizwa maeneo mbalimbali ya mwili.

Akizungumzia tukio hilo, Mkuu wa Wilaya ya Monduli, Frank Mwaisumbe, alisema tukio hilo limetokea Januari10, mwaka huu majira ya jioni, wakati viongozi hao wakiwamo wajumbe wa Kamati ya Siasa ya CCM kata, walipokwenda kijijini hapo kufuatilia mgogoro wa ardhi.

Alisema walipofika eneo lenye mgogoro, walikutana na kundi la Morani zaidi ya 30 waliokuwa wamejikusanya na kujihami kwa silaha za jadi, ambao baada ya kuwaona walianza kuwashambulia kwa mikuki na mawe.

Miongoni mwa viongozi waliokumbwa na kadhia hiyo ni Mwenyekiti wa CCM kata hiyo, Leliya Sengeita na Katibu wake, Joseph Namoyo, walioshambuliwa sehemu mbalimbali za miili yao na baadhi yao kupata majeraha ya kutobolewa jicho, kuvunjwa miguu, mikono, kujeruhiwa kichwani, mbavu na usoni.

Kwa mujibu wa Mwaisumbe, Jeshi la Polisi wilayani humo, limeanza uchunguzi na wanamshikilia Mwenyekiti wa Serikali ya Kijiji hicho, Abrahamu Logolie, kwa upelelezi zaidi, baada ya kuwapo taarifa ndiye aliyehamasisha wananchi wajikusanye.

Alisema kuwa watu saba walijeruhiwa na kupatiwa fomu namba tatu ya Polisi (PF 3) na kwenda kutibiwa katika kituo cha afya kilichoko Mto wa Mbu wilayani humo, huku baadhi yao wakihamishiwa Hospitali ya Rufani ya Mkoa wa Arusha ya Mount Meru, kwa matibabu zaidi.

Mwaisumbe, alisema upelelezi wa tukio hilo unaendelea, kuwabaini na kuwakamata waliohusika kutekeleza shambulizi hilo na ametuma timu ya askari polisi kutoka Monduli ikiongozwa na mkuu wa upelelezi kwenda eneo la tukio kuongeza nguvu katika uchunguzi.


## SHIRIKA LA UMEME TANZANIA (TANESCO)

## TANGAZO LA MNADA WA HADHARA

Shirika la Umeme Tanzania (TANESCO) linawatangazia wananchi wote kuwa, litaondosha kwa njia ya mnada wa hadhara mitambo chakavu iliyokuwa inazalisha umeme kwa kutumia mafuta, Vipuri mbalimbali vya mitambo vilivyotumika pamoja na Mafuta machafu, katika vituo vya Nyakato(Mwanza), Tabora, Songea (Ruvuma), Iyunga (Mbeya), Kigoma (Kigoma, Kasulu, Kibondo), Kilwa Masoko (Lindi), Masasi (Mtwara), Tunduma(Songwe), Sumbawanga (Rukwa),Tunduru(Songea), Biharamulo (Kagera), Ngara (Kagera), Zuzu (Dodoma), Loliondo (Arusha), Ikwiriri (Pwani), Mafia (Pwani) kama inavyoonekana hapa chini.

Mnada utafanywa kwa makampuni yenye vibali vilivyotolewa na waziri mwenye dhamana ya mazingira kwa kuzingatia matakwa ya sheria ya mazingira ya mwaka 2004 na kanuni zake za "Environmental Management (Control and Management of Electrical and Electronic Equipment Waste) Regulations, 2021" na "The Environmental Management (Hazardous Waste Control and Management) Regulations, 2021"

**VITUO AMBAPO MNADA UTAFANYIKA PAMOJA NA VIFAA HUSIKA**

| NA | KITUO | VIFAA VITAKAVYOUZWA | TAREHE YA MNADA |
|---|---|---|---|
| 1 | Old Nyakato | Mitambo chakavu minne (4) aina ya Mirrlees Blackstone iliyokuwa inazalisha umeme kwa kutumia mafuta pamoja na vipuri vilivyotumika | 30/01/2023 |
| 2 | Tabora | Mitambo chakavu miwili (2) aina ya Mirrlees Blackstone iliyokuwa inazalisha umeme kwa kutumia mafuta pamoja na vipuri vilivyotumika | 03/02/2023 |
| 3 | Old Kigoma | Mitambo chakavu mitano (5) aina ya Wartsila iliyokuwa inazalisha umeme kwa kutumia mafu, vipuri vilivyotumika pamoja na mafuta machafu | 06/02/2023 |
| 4 | Kasulu | Mafuta machafu | 08/02/2023 |
| 5 | Kibondo | Mafuta machafu | 10/02/2023 |
| 6 | Ngara | Vipuri mbalimbali vilivyotumika pamoja na mafuta machafu | 13/02/2023 |
| 7 | Biharamulo | Vipuri mbalimbali vilivyotumika | 15/02/2023 |
| 8 | Bukoba | Mafuta machafu | 17/02/2023 |
| 9 | Ikwiriri | Mafuta machafu | 24/02/2023 |
| 10 | Kilwa Masoko | Mtambo chakavu mmoja (1) aina ya Perking iliyokuwa inazalisha umeme kwa kutumia mafuta pamoja na vipuri vilivyotumika | 25/02/2023 |
| 11 | Masasi | Vipuri mbali mbali vilivyotumika pamoja na mafuta machafu | 27/02/2023 |
| 12 | Tunduru | Vipuri mbalimbali vilivyotumika | 01/03/2023 |
| 13 | Old Songea | Mtambo chakavu mmoja (1) aina ya Wartsila uliokuwa unazalisha umeme kwa kutumia mafuta pamoja na vipuri vilivyotumika | 03/03/2023 |
| 14 | Iyunga | Mitambo chakavu mmoja (1) aina ya Wartsila iliyokuwa inazalisha umeme kwa kutumia mafuta pamoja na vipuri vilivyotumika | 06/03/2023 |
| 15 | Tunduma | Vipuri mbalimbali vilivyotumika | 07/03/2023 |
| 16 | Sumbawanga | Vipuli mbalimbali vilivyotumika | 09/03/2023 |
| 17 | Zuzu | Mafuta machafu | 11/03/2023 |
| 18 | Loliondo | Mafuta machafu | 13/03/2023 |
| 19 | Mafia | Mafuta machafu | 15/03/2023 |

**MASHARTI YA MNADA**

1. Bidhaa/Kifaa kitauzwa kama kilivyo na mahali kilipo;
2. Mnunuzi atalazimika kulipa papohapo amana (deposit) isiyopungua asilimia ishirini na tano (25%) ya thamani ya Bidhaa/Kifaa alichonunua, na kukamilisha malipo yote katika muda wa siku kumi na nne (14) kuanzia tarehe ya mnada. Mnunuzi akishindwa kutimiza sharti hili atakosa haki zote za ununuzi wa bidhaa/kifaa husika na amana iliyolipwa haitarudishwa;
3. Mtu yeyote atakaye tamka bei ya juu kisha akashindwa kulipa asilimia ishirini na tano (25%) ya bei aliyotamka, atachukuliwa kuwa ni mwenye kutaka kuvuruga mnada na hivyo hatua kali za kisheria zitachukuliwa dhidi yake kwa mujibu wa sheria za Jamhuri ya Muungano wa Tanzania;
4. Mnunuzi atatakiwa kuondoa/kuchukua bidhaa/kifaa alichonunua katika muda wa siku saba (7) kuanzia siku ya kukamilisha malipo;
5. Mnada utafanywa kwa wanunuzi wenye vibali vilivyotolewa na waziri mwenye dhamana ya mazingira. Wanunuzi watatakiwa kuleta leseni/vibali vyao ambavyo vitakaguliwa kabla ya zoezi la mnada kuanza. Vile vile nakala ya leseni/vibali hivyo itabaki kwa Muuzaji kwa ajili ya kumbukumbu;
6. Ruhusa ya kuangalia vifaa itatolewa siku (5) kabla ya tarehe ya mnada husika;
7. Mnada utaanza saa nne (04:00) kamili asubuhi katika kila kituo kwa mtiririko uliooneshwa.
8. Wananchi wote wenye sifa mnakaribishwa kushiriki katika mnada huu wa hadhara.

**IMETOLEWA NA;**
**MKURUGENZI MTENDAJI**
**SHIRIKA LA UMEME TANZANIA (TANESCO),**
**PLOT 114 BLOCK G DAR ES SALAAM ROAD,**
**S. L. P. 453 DODOMA, TANZANIA.**

117225502

# UNITED BANK FOR AFRICA (TANZANIA) LIMITED

UBA

## VIWANGO VYA CHINI VYA ADA NA TOZO

| NA | KIPENGELE/MUAMALA | | |
|---|---|---|---|
| SEHEMU A | AKAUNTI ZA AKIBA | REJAREJA | KAMPUNI/SHIRIKA |
| 1 | AKIBA HURU | | HAKUNA |
| | Kiasi cha chini cha kufungulia | SH. 15,000 | |
| | Kiasi cha chini cha uendeshaji | SH 2,000 | |
| | Ada ya utunzaji ya kila mwezi | HAKUNA | |
| | Tozo za kutoa pesa | Tozo ya papohapo ni 1,000 | |
| 2 | AKIBA ZA JUMLA | | HAKUNA |
| | Kiasi cha chini cha kufungulia | SH. 20,000 | |
| | Kiasi cha chini cha uendeshaji | SH. 5,000 | |
| | Ada ya utunzaji ya kila mwezi | HAKUNA | |
| | Tozo za kutoa pesa | SH. 1,000 | |
| 3 | AKIBA ZA MWAJIRIWA | | HAKUNA |
| | Kiasi cha chini cha kufungulia | SH. 15,000 USD 15 | |
| | Kiasi cha chini cha uendeshaji | SH. 2,000 USD 10 | |
| | Ada ya utunzaji ya kila mwezi | HAKUNA | |
| | Tozo za kutoa pesa dirishani | SH 2,000 - Kiwango kisichozidi SH 5,000,000<br>SH 2000+ 0.1% (Kiwango kilichozidi 5,000,000)- > 5,000,000.<br>(Kiwango kikubwa cha tozo ni kiasi kisichozidi SH 100,000) | |
| 4 | AKAUNTI ZA AKIBA ZA WATU BINAFSI | | HAKUNA |
| | Kiasi cha chini cha kufungulia | SH. 15,000 | |
| | Kiasi cha chini cha uendeshaji | SH. 5,000 | |
| | Ada ya utunzaji ya kila mwezi | HAKUNA | |
| | Tozo za kutoa pesa dirishani | SH 2,000 - Kiwango kisichozidi SH 5,000,000<br>SH 2000+ 0.1% (Kiwango kilichozidi 5,000,000)- > 5,000,000.<br>(Kiwango kikubwa cha tozo ni kiasi kisichozidi SH 100,000) | |
| 5 | AKAUNTI YA AKIBA YA MSHAHARA | | HAKUNA |
| | Kiasi cha chini cha kufungulia | SH.15,000 | |
| | Kiasi cha chini cha uendeshaji | SH. 5,000 | |
| | Ada ya utunzaji ya kila mwezi | HAKUNA | |
| | Tozo za kutoa pesa kwa dirishani | SH 2,000 - Kiwango kisichozidi SH 5,000,000<br>SH 2000+ 0.1% (Kiwango kilichozidi 5,000,000)- > 5,000,000.<br>(Kiwango kikubwa cha tozo ni kiasi kisichozidi SH 100,000) | |
| 6 | AKAUNTI YA FEDHA ZA KIGENI | | |
| | Kiasi cha chini cha kufungulia | USD 10 | |
| | Kiasi cha chini cha uendeshaji | USD 5 | |
| | Ada ya utunzaji ya kila mwezi | HAKUNA | |
| | Tozo za kutoa pesa | 1% kwa muamala, isizidi USD 150 | |
| 7 | AKAUNTI YA AKIBA YA WATOTO YA U-CARE | | HAKUNA |
| | Kiasi cha chini cha kufungulia | USD 15 | |
| | Kiasi cha chini cha uendeshaji | USD 15 | |
| | Ada ya utunzaji ya kila mwezi | HAKUNA | |
| | Tozo za kutoa pesa | SH. 1,000 au kiasi kinacholingana na hicho | |
| 8 | AKAUNTI YA MALAIKA | | HAKUNA |
| | Kiasi cha chini cha kufungulia | SH. 20,000 | |
| | Kiasi cha chini cha uendeshaji | HAKUNA | |
| | Ada ya utunzaji ya kila mwezi | HAKUNA | |
| | Tozo za kutoa pesa | HAKUNA | |
| 9 | AKAUNTI YA JANJA | | HAKUNA |
| | /Kiasi cha chini cha kufungulia | SH. 20,000 | |
| | Kiasi cha chini cha uendeshaji | HAKUNA | |
| | Ada ya utunzaji ya kila mwezi | HAKUNA | |
| | Tozo za kutoa pesa | HAKUNA | |
| 10 | AKAUNTI YA KIZAZI KIPYA | | HAKUNA |
| | Kiasi cha chini cha kufungulia | SH. 20,000 | |
| | Kiasi cha chini cha uendeshaji | HAKUNA | |
| | Ada ya utunzaji ya kila mwezi | HAKUNA | |
| | Tozo za kutoa pesa | HAKUNA | |
| 11 | AKAUNTI YA HAZINA | | HAKUNA |
| | Kiasi cha chini cha kufungulia | SH. 20,000 | |
| | Kiasi cha chini cha uendeshaji | SH. 20,000 | |
| | Ada ya utunzaji ya kila mwezi | HAKUNA | |
| | Tozo za kutoa pesa | HAKUNA | |
| SEHEMU B | AKAUNTI YA HUNDI | | |
| 1 | AKAUNTI BINAFSI YA HUNDI | | AKAUNTI YA BIASHARA YA HUNDI |
| | Kiasi cha chini cha kufungulia | SH. 30,000 | SH. 100,000 |
| | Kiasi cha chini cha uendeshaji | SH.10,000 | SH. 100,000 |
| | Ada ya utunzaji ya kila mwezi | SH. 10,000 | SH. 12,000 |
| | Kutoa pesa taslimu kwa dirishani | 1 KWA KILA 1,000, kiasi kisichozidi SH. 150,000 | Akaunti SH. 1 KWA KILA 1, 000, Kiasi kisichozidi SH. 250,000 |
| | Adhabu ya kutoa pesa zaidi ya kiwango kinachotakiwa | Kiwango cha kuanzia+ 5% | Akaunti ya SH. Kiwango cha kuanzia + 10% |
| | Brela Seach charge | SH. 5000 kwa wajasiriamali | SH. 25000 kwa kampuni |
| 2 | AKAUNTI ZA KIDIPLOMASIA | | |
| | Kiasi cha chini cha kufungulia | USD 100 | HAKUNA |
| | Kiasi cha chini cha uendeshaji | USD 100 | HAKUNA |
| | Ada ya utunzaji ya kila mwezi | HAKUNA | HAKUNA |
| | Kutoa pesa taslimu kwa dirishani | HAKUNA | HAKUNA |
| | Kufunga Akaunti | HAKUNA | HAKUNA |
| | Adhabu ya kutoa pesa zaidi ya kiwango kinachotakiwa | HAKUNA | HAKUNA |
| | Utumaji wa Fedha Nje ya Nchi (TTs) | USD 50 FLAT ( SHA), USD 90 ( OURS) | HAKUNA |
| | Utumaji wa Fedha Ndani ya Nchi | HAKUNA | HAKUNA |
| | Ubadilishaji wa Fedha za kigeni | Viwango vya bei nafuu vitatumika | HAKUNA |
| 3 | AKAUNTI YA HUNDI YA FEDHA ZA KIGENI | | |
| | Kiasi cha chini cha kufungulia | USD 100/ YURO100/PAUNDI 100 | USD 100/ YURO/PAUNDI 100 |
| | Kiasi cha chini cha uendeshaji | USD100/ YURO100/PAUNDI 100 | USD 100/ YURO 100/ PAUNDI 100/ |
| | Ada ya utunzaji ya kila mwezi | USD 12 au kiasi kinachoendana na hicho | USD 15 au kiasi kinachoendana na hicho |
| | Kiasi cha chini cha kutafutia | USD 25/ YURO 25/PAUNDI 25 | USD 25/ YURO 25/PAUNDI 25 |
| | Kutoa pesa taslimu | 1% kwa muamala | 1% kwa muamala |
| | Kitabu cha Hundi – cha karatasi 25 | USD 10 au kiasi kinacholingana na hicho | HAKUNA |
| | Adhabu ya kutoa pesa zaidi ya kiwango kinachihitajika | Kiwango cha kuanzia + 2%/ Riba ya Mikopo Mikubwa + 2% | Kiwango cha kuanzia+ 2% /Riba ya Mikopo Mikubwa + 2% |
| | TZS Kuhamisha kutoka akaunti ya SH kwenda akaunti ya fedha za kigeni | HAKUNA | HAKUNA |
| SEHEMU C | AKAUNTI ZA KUWEKA FEDHA | | |
| 1 | Akaunti za Uwekezaji | | Akaunti za Uwekezaji |
| | Kiasi/Kima cha chini cha kufungulia | SH.1,000,000 | SH.10,000,000 |
| | Kiasi/Kima cha chini cha uendeshaji | SH.1,000,000 | SH. 10,000,000 |
| | Kiwango cha Salio linalotakiwa kuwamo kwa mwezi | Kulingana na makubaliano | Kulingana na makubaliano |
| | Viwango vya Riba | Kulingana na makubalianio | Kulingana na makubaliano |
| 2 | AKAUNTI ZA MUDA MAALUMU | | AKAUNTI ZA MUDA MAALUMU |
| | Kiasi cha chini kuweka - fedha za ndani | SH. 500,000 | SH. 10,000,000 |
| | Kiasi cha chini cha kuweka fedha –USD | USD 1,000 | USD 10,000 au kiasi kinacholingana na hicho |
| | Viwango vya Riba | Kulingana na makubaliano | Kulingana na makubaliano |
| SEHEMU D | HUDUMA ZA BENKI KIELEKTRONI | | |
| 1 | Huduma za Benki Kielektroni | | Huduma za Benki Kielektroni |
| | Ada ya kila mwezi ya huduma za benki za kielektroni | SH 2,000 kwa Mwezi. | SH.10,000 kwa Mwezi |
| | Huduma za Benki za kimtandao (Utoaji wa nywila mpya) | BURE | BURE |
| | Mfumo wa Benki Kiektroni (Kurejesha muamala) | BURE | BURE |
| | Taarifa za kifedha kielektroni (kupakuliwa na mhusika) | BURE | BURE |
| | Manunuzi POS (ndani ya nchi) | BURE | HAKUNA |
| | Manunuzi ya POS (Kimataifa) | BURE | HAKUNA |
| | Utoaji wa fedha kwa POS | SH.1500 | SH. 1500 |
| | Kurejesha muamala wa Mashine ya kutolea fedha | BURE | HAKUNA |
| | Uhamishaji wa fedha/kiwango kwa kampuni. | SH.1,000 kwa muamala | SH. 1,000 kwa muamala |
| | Kiwango kwa Kadi | SH.1,000 kwa muamala | SH. 1,000 kwa muamala |
| | /Ubadilishaji wa nywila kwa mkono | SH. 1,500 kwa muamala | SH.1,500 kwa muamala |
| | Huduma za kibenki kwa simu (huduma za benki kwa simu kwenda benki –kwenda kwenye waleti) | SH 3,000 (1,000 - 100,000/=), SH 4,000 (100,001 - 200,000/=), SH 5,000 (200,001 - 500,000/=), SH 7,000 (500,001 - 1,000,000/=), SH 10,000 (1,000,001 - Above) | HAKUNA |
| | Uhawilishaji wa fedha kutoka kadi moja hadi nyingine | SH. 1,500 kwa muamala | SH. 1,500 kwa muamala |
| | Kutoa fedha kwenye benki kupitia wakala | | |
| | 1,000-9,999 | SH. 500 | SH. 500 |
| | 10,000-49,999 | SH. 900 | SH. 900 |
| | 50,000-99,999 | SH.1,200 | SH. 1,200 |
| | 100,000-299,999 | SH. 2,000 | SH. 2,000 |
| | 300,000-499,999 | SH. 3,500 | SH. 3,500 |
| | 500,000-1,000,000 | SH. 4,500 | SH. 4,500 |
| | Kutoa fedha kielekrtoni | 2% ya fedha zote zinazotolewa | 2% ya fedha zote zinazotolewa |
| | Kuweka fedha kielektroni | 1.5% ya fedha zote zinazowekwa | 1.5% ya fedha zote zinazowekwa |
| | Africash /Fedha taslimu za Kiafrika | SH. 6000 + 1.5% ya kiasi chote kilichotumwa/UDS 4.45 + 1.5% ya kiasi chote kitakachotumwa | HAKUNA |
| 2 | Kadi ya Mkopo ya Visa | | HAKUNA |
| | Ada za kutolea | SH. 11,800 | |
| | Ada za kutoa tena | SH. 10,000 | |
| 3 | Kadi za Visa za Malipo ya Kabla | | HAKUNA |
| | Ada za utoaji wa kadi papohapo | SH.12,000 | HAKUNA |
| | Ada za Utoaji wa kadi binafsi | SH. 16,000 | HAKUNA |
| | Ada za utoaji tena | SH. 12,000 | HAKUNA |
| | Ada ya kutoa upya nywila mtandaoni | SH. 1,500 | HAKUNA |
| | Ada ya kutoa upya nywila ya mashine ya kutolea fedha | SH. 1,500 | HAKUNA |
| | Ada ya uchakataji | SH.1,000 | HAKUNA |
| | Ada ya ununuzi katika maduka ya mtandaoni –miamala ya nchin | BURE | HAKUNA |
| | Ada za manunuzi ya mtandaoni/Tovuti malipo ya mtandao | BURE | HAKUNA |
| 4 | Utoaji wa Fedha kwenye Mashine za Kutolea Fedha | | HAKUNA |
| | Kwenye ATM za UBA (Kwetu) | SH. 1000 | HAKUNA |
| | Kujua/Kuomba Salio kwenye ATM ndani ya nchi) | SH. 200 | HAKUNA |
| | Kuomba Salio kwenye ATM (Kimataifa) | SH. 1000 | HAKUNA |
| | Kwenye ATM za benki zingine za ndani (za wengine/zetu) | SH. 2,500 | HAKUNA |
| | Kutoa fedha kwenye ATM za Kimataifa | SH. 6000 | HAKUNA |
| | Kutoa fedha kwenye ATM za 'Umoja Switch' | SH.1,300 | HAKUNA |
| SEHEMU E | RASILIMALI ZA BENKI | | |
| 1 | MIKOPO KWA WATEJA | | |
| | Ada ya uchakataji | 2% | HAKUNA |
| | Ada ya Bima | | HAKUNA |
| | | | |
| 2 | MIKOPO | | |
| | Ada ya kushughulikia mkopo | Kulingana na majadiliano | 2% |
| | Bima binafsi kwa ajili ya mkopo | 1.50% | 1.50% |
| | Ada za kisheria | 0.5% ya kiasi cha chini cha SH. 300,000 | 0.5% 0.5% ya kiasi/ cha chini cha SH. 300,000 |
| 3 | DENI LA OVADRAFTI | | |
| | Ada ya ushughulikiaji | 2% | 2% |
| SEHEMU F | BIASHARA YA FEDHA | | |
| 1 | Dhamana | | Dhamana |
| | Kamisheni ya Huduma | 2% kwa mwaka (0.5% kwa robo mwaka. Kima cha chini ni USD 250 kwa robo. | 2% kwa mwaka (0.5% kwa robo mwaka. Kima cha chini ni USD 250 kwa robo. |
| | Ada ya huduma | 2% | 2% |
| | Kiasi kilicholipwa | 0.5% kwa robo Kima cha chini ni 250 kwa robo mwaka. | 0.5% % kwa robo mwaka. Kima cha chini ni 250 kwa robo mwaka. |
| | Marekebisho | USD 100.00 tu | USD 100.00 tu |
| | Nyongeza katika robo inayofuata | 0.5% 05% kwa robo (Au % ya kiasi kilichokubaliwa) | 05% kwa robo (Au % ya kiasi kilichokubaliwa) |
| | Ongezeko la kiasi | 0.5% / robo ya 0.5% kwenye tofauti (Au % ya kiasi kilichokubaliwa) | 0.5% /qtr robo ya 0.5% kwenye tofauti (Au % ya kiasi kilichokubaliwa) |
| 2 | Barua za Mopo – Maduhuli | | Letters of Credit – Imports/ Barua za Mopo – Maduhuli/Biasharandani |
| | Kamisheni ya Utoaji | 0.5% kwa robo. Kima cha chini ni USD 250 | 0.5% kwa robo. Kima cha chini ni USD 250 |
| | Ada za uhifadhi | USD 100 tu | USD 100 tu |
| | Tozo za Haraka? | USD 50 tu | USD 50 tu |
| | Marekebisho | USD 100.00 tu | USD 100.00 tu |
| 3 | Barua za Mopo – Mahuruji | | Barua za Mopo – Mahuruji |
| | Kamisheni ya Ushauri ya Barua ya Mkopo | USD 200 tu | USD 200 tu |
| | Marekebisho ya kamisheni ya Ushauri | USD 100 tu | USD 100 tu |
| | Tozo za Haraka za Ulinganifu | USD 50 tu | USD 50 tu |
| | Ada ya uchunguzi na utunzaji wa nyaraka | 0.5% ya kiasi cha Ankara, kima cha chini cha USD 200 | 0.5% ya kiasi cha Ankara, kima cha chini cha USD 200 |
| | Tozo za msimamizi | USD 100 tu | USD 100 tu |
| | Tozo zilizothibitishwa za Barua ya Mkopo | 1.5% kwa robo (kwa barua za utoaji mkopo zilizothibitishwa) | 1.5% kwa robo (kwa utoaji wa barua za mkopo zilizothibitishwa) |
| 4 | /Barua za Ugharamiaji upya wa Mkopo | | Barua za Ugharamiaji upya wa Mkopo |
| | Riba kwenye ugharimiaji upya | /Kiwango cha msingi cha riba + thamani ya 8% kwa mwaka. Kima cha chini ni USD 100 | Kiwango cha msingi cha riba + thamani ya 8% kwa mwaka. Kima cha chini ni USD100 |
| | Kamisheni ya ugharimiaji upya | USD 50 tu | USD 50 tu |
| 5 | Punguzo kwenye Barua ya Mkopo/Ankara/Hundi | | |
| | Riba kwenye upunguzaji | Kiwango cha msingi cha riba + thamani ya 8% kwa mwaka. Kima cha chini ni USD 100 | Kiwango cha msingi cha riba + thamani ya 8% kwa mwaka. Kima cha chini ni USD100 |
| | Riba kwenye upunguzaji | USD 50 tu | USD 50 tu |
| 6 | Punguzo la Bili(Bili za kubadilisha ikiwa ni pamja na Hundi) | | |
| | Punguzo kwenye riba | Kiwango cha kuanzia + 3% ya nchini; Kiwango cha msingi cha riba ya Kimataifa + 8% | Kiwango cha kuanzia + 3% ya nchini; Kiwango cha msingi cha riba ya Kimataifa +8% |
| 7 | Ukusanyaji nyaraka- Mahuruji | | |
| | Ada za uhifadhi | 0.25% ya Ankara ya kima cha chini cha USD100 tu | 0.25% ya Ankara kima cha chini cha USD 100 tu |
| | Tozo za Msimamizi | USD 100 | USD 100 |
| | Kamisheni ya Ulinganifu | USD 50 kwa kila mfuatiliaji | USD 50 kwa kila mfuatiliaji |
| 8 | Ukusanyaji wa Nyaraka – Maduhuli//Biasharandani | | |
| | Kamisheni ya kuhifadhi | 0.25%. Kima cha chini cha USD100 | 0.25%. Kima cha chini cha USD100 |
| | /Tozo za Haraka Zinazolingana | USD 50 | USD 50 |
| 9 | Bili za Nje kwa ajili ya (Makusanyo stahiki & Kodi Zinazolipwa na Mnunuzi) | | |
| | Kamisheni ya Kuhifadhi | 0.25%. ya thamani, kima cha chini USD 75 au kinachofana na hicho | 0.25%. ya thamani, kima cha chini cha USD 75 au kinachofana na hicho |
| | Tozo za DHL | USD 75 tu | USD 75 tu |
| | Hundi za Kigeni Zilizorejeshwa | Tozo zinazodaiwa + Tozo za ndani ambazo hazijalipwa. | Tozo zinazodaiwa + Tozo za ndani ambazo hazijalipwa. |
| 10 | Bili za Ndani kwa Ajili ya Makusanyo | | |
| | Kamisheni ya kuhifadhi | USD 50 tu kwa kila makusanyo | USD 50 tu kwa kila makusanyo |
| | Iliyotozwa Haraka | USD 40 tu kwa kila makusanyo | USD 40 tu kwa kila makusanyo |
| 11 | Miamala ya Ukusanyaji wa Ndani | | Miamala ya Fedha za Ndani |
| | /Malipo ya Uhamishaji wa Nje(TISS) | SH. 10,000 kwa muamala | SH.10,000 kwa muamala |
| | /Marekebisho ya Ada kwa ajili ya uhamishaji wa nje /wa Haraka/ Uhamishaji wa Telegrafu na mteja au benki | HAKUNA | HAKUNA |
| | Uhamishaji wa Haraka wa Ndani (TISS) | HAKUNA | HAKUNA |
| 12 | Miamala ya Fedha za Kigeni | | Miamala ya Fedha za Kigeni |
| | Malipo ya uhamishaji wa Nje /wa Haraka/ wa Telegrafu | USD 50 FLAT ( SHA), USD 90 ( OURS) | USD 50 FLAT ( SHA), USD 90 ( OURS) |
| | Tozo za Telegrafu za Nje ya nchi/KWETU | Kima cha juu cha USD /YURO/PAUNDI 35-50 TU (KWETU) | Kima cha juu USD/YURO/PAUNDI 35-50 TU (Zinazolipwa kabla) |
| | Marekebisho ya Ada kwa ajili malipo ya ya uhamishaji wa Nje wa Fedha/ wa Haraka/ wa Telegrafu unaofanywa na mteja au benki | USD 10 TU | USD 10 TU |
| | Uhamishaji wa Haraka wa Ndani | USD 5 TU | USD 10 TU |
| | Hawala ya Fedha ya KImataifa | USD 30 kwa Hawala ya fedha ya kimataifa | USD 30 kwa Hawala ya fedha kimataifa |
| | Makusanyo kwa ajili ya Hundi za Kigeni | 0.25% ya thamani. Kima cha chini cha USD75; kima cha juu cha USD 250; | 0.25% ya thamani. Kima cha chini cha USD 75; kima cha juu cha USD 250; |
| SEHEMU G | MENGINEYO | | |
| 1 | Maelezo | | Maelezo |
| | Kwa mwezi | BURE | BURE |
| | Maombi Maalumu | SH. 1,000/UKRASA | SH.1,000/UKRASA |
| 2 | Utoaji wa Vitabu vya Hundi | | Utoaji wa Vitabu vya Hundi |
| | -Vitabu vya karatasi- 25 | SH. 15,000; USD 10 | HAKUNA |
| | - Vitabu vya karatasi – 59 | SH. 30,000; USD 20 | HAKUNA |
| | - Vitabu vya karatasi – 100 | SH. 45,000; USD 30 | SH. 45,000; USD 30 |
| | Maombi ya Kulipwa kwa hundi | SH. 20,000; USDI 10 | SH. 20,000; USD 10 |
| | Maelezo ya Kusitisha Malipo ya Hundi | Upotevu wa karatasi: SH. 20,000; Upotevu wa kitabu SHTZ 40,000; | Upotevu wa karatasi: SH. 20,000; Upotevu wa kitabu SH. 40,000; |
| | Utoaji wa Hundi ya Meneja | SH. 25,000; USD 20 kwa kipengele. | SH. 25,000; USD 20 kwa kipengele. |
| | Ufutaji wa tozo za Hundi za meneja | BURE | BURE |
| 3 | Kanuni Kuu | | Kanuni Kuu |
| | Uanzishaji wa kanuni kuu | SH. 10,000; USD 10 au kiasi kinachofanana na hicho | SH.10,000; USD 10 au kiasi kinachofana na hicho |
| | Utengenezaji wa Kanuni Kuu | HAKUNA | HAKUNA |
| | Kanuni kuu/ Benki za Kigeni (Tozo za TT) | Kima cha chini cha USD 50; 0.25% ya kima cha juu cha USD 200 | Kima cha chini cha USD 50; 0.25% ya kima cha juu cha USD 200 |
| | Kurekebisha/Kusitisha Kanuni kuu | SH.10,000; USD 10 au kiasi kinachofanana na hicho | SH. 10,000; USD 10 au kiasi kinachofanana na hicho |
| | Kanuni kuu zisizolipiwa | SH. 40,000; USD 40 au kiasi kinachofanana na hicho | SH. 40,000; USD 40 au kiasi kinachofanana na hicho |
| 4 | Fedha kidogo/athari hazipo wazi | | Fedha kidogo/athari hazipo wazi |
| | Fedha Kidogo (Mwone mtoafedha) | SH. 50,000; USD 50 | SH. 50,000; USD 50 |
| 5 | Huduma/Tozo Zingine | | |
| | Kuzirejesha Nyaraka za Nyuma (miezi 2-6) | SH.10,000; USD 10 | SH. 10,000; USD 10 |
| | Kuzirejesha Nyaraka (miezi 6 na kuendelea) | SH. 15,000; USD 15 | SH.15,000; USD 15 |
| | Hati ya Uthibitisho/Ukaguzi/ Cheti cha salio | SH. 30,000; USD 20 au kiasi kinachofanana na hicho | SH. 50,000; USD 20 au kiasi kinachofanana na hicho |
| | Maombi ya hali/Barua ya Kumbukumbu/ | SH. 25,000; USD 25 au kiasi kinachofanana na hicho | SH. 25,000; USD 25 au kiasi kinachofanana na hicho |
| | Uthibitishaji wa hundi nje | USD 500 | USD 500 |
| | Ada za uchakataji wa mshahara | SH. 1,500; USD 1 au kiasi kinachofanana na hicho | SH. 1,000; USD 1 au kiasi kinachofanana na hicho |
| | Uamilishaji wa Akaunti isiyofanyakazi | BURE | BURE |
| | Ada ya Uhifadhi wa fedha taslimu –SARAFU PEKEE | 9% ya fedha iliyowekwa | 9% ya fedha iliyowekwa |
| 6 | Noti chakavu | 3% ya kiasi chote | 3% ya kiasi chote |
| 7 | Sarafu | 3% ya kiasi chote | 3% ya kiasi chote |
| | | | |
| | **approved by:** | | |
| | **Signature:** | **(Signed)** | **Signature: (Signed)** |
| | | | |
| | Flavia Kiyanga | | Benson Msangi |
| | **Mkuu wa uendeshaji** | | **Mkuu wa Fedha** |
| | **United Bank for Africa (Tanzania) Ltd** | | **United Bank for Africa (Tanzania) Ltd** |
| | **Disclaimer: All fees are VAT exclusive.** | | |

117225402



Makamu wa Rais wa Vivo Energy wa Ukanda wa Magharibi na Bahari ya Hindi, George Roberts (kushoto), Ofisa Mtendaji Mkuu wa Vivo Energy, Stan Mittelman (wa pili kushoto), Meneja Mauzo, Mhandisi Shaaban Kayungilo (wa tatu kushoto), Mkurugenzi Mtendaji wa Dough Works, Vikram Desai (wa pili kulia), Mkurugenzi wa Dough Works Ltd, Shaffin Jamal (wa tatu kulia) na Mkurugenzi Mkuu wa Vivo Energy Tanzania, Khady Sene (kulia), wakiwa katika hali ya furaha baada ya kuzindua mgahawa wa tano wa BAO katika kituo cha mafuta cha Engen Masaki, jijini Dar es Salaam mapema wiki hii, unaoendeshwa kwa ushirikiano kati ya kampuni ya Dough Works Ltd na Vivo Energy Tanzania na kutoa nafasi zaidi ya 35 za ajira. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Mpango aitaka TFS kupitia upya leseni ukataji miti

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

MAKAMU wa Rais, Dk. Philip Mpango, ameagiza Wakala wa Misitu Tanzania (TFS) kupitia upya utaratibu wa utoaji leseni za ukataji miti kwa ajili ya nishati ya mkaa ili kulinda vyanzo vya maji ambavyo vingi vipo hatarini kukauka.

Alitoa agizo hilo jana baada ya kupanda mti katika Shule ya Msingi Msalato, tukio lililoratibiwa na Ofisi ya Makamu wa Rais Muungano na Mazingira ikiwa ni sehemu ya maadhimisho ya miaka 59, ya Mapinduzi ya Zanzibar.

Alisema ukataji miti kwa ajili ya mkaa nchini unaongezeka kila siku hali inayotishia usalama wa vyanzo vya maji.

"Inabidi mkapitie upya utaratibu huu wa utoaji wa leseni za ukataji miti kwa ajili ya mkaa kwani hivi sasa hali ni mbaya sana kama pale Mzakwe ambako ni chanzo kikuu cha maji kwa jiji la Dodoma, lakini kule juu ya milima watu wanakata miti kwa wingi kwa ajili ya mkaa.

"Kila nikipita barabarani nasikitika sana unakuta misururu ya magunia ya mkaa na shughuli za ukataji miti zikiendelea sasa itafika wakati miti yote ikiisha kule mlimani ambako ndiko eneo muhimu kwa ajili ya vyanzo vyetu vya maji vitakauka mara moja," alisema Dk. Mpango.

Alisema umefika wakati mamlaka husika zihakikishe zinasimamia sheria zilizowekwa ili kulinda mazingira na kuwachukulia hatua kali wote watakao bainika kukiuka.

Aliwaagiza wakuu wa mikoa, wilaya pamoja na wakurugenzi wa halmashauri zote nchini kusimamia maelekezo yalitolewa kwenye Ilani ya Chama Cha Mapinduzi (CCM) kwa kila halmashauri kupanda miti milioni 1.5.

"Niwaagize wakuu wa mikoa, wakuu wa wilaya na wakurugenzi wa halmashauri kuhakikisha kuwa idadi hii ya miti inapandwa na kutunzwa hatuwezi kuwa tunatumia nguvu kubwa kupanda miti harafu watu wengine wanaingiza mifugo yao nilisha waagiza JKT, kwenye eneo lao ikingia mifugo waikamate na kuwapiga faini kali wahusika,"alisema Dk.Mpango.

Pia alisema suala la upandaji miti nchini ni la lazima siyo hiyari hivyo kila mtu anapaswa kutekeleza maagizo ya serikali na kufikia azma yake ya kutunza na kuhifadhi mazingira, ili kukabilina na mabadiliko tabianchi.

Waziri Mkuu mstaafu Mizengo Pinda, akizungumza katika tukio hilo, alisema upandaji miti ni suala muhimu kwa taifa kwakuwa maisha ya mwanadamu yategemea hewa safi ili aishi.

"Suala la kupanda miti ni jambo la lazima sio hiari kwani hata katika vitabu vya dini vimeeleza umuhimu wa miti na imeonekana kuwa bila mimea hakuna uhai, lakini pia tunapopanda mti lazima tushirikishe wataalam ili kama tunataka kupanda mti kwenye chanzo cha maji watueleze ni mti gani unafaa sio kupanda kila mti," alisisitiza Pinda.

Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano na Mazingira), Selemani Jafo, alisema watayafanyia kazi maelekezo yote yalitolewa na Makamu wa Rais, ili kuhakikisha mazingira yana-



# Atakayemwona mtoto huyu atoe taarifa

**Na Maulid Mmbaga**

MKAZI wa Mbagala, jijini Dar es Salaam, Pendo Thomas, ameomba mtu yeyote atakayemwona mtoto wake Ikramu Rashidi (9) aliyepotea tangu Desemba 12, mwaka jana, atoe taarifa kituo chochote cha polisi.

Akizungumza na Nipashe jana, Pendo alisema mwanawe alitoweka nyumbani baada ya kuzozana naye kwa kuwa alikataa kwenda madrasa.

"Mwanangu alikuja na kuniambia mama leo sijisikii kwenda madrasa, wala sehemu yoyote, nilimuuliza kwanini, akasema sijisikii tu kwenda, nilimkemea aende ila hakutaka, baadaye alitoka akakimbia na mimi sikukaa ndani nilitoka huku nikimuita ila hakurudi, nilimfuatilia bila mafanikio," alisema Pendo.

"Kila nilikopita nikiuliza naambiwa kapita muda sio mrefu, wengine wanasema alikuwa anacheza, mimi nikawa najipa imani kwamba mwanangu atarudi kwani ni mara ngapi ananifanyia makusudi, lakini chakusikitisha sijamuona hadi leo," alisema Pendo.

Alisema mwanawe ni mwanafunzi wa Shule ya Msingi Amani iliyoko Buza na ameshatoa ripoti polisi na kupewa RB namba MBL/RB/1802/.

Aidha, aliwaomba Watanzania hasa wakazi wa Dar es Salaam kwa yeyote atakayemwona mtoto wake awasiliane naye kwa namba **0693 040615**, au ampeleke kituo chochote cha polisi kilicho karibu naye.

# Waziri Nape Nnauye aihakikishia SUA mawasiliano

**Na Ashton Balaigwa, KATAVI**

WAZIRI wa Habari, Mawasiliano na Teknolojia, Nape Nnauye, amekihakikishia Chuo Kikuu cha Sokoine cha Kilimo (SUA), Kampasi ya Mizengo Pinda na wananchi wa Halmashauri ya Wilaya ya Mpimbwe, mkoani Katavi kupata mawasilino ya uhakika ya simu pamoja na redio kabla ya mwezi wa sita, mwaka huu.

Waziri Nape alitoa ahadi hiyo juzi alipotembelea kampasi hiyo katika ziara yake ya kikazi na viongozi wakuu wa mashirika yaliyo chini ya wizara hiyo.

Wakuu hao ni Kampuni ya Mawasiliano ya Simu Tanzania (TTCL), Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania (TCRA), Mfuko wa Mawasiliano kwa wote (UCSAF) na Shirika la Utangazaji Tanzania (TBC).

Ziara hiyo ililenga kwenye mikoa ya mipakani mwa Tanzania kuangalia usikivu na huduma za mawasiliano jinsi zinavyowafikia wananchi wanaoishi maeneo hayo.

Alisema kwa sasa mawasiliano ndiyo kila kitu na siku za usoni suala la mawasiliano litakuwa kitu kingine kikubwa na kwamba itafika mahali kutokuwa na mawasiliano ni sawa na kutokuishi hivyo serikali itahakikisha inaweka mawasiliano ya uhakika kwani ni sehemu ya haki za binadamu.

"Kwenye kazi za utafiti kama za kwenu hapa SUA usipounganishwa na mawasiliano utashindwa kufanya kazi na kutimiza wajibu wako sawasawa, hapa kwenu mnayo huduma kidogo ya TTCL na nimekuja na Mkurugenzi Mkuu wa TTCL aseme mwenyewe atafanya nini maana maagizo yalitoka kwa Waziri Mkuu mstaafu Mizengo Pinda, lazima yatekelezwe," alisema Nape. Alisema alikutana na Waziri Mkuu mstaafu Pinda akimueleza kwenye Kata ya Kibaoni katika jimbo hilo kuna kampasi ya SUA na imepewa jina lake, lakini wanahangaika kupata mawasiliano kutokana na tatizo la mtandao kitu ambacho kinawakwamisha shughuli za utafiti.

"Wakati ananieleza hayo akijua mimi ndio Waziri mwenye dhamana , nikamwambia Mzee nimekusikia ngoja nione nitafanyaje ndio maana leo nimekuja na Mkurugenzi wa TTCL aeleze mwenyewe jinsi atakavyoboresha mawasiliano hapa" alisema Nape.

Akijibu namna ya kumaliza tatizo hilo Mkurugenzi Mkuu wa TTCL Mhandisi. Peter Ulanga alisema kwa kuanzia wataboresha huduma ya mtandao wanaotoa kwenye kampasi hiyo na hatua itakayofuata ni kupeleka Mkongo wa Taifa kutoka kwenye kituo chao hadi kufika chuoni hapo mpango utakaokamilika kabla ya mwezi wa sita mwaka huu.

"Sisi kama TTCL tumeshafanya kikao na Makamu Mkuu wa Chuo Kikuu cha Sokoine Profesa Raphael Chibunda kule kampasi Kuu wameshatupatia mpaka eneo la kujenga Community WiFi ambapo tunaweka WiFi mahali na wanafunzi wanaweza kuitumia," alisema.

Mtendaji Mkuu wa UCSAF, Justina Mashiba, alisema ni jukumu la taasisi yake kupeleka huduma za mawasiliano vijijini kwa kuwa makampuni ya simu yanaona kuna baadhi ya maeneo ya vijijini hayapati faida hivyo serikali itaongeza ruzuku, ili watanzania wa maeneo hayo wapate huduma za mawasiliano.

Awali akisoma taarifa fupi ya kampasi hiyo Rasi wa Ndaki ya Mizengo Pinda, Profesa Josiah Katani alisema pamoja na mafanikio makubwa yaliyopatikana toka kunzishwa kwa kampasi hiyo mwaka 2019, ikiwemo kuleta mageuzi kwenye sekta ya elimu na kilimo nchini lakini wanakabiliwa na changamoto mbalimbali hasa ya mawasiliano.

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# DART usafiri huu wa wanafunzi uwe endelevu

**MWANZONI** mwa wiki hii Wakala wa Mabasi Yaendayo Haraka (DART), iliongeza idadi ya mabasi kwa ajili ya kurahisisha usafiri wa kwenda na kurudi kwa wanafunzi wa shule za msingi na sekondari jijini Dar es Salaam.

Hatua hiyo ilichukuliwa baada ya shule zote za msingi na sekondari kufunguliwa Jumatatu iliyopita na kusababisha mahitaji makubwa ya usafiri kwa wanafunzi wakati wa kwenda na kurudi.

Kwa mujibu wa maelezo ya viongozi wa DART, waliamua kuchukua uamuzi huo baada ya kuona ongezeko kubwa la wanafunzi wa shule za msingi na za sekondari lililochagizwa na sera ya serikali ya elimu bure.

Chini ya utaratibu huu wa DART mabasi mawili yanayobeba watu 150 yatasafirisha wanafunzi kuanzia saa 12 asubuhi kutoka Kimara kwenda Kivukoni na mawili yatawasafirisha kutoka Kimara muda kama huo kwenda Gerezani na kufanya hivyo tena jioni. Sisi tunaona hatua hii ni muhimu na ya kupongezwa kwani itawapunguzia adha ya usafiri wanafunzi wengi wakati wa asubuhi na jioni wanaporudi nyumbani.

Wanafunzi wengi wamekuwa wakipata shida ya usafiri kwenye daladala hasa asubuhi kutokana na wingi wa abiria hivyo kuchukua hatua ya kuwatengea mabasi maalumu ya kuwasafirisha na hivyo kuwa jambo jema na la busara.

Imekuwa kawaida kuona msururu wa wanafunzi kwenye vito vya daladala wakisubiri usafiri nyakati za asubuhi na jioni muda ambao kunakuwa na shida kubwa ya usafiri kutokana na wafanyakazi wengi pia kuhitaji usafiri huo.

Uzoefu unaonyesha mwanafunzi anapokuwa kwenye mazingira mazuri ya kusomea kama kupata usafiri mzuri unaomfikisha shule na kurudi nyumbani kwa wakati anakuwa na uwezekano mkubwa kufanya vziuri kwenye masomo yake.

Utaratibu huu wa DART utawafanya wanafunzi wa shule za sekondari na msingi kusafiri kwa raha na bila msongamano na kuwasaidia kuwahi shuleni nyumbani.

Sisi tunaona uamuzi huu umekuja wakati muafaka na unahitaji kuwekewa utaratibu mzuri ili uwe endelevu na ikiwezekana DART iongeze ruti zingine za wanafunzi pale miundombinu ya mabasi yake itakapokamilika kwenye maeneo mengine ya Jiji la Dar es Salaam. Kwa sasa wanafunzi wa shule sita za Kimara, saba za Kivukoni, 14 za Gerezani na saba za Ubungo wananufaika na usafiri huo.

Tunatarajia baada ya kukamilika kwa miundombinu mingine ya DART kwenye maeneo mengine ya Jiji la Dar es Salaam ikiwamo ruti ya Mbagala-Gerezani, itaona umuhimu kutenga mabasi mengine kwa wanafunzi wa ukanda huo ili nao waweze kuwahi shuleni na kurejea makwao. Kwa kuwa imekuwa kawaida kuona mambo mazuri kama haya yakianzishwa na kupotea katika kipindi kifupi hatutarajii hili nalo litakuwa la kupita.


Ni vyema sasa serikali kupitia wakala wa DART ikasimamia kwa weledi mpango huu kuhakikisha unakuwa imara na endelevu kwa kuwa utawasaidia wanafunzi kuondokana na msongo wa mawazo unaotokana na purukushani za usafiri wa kwenda shule na kurudi. Utulivu wa wanafunzi wanapopata usafiri wa uhakika utasaidia kuongeza maendeleo ya taaluma shuleni kwani wanafunzi watafika shuleni kwa wakati na wakiwa hawana uchovu na vivyo hivyo watakaporudi nyumbani.

Na kwa kuwa mwishoni mwa mwaka jana Mkurugenzi Mtendaji wa DART, Dk. Edwin Mhede, aliahidi kuwa wanatarajia kuongeza mabasi mengine 177 ili kuboresha huduma hiyo ni vyema wakafikiria kuongeza tena idadi ya mabasi ya kubeba wanafunzi pekee hata wakati wa mchana.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:

THE GUARDIAN LIMITED

**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0782 253676
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com






Na Adam Fungamwango

## Muungwana Lazima Nilonge

# Hongera DART, ila kuna mapungufu, njia ya Kinondoni, Mwananyamala mmetusahau

**MOJA** ya vitu ambavyo wazazi wengi wa Dar es Salaam wamefurahishwa navyo ni kuwepo kwa mabasi maalum ya wanafunzi wa shule za msingi na sekondari.

Wakala wa Mabasi yaendayo haraka (DART) ilianza mpango mkakati wa kutoa mabasi mawili kwa ajili ya kuunga mkono sera ya serikali ya elimu bure ambayo imesababisha ongezeko kubwa la wanafunzi nchini, hususan jiji kubwa la Dar es Salaam.

Kwa kuona uhitaji bado unahitajika, Mkurugenzi wa uendeshaji na Usimamizi wa Miundombinu Dk. Philemon Mzee amesema wamelazimika kuongeza mabasi mengine marefu yenye mita 18 na kuwa manne.

"Tulianza na mabasi mawili, lakini kutokana na mwitikio kuwa mkubwa tumeongeza yawe manne na ni yale marefu yenye mita 18 yanayobeba watu wazima 150," alisema Dk. Mzee.

Akasema kuwa mabasi hayo maalum tu kwa wanafunzi, yanaanza safari zake kuanzia saa 12:00 asubuhi na saa 12:20 yakitokea Kimara kwenda Gerezani mawili, na mengine mawili yakitokea Kimara kwenda Kivukoni.

Na pia jioni hutoka Kivukoni kuanzia saa 10:30 kwenda Kimara na saa 11:00 jioni kutoka Gerezani Kwenda Kimara. Mbali na wanafunzi, lakini mabasi hayo pia wanaruhusu kupanda watu walio kwenye makundi maalum kama wazee, wajawazito na walemavu.

Nimpongeze Dk. Mzee, na DART kwa ujumla kwa kuja na ubunifu na mkakati huo ambao mbali na kuwezesha wanafunzi na watu wa aina hiyo kusafiri bila matatizo yoyote, lakini pia inaweza ikawa ni njia ya kupunguza idadi kubwa ya watu vituoni na kwenye mabasi yote na si mwendokasi pekee.

Pia wazo hilo limesababisha wanafunzi wengi kuwahi shuleni na kurejea majumbani kwenye muda rafiki.

Inatia huruma na huzuni kwa wakati mmoja unaona mwanafunzi anaamka alfajiri kuliko hata wazazi wake, anakwenda kituoni kwa ajili ya kusaka usafiri wa kwenda shule, lakini anashindwa kugombea kwa sababu hana ubavu wa kusukumana na watu wazima, hivyo anakaa hapo mpaka jua linatoka, wakati mwingine hadi saa nne. Anapofika shuleni kachelewa mwalimu hajui hilo, atamuadhibu tu.

Na wakati wa kurejea mara nyingi utakuta wazazi wanawahi kurejea majumbani kabla ya watoto wao. Hilo huwa linawaumiza sana wazazi. Mtoto anaondoka kabla yake na anarejea anamkuta yupo nyumbani.

Naishauri DART iangalie changamoto chache zilizopo na kuwe na usimamizi mzuri ili mpango huu uwe endelevu kwani likitokea tatizo lolote lile, basi wanafunzi watarejea tena kule kule tena kuanza kusukumana na watu vituoni, wakati mwingine wakikatazwa kuingia kwenye mabasi. Na hata wakiingia humo ndani kuna baadhi ya daladala wananyanyaswa humo bila ya kuwa na msaada wowote, kwani nimeshuhudia wasafiri wengi wamekuwa kimya na hawasemi lolote wanapoona wanafunzi wanasemwa vibaya au kutolewa maneno yasiyofaa na baadhi ya makonda.

Nadhani shule nyingi za mjini zikiwemo Muhimbili, Mchakichini, Olimpio, Gerezani, Mchikichini, Forodhani na nyinginezo zimenufaika na mpango huo.

Lakini pamoja na yote hayo, nimeangalia nimeona mabasi yote hayo manne yanatoka eneo moja ambalo ni Kimara.

Ina maana wanafunzi wanaoishi, Kimara, Ubungo, Manzese, Sinza, Magomeni na sehemu zinazopakana kidogo na maeneo hayo ndiyo wanaonufaika.

Naishauri sasa DART kuangalia pia uwezekano wa kutoa pia mabasi angalau mengine mawili yaanzie kwenye maeneo ya Kinondoni Morocco kwenda Kivukoni na Gerezani.

Nimesema hivyo kwa sababu DART ina njia yake kwenye barabara hiyo, lakini sijaona nako wanafunzi wakipelekewa mabasi.

Nafikiri eneo la Kinondoni Morocco lina idadi kubwa ya wanafunzi kwa sababu linakusanya maeneo mengine mbalimbali kama Kinondoni zote A, B, Manyanya, Mkwajuni, Studio, Muslim , Moscow, Msasani, Makumbusho, Mwananyamala, Tandale ambako wanafunzi watakuwa wakitoka majumbani kwao na kusogea vituoni kusubiri mabasi.

Maeneo niliyoyataja hapa kwa jiografia ya Dar es Salaam yana wakazi wengine wanaokaa eneo moja, maarufu kama 'uswahilini', hivyo pia kuna wanafunzi wengi wanaohitaji huduma hiyo. Vile vile hapa kuna wakazi wengine pia ambao wapo kwenye makundi maalum nao wanahitaji kunufaika na huduma hiyo.

Nadhani DART kwa sababu wameonyesha nia ya uthubutu huo wa kujali, na hilo nafikiri watalitekeleza.

HABARI KITAIFA



Msemaji wa Wizara ya Mambo ya Nje ya China, Wang Wenbin, akiongea na waandishi wa habari katika Wizara ya Mambo ya Nje, Beijing. **PICHA: WIZARA YA MAMBO YA NJE YA CHINA**

# China yapinga vizuizi vya kibaguzi

**Na Mwandishi Maalumu**

SERIKALI ya China inapinga vikali baadhi ya nchi kuchukua hatua za kibaguzi za vizuizi vya kuingia kwa watu vinavyoilenga China.

Kwa mujibu wa Tovuti ya Gazeti la Umma ya nchi hiyo, Msemaji wa Wizara ya Mambo ya Nje ya China, Wang Wenbin, alisema hayo Jumanne iliyopita mjini Beijing.

Wang aliyasema hayo kwenye mkutano na waandishi wa habari alipojibu swali kuhusu tangu China itangaze uamuzi wa kushughulikia udhibiti wa UVIKO-19 kwa kuchukua hatua dhidi ya magonjwa ya kuambukizia ya aina ya B na hatua za mpito za usafiri wa kuvuka mpaka, nchi nyingi zimekaribisha, lakini nchi chache zimetangaza hatua za kuzuia watu kuingia zinazolenga wasafiri kutoka China.

"Kwa dhati kubwa, upande wa China ulikuwa na mawasiliano ya msingi na nchi zinazohusika na kufafanua juu ya kukamilisha kisayansi na kwa kufaa hatua zetu za kukabiliana na UVIKO na hali ya sasa ya China," alisema.

Kwa masikitiko, nchi chache, kwa kupuuza sayansi, ukweli na hali yao halisi ya janga, zimesisitiza kuchukua hatua za kibaguzi za kuzuia watu kuingia zinazoilenga China, alisema.

Wang alisema; "Kwa mara nyingine tena tunatoa wito kwa nchi zinazohusika kuhakikisha kuwa hatua zao za kukabiliana na UVIKO ni zenye msingi wa ukweli, wa kisayansi na kulingana na hali, na mwitikio wa kukabiliana na COVID haupaswi kutumiwa kama kisingizio cha udanganyifu wa kisiasa."

Alisema mwitikio wa kukabiliana na UVIKO haupaswi kuwa wa kibaguzi na kuathiri usafiri wa kawaida wa kuvuka mipaka na mabadilishano kati ya watu na ushirikiano.




Waziri wa Fedha na Mipango, Dk. Mwigulu Nchemba (kulia), akizungumza na Mkurugenzi wa Kampuni ya Multy Mazao Ltd, Riyaz Khan, baada ya kufungua kongamano la kodi kitaifa, jijini Dar es Salaam juzi. **PICHA: MIRAJI MSALA**

# Waziri ataja mbinu kutatua tatizo la ajira

**Na Halfani Chusi**

WAZIRI wa Fedha na Mipango, Dk. Mwigulu Nchemba, amesema ili kumaliza tatizo la ukosefu wa ajira nchini, sekta binafsi zinapaswa kusimama imara na kupewa ushirikiano wa dhati kutoka serikalini.

Mwigulu aliyasema hayo juzi jijini Dar es Salaam, kwenye kongamano la uzinduzi mpango wa kodi kitaifa wenye kaulimbiu 'Maboresho ya sera kwa maendeleo ya watu'.

Kongamano hilo lilihudhuriwa na viongozi mbalimbali wakiwamo manaibu waziri, makatibu wakuuu, wafanya biashara wakubwa na wadogo, maofisa toka Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA), na viongozi kutoka taasisi za dini.

Nchemba alisema sekta binafsi ni nyenzo muhimu kwenye kumaliza tatizo hilo, akibainisha kuwa idadi ya wanafunzi wanaoingia kwenye soko la ajira na nafasi zilizoko serikalini ni tofauti.

Alisema wanafunzi wasiopungua milioni moja kila mwaka huingia kwenye soko la ajira na wahitimu wa idadi hiyo hawahitaji serikali pekee pia wanahitaji sekta binafsi ili wote waweze kupata ajira.

"Zamani mambo yote yalikuwa yanaweza kufanywa na serikali, watu walikuwa hawaoni nafasi ya sekta binafsi miaka ya nyuma wanafunzi walikuwa wanapewa ajira wakiwa vyuoni kwa sababu wasomi walikuwa wachache kuliko mahitaji kipindi hicho.

Pia, alisema mtu yeyote anayeanzisha shughuli ya uzalishaji anatakiwa aheshimiwe kwa kupewa ushirikiano wa kutosha na serikali kwa sababu anatengeneza ridhiki za wengi na watendaji wote walioko serikalini wanatakiwa wamkimbilie na kumpa msaada.

"Tunavyo tafakari hapa tuitafakari na kodi na ushuru kama sehemu ya kukuzia uchumi pamoja na kutoa ushauri na maoni yatakayo isaidia serikali kwenye kufanyia maboresho ya kodi."

Alikemea wafanyabiashara wasiodai na kutoa risiti kwamba tabia hiyo inarudisha nyuma maendeleo ya taifa.

Alisema kuna baadhi ya wafanyabiashara wana waongoza wananchi kukwepa kodi kwa kutoa risiti bandia hali inayomshawishi mteja kukwepa kodi.

"Kuna muda mfanyabiashara anamuongoza mwananchi anamwambia kama unanunua bidhaa hii nikupe bei isiyo na risiti ya TRA au nikupe kwa bei ya risiti ya TRA."

"Mwananchi yeyote anapofanya shughuli ya kulipa kodi aone sio jambo la TRA bali ni wajibu wake kwa mujibu wa sheria za nchi yetu," alisema.

Juma Msuya mfanyabiashara aliyehudhuria kongamano hilo aliomba serikali kufanya mikutano hiyo mara kwa mara ili kuwarahisishia kuwasilisha kero zao.

**KABWELA** **Na Fadhili Mohammed**



# TCRA CCC yaingilia kati kupaa bei vocha

**Na Christina Mwakangale**

BARAZA la Ushauri la Watumiaji wa Huduma za Mawasiliano (TCRA CCC), limewataka watoa huduma za vocha na wauzaji wa huduma hiyo rejareja, kutofanya mabadiliko yoyote kwa lengo la kujipatia kamisheni, kwa mbinu ya kumbebesha mnunuzi gharama kila anaponunua muda wa maongezi.

Aidha, limesema wauzaji wanaofanya hivyo ni kosa la jinai na kwamba itolewe taarifa kituo cha polisi kwa hatua za kisheria, likisema wakati changamoto hiyo ikitatuliwa, watumiaji na wanunuzi wa muda wa maongezi wanunue kupitia simu za mkononi. Kwa mujibu wa taarifa iliyotolewa jijini Dar es Salaam, jana na Katibu Mtendaji wa Baraza hilo, TCRA CCC imebaini hivi karibuni kumekuwa na malalamiko ya watumiaji wa huduma za mawasiliano kuhusu kupanda kwa bei za vocha za simu za mkononi katika maeneo mbalimbali.

Taarifa ilisema, bei hizo zimekuwa zikitofautiana baina ya wauzaji na kusababisha malalamiko kutoka kwa watumiaji, huku likitaka watoa huduma kujadiliana na mawakala wao namna bora ya kutoza kamisheni bila kumwongezea mtumiaji mzigo.

"Taarifa mbalimbali baraza lilizopata kupitia kamati za watumiaji za mikoa, pamoja na taarifa zinazosambaa kupitia vyombo vya habari, zinaonyesha kuwa vocha ya Sh. 500 inauzwa kwa 550 hadi 600. Vivyo hivyo vocha ya Sh. 1,000 kuuzwa kwa 1,100 hadi 1,200. Aidha, taarifa ilisema gharama za vocha za simu hazijapanda watumiaji wanapaswa kununua vocha kwa bei husika ambayo inaandikwa katika vocha anayonunua, pia muuzaji yeyote anayeuza vocha kwa bei tofauti na iliyoidhinishwa anafanya kosa la jinai na aripotiwe kituo cha polisi.

"Baadhi ya watoa huduma wameeleza kwamba wamefanya mabadiliko katika kamisheni wanazopata wasambazaji wakubwa wa huduma za vocha. Wasambazaji wakubwa wameshusha makato ya kamisheni kwa wauzaji wadogo wa rejareja na wauzaji wa rejareja wameongeza gharama za vocha kwa watumiaji," ilisema taarifa hiyo. "Kamisheni kwa wauzaji wa jumla haipaswi kubebeshwa mtumiaji wa mwisho kwa kuwa makubaliano ni kati ya mtoa huduma na mfanyabiashara husika."



Katibu Mtendaji wa Baraza, TCRA CCC, Mary Msuya

Pia taarifa ilisema Baraza litaendelea kufuatilia hali hiyo na kushauri hatua za kuchukua kwa haraka, ili watumiaji wa huduma za mawasiliano wapate haki ya kupata huduma kwa bei halali na yenye ubora. "Baraza la Ushauri la Watumiaji wa Huduma za Mawasiliano Tanzania, limeanzishwa chini ya Sheria ya Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania (TCRA) ya Mwaka 2003 iliyorekebishwa Mwaka 2017 kwa lengo la kuwakilisha maslahi ya watumiaji wa huduma za mawasiliano kwa kushauriana na serikali, TCRA na watoa huduma za simu, intaneti, utangazaji na Posta."


MWANGA HAKIKABANK

MWANGA HAKIKA BANK LIMITED
MINIMUM DICLOSURE OF CHARGES AND TARIFFS

| PRODUCTS/ SERVICES | BUSINESS CURRENT A/C | PREMIUM CURRENT A/C | PERSONAL SAVING A/C | SALARY A/C | MTOTO SAVING A/C | JIPANGE SAVING A/C | WEKEZA GROUP A/C | MALENGO SAVING A/C | FOREX ACCOUNT USD & EURO | JIWEKEE SAVING A/C | MHB PAMOJA A/C | MSOMI ACCOUNT |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| Account opening | 100,000.00 | 50,000.00 | 20,000.00 | 0 | 10,000.00 | 10,000.00 | 20,000.00 | 100,000.00 | 10 | 0 | 50,000.00 | 10,000.00 |
| Minimum operating Balance | 100,000.00 | 50,000.00 | 10,000.00 | 5,000.00 | 5,000.00 | 0 | 10,000.00 | 100,000.00 | 10 | 10,000.00 | 50,000.00 | 5,000.00 |
| Interest Payable | N/A | N/A | 3.00% | 3.00% | 6.00% | 2.00% | 3.00% | 2% < 10Mil, 4%>=10Mil | 0.50% | 2.00% | 2% | 3.00% |
| Interest bearing amount | N/A | N/A | 50,000.00 | 50,000.00 | 50,000.00 | 50,000.00 | 50,000.00 | 100,000.00 | 5,000.00 | 20,000.00 | 500,000.00 | 20,000.00 |
| Monthly Mantainance fee | 20,000.00 | 10,000.00 | 2,500.00 | 2,500.00 | Free | Free | Free | Free | 2 | Free | Free | Free |
| Deposit | Free | Free | Free | Free | Free | Free | Free | Free | Free | Free | Free | Free |
| Monthly Statement | Free | Free | Free | Free | Free | Free | Free | Free | Free | Free | Free | Free |
| Adhock statement Per page | 2,000.00 | 2,000.00 | 2,000.00 | 2,000.00 | 2,000.00 | 2,000.00 | 2,000.00 | 2,000.00 | 1 | 2,000.00 | 2,000.00 | 2,000.00 |

OTHER CHARGES

| SERVICES | AMOUNT ( TZS) |
|---|---|
| Certificate of Balance | 30,000.00 |
| Confirmation to the Auditors | 30,000.00 |
| Search for information above 5 years | 15,000.00 |
| Cheque book cost (Per Leaf) | 600.00 |
| Status report | 30,000.00 |
| Stop payment order | 30,000.00 |
| Dishonoured cheque for lack of funds or refer to drawer or effect not cleared | 100,000.00 |
| Dishonoured cheque due to the technical error caused by customer | 60,000.00 |
| Dormant Account Activation | Free |
| Account Closing on Customer Demand | 10,000.00 |
| Counter cheque per leaf [Within the Bank] | 15,000.00 |
| Salary Processing fee [ per Transaction] | 1,000.00 |
| Customer ID | 10,000.00 |
| Pre-Mature breaking of Fixed Deposit on customer request | Minimum of 50% of the accrued interest |
| CCTV Camera footage searching request from Customer | 30,000.00 |
| Uncollected Cheque Book/Destruction | 5,000.00 |
| Visa Card Issuance-Classic | 10,000.00 |
| Visa Card Issuance-Gold | 15,000.00 |
| Replacement Visa Card-Classic | 15,000.00 |
| Replacement Visa Card-Gold | 25,000.00 |
| Umoja Card Mantainance fee | 1000 per month |
| Visa Card- Classic Mantainance fee | 3,000 per QTR |
| Visa Card-Gold Mantainance fee | 5,000 per QTR |
| Uncollected ATM Card | 5,000.00 |
| PIN reset fee | 5,000.00 |
| Withdraw fee local (Umoja ATM) | 1000-99,000=1500 100,000-400,000=1700 |
| Withdraw fee other Bank (Domestic Banks) | 3,500 |
| Withdraw fee other Bank (International) | 11,000 |
| Balance inquiry Umoja ATM | 300 |
| Balance inquiry other Domestic Banks | 950 |
| Balance inquiry other Bank (International) | 2,000 |
| Decline Domestic [Insufficient fund] | 1,000 |
| Decline International [Insufficient Balance] | 1,500 |
| QR transactions | 3% of Transaction Amt |
| POS transactions | 3% of Transaction Amt |
| E-commerce transactions | 3% of Transaction Amt |

Cash Withdraw Over the Counter [TZS/ USD/EURO]

| TRANSACTION AMOUNT | RATES |
|---|---|
| Wekeza/Jiwekezee | 2,000.00 |
| Bellow 10 Mil | 3,000.00 |
| Above 10Mill to 50 Mil | 0.10% |
| Above 50Mil t0 100 Mil | 0.090% |
| Above 100Mil to 300 Mil | 0.089% |
| Above 300 Mil | 0.079% |

Cash Withdraw Over the CounterForeign Currency [USD/EURO]

| TRANSACTION AMOUNT | RATES |
|---|---|
| Below USD/EURO 4,000 | 2 |
| Above USD/EURO 4000 | 0.1% more than USD/EURO 40 |

AGENCY BANKING CHARGES

| TYPE OF SERVICES | RATES |
|---|---|
| Deposit | Free |
| Balance Inquiry | 500 |
| Min Statement | 700 |
| Transfer of fund within MHB | 2,000 |
| Transfer of funds to other Bank | 13,000 |

AGENCY BANKING WITHDRAWAL FEE

| AMOUNT | FEE |
|---|---|
| Up to 50,000 | 850.00 |
| 50,000 - 100,000 | 1,000.00 |
| 100,000 - 300,000 | 2,000.00 |
| 300,000 - 500,000 | 3,500.00 |
| 500,000 - 1,000,000 | 4,500.00 |
| 1,000,000 - 3,000,000 | 6,000.00 |
| 3,000,000 - 5,000,000 | 10,000.00 |

MOBILE BANKING CHARGES

WITHDRAWAL CHARGES

| MINIMUM [TZS] | MAXIMUM [TZS] | RATES [TZS] |
|---|---|---|
| 0 | 10,000 | 800 |
| 10,001 | 19,999 | 1,800 |
| 20,000 | 49,999 | 3,500 |
| 50,000 | 99,999 | 5,200 |
| 100,000 | 199,999 | 7,200 |
| 200,000 | 499,999 | 8,200 |
| 500,000 | 999,999 | 10,500 |
| 1,000,000 | 2,000,000 | 11,200 |
| 2,000,001 | 3,000,000 | 12,000 |
| 3,000,001 | 5,000,000 | 15,000 |

FUND TRANSFER CHARGES

| | |
|---|---|
| Transfer of Funds within MHB | 2,000.00 |
| Transfer of funds to other Banks | 13,000.00 |

EFT/SWIFT/TISS

| | |
|---|---|
| EFT within the Bank (Incoming) | Free |
| EFT to other Banks | 1,500.00 |
| TISS Transfer | 10,000.00 |
| T.T. Transfer | - |

STANDING ORDER

| | |
|---|---|
| Instructions within MHB | FREE |
| Standing Order to other Bank | 10,000/= |

www.mhbbank.co.tz

117223302


# Hukumu ya wanaodaiwa kuiba kontena la pedi, Januari 26

**Na Grace Gurisha**

MAHAKAMA ya Hakimu Mkazi Kisutu, Dar es Salaam inatarajia kutoa hukumu Januari 26, mwaka huu dhidi ya makarani wanne wa Bandari ya nchi kavu ya PMM wanaotuhumiwa kuiba kontena mbili za taulo za kike.

Makarani hao ni Pasco Mtaki, George Shauri, Adam Mzava na Munasary Salim, jana walimaliza kujitetea na wakili wao Shamo Shedrack, kufunga utetezi wao.

Hukumu hiyo inatarajiwa kutolewa na Hakimu Mkazi Mwandamizi, Ramadhani Rugemalira, baada ya usikiliza mashahidi wa upande wa mashtaka na utetezi wa washtakiwa.

Hakimu Rugemalira alisema atatoa hukumu Januari 26 na washtakiwa wako nje kwa dhamana.

Upande wa mashtaka katika kesi hiyo ulipeleka mashahidi 10 na vielelezo kadhaa kwa ajili ya kuthibitisha kesi yao.

Washtakiwa wote wanakabiliwa na mashtaka mawili ambayo ni kula njama kwa nia ya kutenda kosa na wizi wa kontena mbili.

Katika shtaka la kwanza wanadaiwa Mei 8, mwaka 2017 maeneo ya Bandari ya nchi kavu Dar es Salaam, walikula njama kwa nia ya kutenda kosa.

Katika shtaka la pili inadaiwa siku hiyo na maeneo hayo washtakiwa waliiba kontena mbili za taulo za kike katoni 5,390, zenye thamani ya Dola za Marekani 20,000 mali ya PMM.



# Uzalishaji wataalamu VETA waitangaza Tanzania kimataifa

**Na Godfrey Mushi,** MOSHI

UMAHIRI wa Chuo cha Ufundi Stadi (VETA) Moshi, kuzalisha wataalamu wabobezi wa fani za ufundi na utaalamu wa kada mbalimbali nchini umeanza kuitangaza Tanzania kimataifa.

Hali hiyo imesababisha baadhi ya Watanzania kuanza kuajiriwa katika nchi za Mauritania, Congo DRC na Ghana.

Akizungumza jana na wakufunzi, watumishi na wakuu wa vyuo vya VETA vya mikoa ya Kilimanjaro, Arusha, Manyara na Tanga, Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia, Prof. Adolf Mkenda, alisema licha ya Watanzania hao kufungua milango kwa wengine, anatamani Bodi ya VETA, chini ya Mwenyekiti wake Peter Maduki, wajitangaze ili watu wajue kuna fursa kubwa ambazo zinaweza zikawapeleka watu mbali.

"Nimemwambia Mwenyekiti wa Bodi, Peter Maduki, mjue na nyie kutamba kidogo. Kuna faida nyingi sana, kwanza kuhimiza watu wengine kuja kuungana na sisi katika juhudi hizi ili tuweze kwenda mbele na pili watu wajue kuna fursa kubwa hapa ambazo zinaweza zikawapeleka watu mbali.

"Kwa mfano, nimefurahi sana utaratibu mlionao wa mafunzo ambayo yanaunganisha moja kwa moja kwenye shughuli halisi za uzalishaji wa viwanda, mfano kwenye madini. Kwamba watu wanafundishwa hapa, lakini kuna mawasiliano ya moja kwa moja. Mwanafunzi akitoka VETA uwezekano wake wa ajira ni zaidi ya asilimia 90," alisema.

Aidha, Waziri Prof. Mkenda aliagiza kuanzishwa kanzidata ya taifa ya utambuzi wa wahitimu wa vyuo vya ufundi stadi nchini (VETA), huku akitaka walioajiriwa nje ya nchi kufuatiliwa na kuwashawishi kuisaidia Tanzania kuvutia wengine kuacha alama katika tasnia hiyo.

Kuhusu sekta ya ajira, Prof. Mkenda alisema serikali iko tayari kuwachukua wanaohitimu VETA, lakini suala la maboresho na mikakati ya kusukuma jambo hilo, liko chini ya menejimenti ya VETA.

Mkurugenzi wa VETA Kanda ya Kaskazini, Monica Mbelle, akizungumza katika kikao hicho, alisema sasa hivi kanda hiyo ina vyuo 13 ambapo kati ya hivyo sita ndio vinavyotoa mafunzo na saba vipo katika hatua za umaliziaji.

Alisema; "Mahitaji ya ufundi stadi katika kanda yetu ni makubwa, tuna jumla ya udahili kwa mwaka uliopita wa mafunzo zaidi ya wanafunzi 4,000 wanaosoma katika vyuo vinavyomilikiwa na VETA lakini kuna vyuo zaidi ya 100 vinavyomilikiwa na taasisi mbalimbali, hii inaonyesha ni jinsi gani mafunzo ya ufundi stadi yalivyokuwa makubwa katika kanda yetu".

# Manyara yaanza kuvisajili kidigitali vyama vya ushirika

**Na Jaliwason Jasson,** BABATI

MKOA wa Manyara umeanza kuvisajili upya kwa mfumo wa dijitali vyama vya ushirika ili kuisaidia serikali kujua takwimu sahihi za vyama hivyo na kutengeneza utaratibu maalum wa namna ya kuvikagua.

Akizungumzia usajili huo jana, Mrajis Msaidizi wa Vyama vya Ushirika mkoani humo, Absalom Cheliga, alisema tangu wameanza usajili wa vyama kwa mfumo huo mpaka sasa wameshasajili vyama 40.

"Vyama vyote vitafanyiwa usajili mpya na mpaka sasa tunaendelea na kazi hiyo. Moja ya faida kubwa ya mfumo huo ni kusaidia kurahisisha ukaguzi wake na unatoa fursa kwa wadau kuzingatia maelekezo ya serikali ya namna ya kupitisha bajeti zao.

"Lakini tutautumia mfumo huu kwa ajili ya kupunguza gharama za usimamizi kwa wasimamizi wa vyama na usimamizi kwa vyama vyenyewe.

Niwaombe watendaji na viongozi wa vyama vya ushirika, kuacha kujitenga na jamii ili kuepuka kuibuka kwa migogoro ya wananchi," alisisitiza Cheliga.

Vilevile alisema kuanzishwa kwa mfumo huo wa kidijitali, utasaidia kudhibiti migogoro ya vyama ambayo mingi inasababishwa na utendaji hafifu wa viongozi wa Vyama vya Ushirika wa Kilimo na Masoko (AMCOS).

Kaimu Meneja wa Chama Kikuu cha Ushirika cha Rift Valley Cooperative Union (RIVACU), Vivian George, akizungumzia mfumo huo alisema utawasaidia kutunza taarifa za wanachama na kuziingiza kwenye mfumo.

Aidha, Katibu wa Chama cha Wasindikaji wa Mafuta ya Alizeti, mkoani Manyara (MASUPA), Julian Kambayta, alisema mfumo huo wa kidijitali utakuwa mzuri na utasaidia serikali kwa kuwa ilikuwa na shida ya kumbukumbu.

Kambayta alisema kupitia mfumo huo, MASUPA wakipata mdau mwenye bidhaa tofauti na ya kwao ni rahisi kuangalia kwenye mfumo na kumuunganisha na wanachama.



Mkuu wa Wilaya ya Babati, mkoani Manyara, Lazaro Twange, akifanya usafi katika soko kuu la Babati jana, ikiwa ni sehemu ya maadhimisho ya miaka 59 ya Mapinduzi ya Zanzibar. **PICHA: JALIWASON JASSON**

# DC awaonya wananchi wanaowabeza walimu

**Na Allan Isack,** ARUMERU

MKUU wa Wilaya ya Arumeru, mkoani Arusha, Richard Ruyango, amewaonya wananchi wanaowabeza walimu, akiwataka kuacha mara moja kwa sababu wanawavunja moyo.

Aliyasema hayo wakati wa kikao chake na walimu wakuu wa shule za msingi, sekondari na waratibu wa elimu kata za Halmashauri ya Arusha.

Ruyango alisisitiza kuwa taifa linawategemea walimu kwa kuwa ndiyo kiwanda cha kuzalisha wataalamu nchini.


Alisema: "Walimu wana dhamana kubwa ya maisha ya watu, kwa kuwa ndiyo kiwanda cha kuzalisha wataalamu duniani, hivyo niwaombe na ninyi walimu kutumia dhamana hiyo kuzalisha wataalamu ambao watakuwa wajenzi wa taifa letu.

"Ninatambua kazi kubwa mliyoifanya walimu mwaka jana, tumepambana kwa umoja wetu kuhakikisha wanafunzi wanafundishwa na kufanya vizuri katika mitihani yao ya ndani na ile ya taifa na tumemaliza mwaka salama, ninawapongeza sana na niwatakie mwaka 2023 kwa pamoja tuongeze bidii zaidi," alisema.

Kutokana na halmashauri hiyo kufanya vizuri katika mitihani ya taifa ya darasa la saba na kidato cha nne mwaka jana, aliagiza walimu kuanza mwaka wa masomo wa 2023 kwa kuongeza bidii na maarifa katika utendaji kazi wao.

Alisema walimu wana dhamana kubwa ya maisha ya watu kwa kuwa ndiyo kiwanda cha kuzalisha wataalamu duniani, hivyo aliwataka kutumia dhamana hiyo kuzalisha wataalamu ambao watakuwa wajenzi wa taifa.

Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Arusha, Seleman Msumi, alisema amepokea maelekezo hayo na atakwenda kuyafanyia kazi kulingana na utaratibu za utumishi wa umma kwa kuwa wanatambua na kuthamini kazi kubwa ya kuwahudumia wananchi inayofanywa na watumishi wa kada zote.





# Maofisa uvuvi wadaiwa kufanya kazi wakiwa wamelewa

**Elizabeth Seleman,**
SENGEREMA

BAADHI ya maofisa wa idara ya uvuvi kutoka wilayani Sengerema mkoani Mwanza wamelalamikiwa kufanya kazi wakiwa wamelewa, hali inayokosesha ufanisi katika makusanyo ya mapato wilayani humo.

Hayo yalibainishwa juzi katika mkutano wa Baraza la Madiwani la kupitisha bajeti ya fedha kwa mwaka 2023/2024 na kusema kuwa wanatakiwa kuboresha vyanzo vya mapato na kuvitambua vyanzo ambavyo vinawaingizia mapato.

Katika kikao hicho ilielezwa kuwa maofisa uvuvi hao wamekuwa wakifanya kazi wakiwa wamelewa na kusababisha kutokusanya mapato kwa kiwango ambacho kinatakiwa.

Diwani wa Kata ya Tabaruka, Sospiter Busumabu, alisema watumishi ambao wanakuwa wanakusanya mapato wanatakiwa kuwa waadilifu ili kuifikia malengo ya bajeti iliyopangwa kukusanywa katika mwaka wa fedha 2023-2024.

"Hatutakiwi kuwafumbia macho watumishi ambao watasababisha kutofikia malengo ambayo wameyaweka kila mmoja anatakiwa kutimiza wajibu wake," alisema Busumabu.

Diwani wa Kata ya Nyampande, George Maria, alisema maofisa uvuvi wanatakiwa kubainisha mialo ambayo bado haijatambulika na kusema mialo 31 ambayo inatambulika inatakiwa kukusanya mapato kama inavyotakiwa

Akitoa taarifa ya ukusanyaji mapato, Ofisa Mipango wa Halmashauri ya Wilaya ya Misungwi, Pastor Mkaruka alisema halmashauri hiyo inatakiwa kukusanya Sh. bilioni 56.1 kwa mwaka wa fedha 2023/2024.

Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Sengerema, Binuru Shekidele, alisema atahakikisha vyanzo vyote vya mapato vinafanya kazi na kukusanya mapato ya halmashauri.



Mjumbe wa Halmashauri Kuu Taifa (NEC) ya CCM na Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Dk. Angelina Mabula, akipokea maua ya ishara ya kumkaribisha katika Ofisi za CCM, mkoani Mwanza juzi, wakati wa sherehe ya kumpokea na kumpongeza kwa ushindi uliompatia nafasi ya NEC. Kushoto kwake ni Mkuu wa Mkoa wa Mwanza, Adam Malima. **PICHA: ROSE JACOB**

# Mahabusu adaiwa kujinyonga kwa kutumia shati rumande

**Na Ndalike Sonda,**
BUDAGA

MKAZI wa Kijiji cha Mwanhela wilayani Busega mkoani Simiyu, Michael Nome, amejinyonga kwa kutumia shati lake wakati akiwa mahabusu katika Kituo cha Polisi Busega mkoani Simiyu.

Akizungumza na waandishi wa habari kuhusu tukio hilo, Kamanda wa Polisi Mkoa wa Simiyu, ACP Blasius Chatanda alisema tukio hilo lilitokea juzi majira ya saa 12:30 asubuhi baada ya kugundulika na kwamba katika chumba hicho cha mahabusu alikuwa peke yake.

Kamanda Chatanda alisema Nome alifikishwa katika Kituo cha Polisi Busega, Januari 8, mwaka huu, majira ya saa 12:00 jioni akishtakiwa na mzazi mwenzake aitwaye Bahati Maduhu kwamba anamfanyia fujo.

Alisema Nome alituhumiwa kumfanyia fujo na kumpiga mwenza wake kutokana na mgogoro wao wa kifamilia wa muda mrefu ambao umekuwa ukifanyiwa suluhisho mara kwa mara bila mafanikio. Kamanda Chatanda alisema mtuhumiwa alifikishwa mahakamani Januari 9, mwaka huu, lakini alirudishwa katika mahabusu ya kituo hicho cha polisi kutokana na hakimu kuwa na majukumu mengine. Alisema uchunguzi wa awali wa tukio hilo umeonyesha kwamba chanzo cha mtuhumiwa huyo kujinyonga ni hasira na kukwepa mkono wa sheria.

## Serikali yaombwa kutoa adhabu kali wanaofanya ukatili

**Na Shaban Njia,** KAHAMA

SERIKALI imeshauriwa kutoa adhabu kali kwa watu watakaopatikana na makosa ya ukatili wa kijinsia ili kutokomeza kuongezeka kwa vitendo hivyo ambavyo vimekuwa vikiongezeka kila siku.

Mwalimu Mkuu wa Shule ya Sekondari ya Lunguya, Maduhu Bujiku, alitoa ushauri huo katika mjadala wa kupinga ukatili wa kijinsia kwa wanawake na watoto uliondaliwa na Mtandao wa Jinsia Tanzania (TGNP).

Mkutano huo ulikuwa na lengo la kuangalia ni jinsi gani ushiriki wa wanaume katika kupinga vitendo vya ukatili wa kijinsia.

Pia aliiomba jamii kuendelea kukemea hali hiyo na kuchukua hatua kwa kutoa taarifa katika vyombo vya sheria kwa hatua zaidi pale wanapoyabaini matukio na siyo kukaa kimya na kumalizana familia.

Alisema watoto wamekuwa wakikosa masomo yao kwa kufanyiwa vitendo hivyo ikiwamo kuozeshwa wakiwa wadogo au kwenda kuchunga mifugo.

Alisema endapo serikali itaweka adhabu kali kwa ambaye atabainika kushiriki katika vitendo hivyo itasaidia kupunguza au kumaliza tatizo hilo.

Bujiku alisema kuna baadhi ya wazazi hudanganya shuleni na kuhamisha watoto wao, huku wakitoa sababu za kuhamia katika mikoa mingine ya Kigoma na Rukwa jambo ambalo siyo kweli na wanapowafuatilia wanakuta wamewaozesha kwa wanaume.

Bujiku alisema baada ya kugundua tabia hiyo wameamua kuweka sheria katika shule hiyo ya kutokuwachukua watoto hadi pale vibali vitakapotoka katika mamlaka husika hali ambayo tatizo kwa sasa limepungua la kuhamisha watoto kinyemela.

Nicolaus Willium alisema ili kuhakikisha watoto wanahitimu masomo yao vema shule zinapaswa kuweka utaratibu wa kuwapiga faini wazazi wenye wanafunzi ambao hawatahudhuria masomo kwa muda wa siku tatu bila taarifa.

Alisema hali hiyo itawalazimu wazazi kuwahimiza watoto kwenda shuleni.

Mwakilishi wa Jeshi la Polisi Mkoa wa Shinyanga, Mbwana ambaye ni Mkuu wa Dawati la Jinsia Halmashauri ya Msalala alisema, matukio ya ukatili yamekuwa yakifanyika katika familia hasa zilizoko vijijini, lakini wahusika hawatoi taarifa katika ofisi za watendaji wa vijiji na kata kwa ajili ya msaada wa kisheria.

Alisema kutoa taarifa katika vyombo vya sheria kunasaidia kudhibiti vitendo vya kikatili na kwamba elimu inahitajika kwa wananchi ili watambue misingi sahihi ya kutoa taarifa, kwamba TGNP kwa kushirikiana na ustawi wa jamii wanapaswa kulichukua suala hilo kwa uzito.




Ukurasa 13

Mikutano itumike kuibua uozo, udhaifu

BUFE
IJUMAA JANUARI 13, 2023
Nipashe
BIASHARA, UCHUMI NA FEDHA



**BOSI MKUU AJIGAMBA: Licha ya mtikisiko wa Covid 19, UTT yang'ara katika miradi yote ya fedha nchini**

Ukurasa 12

MIAKA 59 YA MAPINDUZI SMZ

# Waziri aeleza mageuzi kuhamia uvuvi biashara, jinsi boti 500 zilivyozinduliwa

**Na Christina Mwakangale**

INAPOTIMIA miaka 59 tangu yalipotokea Mapinduzi Matukufu Zanzibar, sasa Serikali ya Mapinduzi Zanzibar (SMZ), kupitia Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Rais Dk. Hussein Ali Mwinyi, sasa imejikita kwenye kuimarisha uchumi, kupitia rasilimali inayokizunguka kisiwa hicho, bahari.

Uchumi wa Bluu utokanao na matumizi ya bahari na rasilimali zake, hapo unaangukia katika mazao ya samaki, mwani mafuta na gesi, ambako ndiko nguvu zinaelekezwa na serikali ya SMZ, kwa kipindi cha muda mfupi, kati na mrefu.

Waziri wa Uchumi na Uvuvi Zanzibar, Suleiman Masoud Makame, katika mazungumzo na kituo cha televisheni ya ITV, anasema SMZ imelenga kuwa na maendeleo endelevu kupitia rasilimali hiyo na ndio dhana na mkakati uliopo, akisema awali utambulisho wa azma hiyo ulikuwa haujaeleweka ipasavyo.

"Wakati ikinadiwa dhana ya uchumi wa buluu, ilikuwa haijaingia katika vichwa vya watu. Kwa kiasi kikubwa, serikali kupitia Rais Dk. Hussein Mwinyi, imekuwa ikizungumzia kwenye mikutano yake mingi, lakini wizara nayo tumeanza.

"Wizara ya Uchumi na Uvuvi katika fedha zile za Uviko-19, nayo ilipata Sh. bilioni 36.5 na tumeanza kuwawezesha wavuvi, wakulima wa mwani, wafugaji samaki, matango bahari na tumetenga utengenezaji wa boti 1,077.



Boti mojawapo ya uvuvi, iliyozinduliwa na Rais mstaafu Dk. Ali Shein mtangulizi wa Dk. Hussein Mwinyi, katika zama za uongozi wake. PICHA:MTANDAO.

"Namna tunaenda kutumia bahari kiuchumi kuendeleza wavuvi, wafugaji wa mazao ya bahari. Ndani ya miaka mitano 2020 hadi 2025, lengo ni kuzalisha ajira 300,000, lakini tutazalishaje ajira ni kupitia sekta ya uchumi," anasema Waziri huyo.

Anafafanua kuwa, mikakati iliyoko ni kuzikabili changamoto ambazo ni matumizi mabaya ya uvuvi baharini, akisema kati yake boti 577 zitakuwa za kisasa za kutunza mazingira, ambazo zitakuwa na kiongoza meli au GPS, pamoja na kitafuta samaki ('fish finder'), ili kuwaongoza wavuvi kubaini palipo na samaki wengi.

**KILIMO BAHARI**

Anasema kwenye kilimo cha mwani, changamoto iliyoko ni soko, mitaji na taaluma na kwamba hivi sasa elimu imetolewa kwao kuwawezesha wakulima hao kupata mkopo nafuu usio na riba, kwa kuwapatia boti 500 kwa jumla ya vikundi 500 vya Unguja na Pemba.

"Kwa mila, silka na desturi za Kizanzibari, utakapotoa mikopo ambayo ina 'interest' ndani yake, wale wengi wangeogopa kuchukua mkopo. Pia, tumeanza ujenzi wa kiwanda kikubwa cha zao la mwani, ambacho kitasarifu zao la mwani," anasema Makame.

Lingine analolizungumzia, ni hadi sasa zao hilo linatengeneza bidhaa nyingi, ikiwamo chakula, mbolea, dawa, kinywaji, pia mapambo na kwamba matarajio yaliyoko sasa, ni bei ya kilo moja ya unga inaongezeka na kufikia kati ya Sh. 5,000 hadi 10,000 kutoka Sh. 700 ya awali. Hata hivyo hakufafanua ni lini.

"Mkulima sasa atakuwa hana wasiwasi na kiwanda hiki kimepandisha thamani ya zao, kwa muda mrefu tumekuwa tukisafirisha bidhaa zetu nje kwa bei ndogo, lakini ikifanyiwa uchakataji hapa inakuza thamani," anasema Makame.

**VIWANDA VYA DAGAA**

Waziri Makame anasema, zao la dagaa kwa miaka kadhaa limekuwa likisafirishwa kwa tani nyingi kwenda nchi jirani, ikiwamo Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo (DRC), ingawa uvunaji wake umekuwa wa kienyeji.

"Ujenzi wa kusarifu samaki umeanza, Zanzibar tunajivunia uwepo wa dagaa ingawa tumekuwa tukiuza 'locally' (kienyeji), kwenye soko la Congo, sasa viwanda hivi vitawezesha dagaa kuwaandalia kabisa, ukifika nyumbani ni kufungua na kuanza kula na ugali wako. Tunaongeza thamani ya mazao ya bahari, kipato na uchumi," anaeleza.

Pia, waziri huyo mwenye dhamana na uvuvi, anaeleza kuwa mwelekeo wa sasa wa uvuvi ni kweye bahari kuu kwa kutumia boti ya kisasa, akisema bahari ambayo ndio chanzo kikuu cha uchumi, itabeba utalii.

**WANUFAIKA MIKOPO**

Makame anawataja watakaonufaika na mikopo hiyo tajwa, ni wavuvi wadogo ambao awali walienda bahari ni kurudi nyumbani wakiwa na kitoweo kidogo kwa ajili ya mboga, pasipo kusalia cha ziada walau cha kuuza kiasi

"Mikopo hii tunaratibu na benki, kwa kuangalia vigezo; kweli ni mvuvi, anaweza kufanya shughuli hii, atarejesha fedha? Boti ambazo tumezichonga za mita saba zipo 300 na zote zina jokofu na kila moja inabeba watu watano.

"Kwa boti hizi kwenye 'field' (eneo la kazi baharini) kunafanyika kazi, wanaweza kwenda watu 5,000 hawa wakirudi na samaki watatoa ajira kwa watu takribani 70,000 za moja kwa moja. Watakuwa wanakatakata samaki wanaoenda kuwauza," anasema Makame.

Anafafanua, lengo la serikali pia ni kuwekeza kwenye uhifadhi wa samaki, mara baada ya kuwavua, kwa kuwapo majokofu makubwa yenye uwezo wa kuhifadhi samaki kilo 600 na barafu 400.

Makame anasema, kuna mchakato wa kutafuta mafuta na gesi yanayochukua muda mrefu na ulianza kutathminiwa tangu zama za miaka ya 1950 na kwamba, zipo nyaraka za majibu zilipokelewa mwaka jana, waliona viashiria vya uwapo rasilimali hiyo.

Anasema, kwa hivi sasa uhamasishaji uko katika watu kujiajiri na kwamba kuna wanawake 80 waliojikita kwenye uchuuzi wa buluu, wamekwishanufaika kwenye sekta hiyo, akitoa wito kwa vijana wengine nao wajiajiri.

FEDHA

BOSI MKUU AJIGAMBA:

# Licha ya mtikisiko wa Covid 19, UTT - AMIS yang’ara katika miradi yote ya fedha nchini

**Na Frank Monyo**

MWANZONI mwa mwaka 2023 Shirika la Fedha Ulimwenguni Duniani (IMF), kupitia Mkurugenzi wake Kristalina Georgieva, alinukuliwa akisema:

“Uchumi wa dunia utakabiliwa na wakati mgumu zaidi kwa mwaka huu, sababu ni mataifa makubwa yakishuhudia shughuli zao zikidhohofika.”

Mkurugenzi huyo anatoa taarifa wakati akihojiwa kituo kimoja, akitamka: “Mwaka huu wa 2023 utakuwa mgumu kuliko mwaka uliopita (2022), kwa sababu mihimili ya uchumi wa kimataifa ambayo ni Marekani, Umoja wa Ulaya (EU) na China, zinashuhudia kwa wakati mmoja kusuasua kwa shughuli zao.”

Wakati kuna kauli hiyo kimataifa mwaka jana, mwezi Oktoba Benki ya Dunia (WB) iliimwagia sifa Tanzania, kwa usimamizi mzuri wa uchumi na utekelezaji wa miradi mbalimbali ya maendeleo inayopata fedha kutoka kwenye taasisi hiyo, ikilinganishwa na nchi nyingine nyingi za Afrika kusuasua.

**NAFASI YA UTT**

Ni pongezi zinazoenda sambamba na mafanikio iliyoyapata Taasisi ya Uwekezaji Fedha ya UTT - AMIS kwa mwaka wa fedha ulioishia Juni 30, 2022, ikifanya vizuri katika mifuko yake yote.

Hapo Mfuko wa Umoja inaoumiliki ulikuwa na thamani na ikiongezeka kutoka shilingi bilioni 612.8 mnamo Juni 30, mwaka juzi, hadi kufikia shilingi bilioni 996.5 mwaka mmoja baadaye, yaani Juni 30, 2022 sawa na asilimia 12.

Mkurugenzi Mtendaji wa UTT - AMIS, Simon Migangala, akitoa taarifa kwa wawekezaji katika Mkutano Mkuu wa Mwaka wa Mifuko ya Uwekezaji ya taasisi hiyo uliofanyika Septemba mwaka jana, ambayo ni Mfuko wa Umoja, Mfuko wa Watoto, Hatifungani, Jikimu, Wekeza Maisha na Mfuko wa Jikimu.

Migangala anasema, ongezeko hilo la kiasi cha Shilingi bilioni 383.7, ni sawa na asilimia 62.6 ikilinganishwa na ongezeko la shilingi bilioni 206.8 sawa na asilimia 50.0 kwa mwaka uliotangulia.



Mkurugenzi Mtendaji wa UTT - AMIS, Simon Migangala, akitoa taarifa ya wawekezaji katika Mkutano Mkuu wa Mwaka wa Mifuko ya Uwekezaji ya taasisi.

Anasema, hayo ni mafanikio katikati ya changamoto mbalimbali ambazo dunia inakabiliana nazo, huku uchumi wa Tanzania ukiendelea kufanya vizuri na kuhimili mtikisiko hasa uliosababishwa na matatizo ya vita nchini Ukraine.

ONGEZEKO LA WAWEKEZAJI

Anasema, mafanikio hayo ni kwa mara ya kwanza tena tangu kuanzishwa UTT AMIS na mifuko yake, kukishuhudiwa ongezeko kubwa kama hilo ndani ya kipindi cha mwaka mmoja.

Ongezeko la ukubwa wa mifuko hiyo, umeenda sambamba na ongezeko la idadi ya wawekezaji 29,832 sawa na asilimia 17.0 waliojiunga katika mifuko kwa mwaka wa fedha ulioishia Juni 30, 2022.

Hapo ni kulinganishwa na wawekezaji 12,798 sawa na asilimia 8.0 waliojiunga katika mwaka wa fedha uliotangulia.

**FAIDA YA MFUKO UMOJA**

“Kama nilivyosema hapo awali, mifuko yote imetoa faida nzuri kwa wawekezaji wake. Faida kwa Mfuko wa Umoja ilikuwa asilimia 12.6. ikilinganishwa na asilimia 8.7 ya kigezo linganifu.

“Katika kipindi cha mwaka wa fedha ulioishia Juni 2022, thamani ya mfuko iliongezeka kutoka shilingi bilioni 258 iliyofikiwa tarehe 30 Juni 2021 hadi dhilingi bilioni 289 tarehe 30 Juni 2022.

“Ongezeko hili la thamani ya mfuko, linatokana na imani ya wawekezaji pamoja na kueleweka kwa elimu inayotolewa, kuhusu faida za mifuko

Migangala anafafanua: “Pamoja na changamoto mbalimbali ambazo dunia inakabiliana nazo, uchumi wa Tanzania uliendelea kufanya vizuri na kuhimili mtikisiko hasa uliosababishwa na matatizo ya vita nchini Ukraine.”

Kwa mujibu wa machapisho ya Ofisi ya Taifa ya Takwimu ya Taifa, Pato la Taifa (GDP) lilikuwa kwa asilimia 5.4 katika kipindi cha robo mwaka kilichoishia tarehe 31 Machi 2022 na asilimia 4.8 kwa robo mwaka iliyoishia tarehe 30 Juni 2022, ikilinganishwa na asilimia 4.9 na aslimia 4.3 za robo ya tatu na ya nne za mwaka wa fedha 2020/2021.

Kwa mujibu wa Ripoti ya Benki Kuu ya robo mwaka iliyoishia tarehe 30 Juni 2022, mfumuko wa bei ulikuwa asilimia 4.1 ikilinganishwa na wastani wa asilimia 9.4 katika nchi za Afrika Mashariki na wastani wa asilimia 10.1 kwa nchi za ukanda wa SADC (Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika)ukiondoa nchi ya Zimbabwe.

**MWENYEKITI UTT**

Mwenyekiti wa Bodi ya UTT AMIS, Casmir Kyuki, anasema matarajio ya mwaka 2022/23 ya utekelezaji mpango mkakati wa UTT AMIS utakaoishia Juni 30, 2024, umekuwa na mafanikio makubwa zaidi ya ilivyotarajiwa.

“Kampuni itaendelea kutekeleza vipaumbele vilivyoainishwa kwenye mpango huo ikiwemo kuboresha mifuko, huduma kwa wawekezaji na kubainisha fursa nyingine za kibiashara kwa manufaa ya wawekezaji, serikali na wadau wengine.

“UTT AMIS itaendelea kuboresha namna ya uendeshaji wa mifuko ili uwe wa kisasa zaidi na kuhakikisha wawekezaji wanapata faida shindani kuendana na hali ya soko,” anasema Kyuki.

**MFUKO WEKEZA MAISHA**

Kuhusu mfuko wa Wekeza Maisha, Kyuki anasema kwa mwaka wa fedha ulioishia Juni 30, 2022 unaendelea kufanya vizuri na faida kwa wawekezaji ilikuwa kubwa, ikilinganishwa na kigezo linganifu au kitaalamu inaitwa ‘performance benchmark.’

Kyuki anafafanua kuwa, faida kwa mwaka huo ilikuwa asilimia 14.1, ikilinganishwa na asilimia 8.7 ya kigezo linganifu cha awali. Hapo anaendelea kufafanua: “Katika kipindi cha mwaka wa fedha ulioishia Juni 2022, thamani ya Mfuko iliongezeka kutoka Shilingi bilioni 1.8 iliyofikiwa tarehe 30 Juni 2021 hadi Shilingi bilioni 4.4 tarehe 30 Juni 2022.”

Anaongeza kuwa, katika mwaka wa fedha ulioishia Juni mwaia jana, inaonyesha kuwa na ongezeko la asilimia 7.5 kutoka Juni 30,2022, 2022 ikilinganishwa na ongezeko la asilimia 4.8 kwa mwaka ulioishia Juni 30, 2021.

**MFUKO HATIFUNGANI**

Kyuki anadems, faida katika Mfuko wa Hatifungani kwa mwaka wa fedha ulioisha Juni 2022, ilikuwa asilimia 14.9, ikilinganishwa na asilimia 15.7 ya mwaka uluioshhia 2021.

Hapo anafafanua kuwa, jumla ya gawio la shilingi 12.0 lililipwa kwa wawekezaji sawa na shilingi 1.0 kwa kila kipande, malipo yaliyolipwa kwa mpango wa kila mwezi.

“Napenda kumshukuru Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan na Serikali kwa ujumla kwa kuweka sera na mazingira bora ya kufanya biashara.

“Pia, kwa kuweza kudhibiti athari zitokanazo na janga la UVIKO-19 na kuyumba kwa mfumo wa shughuli za kibiashara ulimwenguni. Ni tumaini langu kuwa Dunia itaendelea kuimarika na hatimaye kuondokana na athari hizo,” anasema.

**MFUKO WATOTO/ KUJIKIMU**

Hapo Kyuki anasema, faida katika Mfuko wa Watoto kwa mwaka wa fedha ulioisha Juni mwaja jana, ilikuwa asilimia 14.1, ikilinganishwa na asilimia 19.9 mwaka 2021. Anasema kupungua faida ya mwaka huo, kulichangiwa na kushuka viwango vya riba sokoni.

Kwa upande wa Ofisa Mwandamizi wa Masoko na Uhusiano wa UTT AMIS, Rahim Mwanga, anasema faida katika mfuko wa Jikimu kwa mwaka wa fedha ulioisha Juni 2022, ilikuwa ni asilimia 13.6, ikilinganishwa na asilimia 18.8 ya mwaka 2021.

Kwa kipindi cha mwaka mmoja jumla ya gawio lililipwa kwa wawekezaji sawa na shilingi 3.0 kwa kila kipande, katika mpango wa robo mwaka.

**MFUKO WA UKWASI**

Mwanga, anasema faida katika mfuko wa Ukwasi kwa mwaka wa fedha ulioisha Juni 2022 ilikuwa ni asilimia 14.2 ikilinganishwa na asilimia 15.3 ya mwaka 2021. Kupungua kwa faida ya mwaka kulichangiwa na kushuka kwa viwango vya riba sokoni.



Wanafunzi wa shule ya biashara wakisikiliza mada iliyotolewa na Mkurugenzi Mtendaji wa UTT AMIS, Simon Migangala, kuhusu fursa za uwekezaji zinavyochochea mabadiliko ya kiuchumi katika jamii. **PICHA ZOTE: MTANDAO.**

TAFAKURI YA MLALAHOI

## Mikutano itumike kuibua hali ya uozo na udhaifu





**NA JOSEPH KULANGWA**
Simu: +255 713 410008
barua pepe: kulangwasos@gmail.com.

NDEREMO za kisiasa zinaendelea karibu kila kona ya nchi. Watu wana jipanga, wengine wameanza kuvamia majukwaa ya kisiasa kutoa ya moyoni, baada ya kukaa ‘kifungoni’ kwa miaka takriban saba.

Ilitokana na tamko moja tu la mtu mmoja mwenye mamlaka, kwamba haitakiwi mikutano ya hadhara ya vyama vya siasa, kwa sababu baada ya uchaguzi ni wakati wa kujenga nchi.

Tamko hilo likafuatiwa na kamata kamata ya wapinzani waliokaidi na kufanya si tu mikutano ya hadhara, bali hata ya ndani na wakati mwingine maandamano rahisi na mepesi ya kudai haki.

Hata hivyo, watu walitii kwa shuruti na kujifungia ndani huku wakiomba ije siku moja ya kutoka kifungoni na kufanya yaliyofanyika kabla ya kuingia madarakani kwa Rais Dk. John Magufuli.

Hatimaye juzi kati hapa, Rais Samia Suluhu Hassan, baada ya kujadiliana na waansiasa wenzake waandamizi wa vyama vyote, akaona isiwe shida, kwanini watu wasifanye mambo yanayowaweka nchini.

Ikumbukwe kuwa, kuongoza au kusimamia chama kwa baadhi ya watu kulichangia mkono kwenda kinywani kwa namna moja au nyingine, hivyo kusimamisha shughuli zao kwa sababu iliyotolewa ilikuwa kuwaonea.

Hivi sasa, vyama vya siasa hususan vya upinzani vimefunguliwa na vinaweza kufanya shughuli bila ya kuzuizi, lakini kwa masharti ya kutoa taarifa na kukubali kulindwa na polisi.

Kulindwa na polisi hakumaanishi kubanwa na kupangiwa ya kusema, la hasha! Ni kuhakikisha usalama na utulivu kwamba kusitokee mtafaruku au wawanachama wenyewe kwa wenyewe au wa vyama tofauti.

Pia, ruhusa hiyo, si kibali cha kutukanana na kuchafuana baina ya vyama, mambo ambayo yanaweza kuvunja amani na kuondoa maana ya ruhusa hiyo adhimu iliyosubiriwa na wengi.

Tujue pia, kuwa sisi ni binadamu na kila mmoja kaumbwa kivyake kimwili na kiakili na uwezo wa kupambanua jema na baya. Maumbile hayo ndiyo yatakayotuongoza kufanya vizuri katika muktadha huo.

Kukaa miaka saba au minane bila ya kusema kile ambacho ulikiona hakiko sawa, lakini kwa amri ya kuzuia kufanya hivyo, mtu umekuwa nacho kikikubana mwilini na sasa unaambiwa unaweza kukisema ni faraja kuu.

Hapo sasa kuna mawili, ama kusema vizuri usiharibu, au kusema vibaya na kuharibu. Ndiyo sababu hata Rais Samia akahadharisha kuhusu ustaarabu katika mikutano yetu.

Ni dhahiri kusema na kutakuwapo, kama ilivyokuwa awali kabla ya tamko, hivyo inatakiwa ngozi ngumu katika hayo, kwa sababu iwe iwavyo serikali itasemwa sana, kwani kipindi chote hicho haikusemwa kama ilivyokuwa awali.

Kusemwa huko pia kutasaidia mambo mengi kujulikana, yakiwamo ya udhaifu wa baadhi ya viongozi, pia ufisadi katika taasisi za umma; wizi na ubadhirifu kwa baadhi ya watu.

Siyo siri kuwa, kumekuwapo kulindana kwa baadhi ya watu kwenye taasisi za umma, ambako kulifumbiwa macho hasa kutokana na kukosekana majukwaa ya watu kuyasema. Lakini sasa, kwa fursa hii, yataanikwa!

Kukosekana mikutano ya hadhara ya wanasiasa, kulikosababisha baadhi ya viongozi kama kulala vile, huku ikishajihishwa na Bunge kuonekana kama vile ni la chama kimoja na sura ya kukosekana upinzani uliokuwapo awali.

Wananchi jukumu letu litakuwa kusikiliza wanasiasa wetu wanachokisema, huku tukipembua mchele na pumba badala ya kumeza kila kitu kitakachotujaza sumu ya ujinga na pengine kutumia fursa hiyo kuvuruga amani tuliyo nayo.

Jukumu lingine la msingi, ni kuwakatalia wale watakaokuwa wanatujaza ujinga huo, ili tuwaamini kwakuwa tu wana lengo la kuingia Ikulu. Mtanzania wa leo si wa kudanganywa kwa rupia, tuwe makini na wadanganyifu hao.

Kwa kuwa nchi hii ni yetu sote na kwa kuwa RaisSamia ametaka tuwe wamoja zaidi, bila ya kujali itikadi zetu, basi palipo na uozo tuuanike ufanyiwe kazi, kama ambavyo mkuu wa nchi amesema, kwamba akosolewe yeye na serikali yake ili udhaifu ufanyiwe kazi.

Inshallah, hakuna mkubwa kuliko Mama Tanzania, tuilinde kama nchi, tulinde uhuru, amani na mshikamano wetu kwa muktadha mwema wa vizazi vilivyopo na vijavyo. Alamsiki!

# Mzee Butiku ang'aka uzazi usiolea maisha

**Na Christina Mwakangale**

MKURUGENZI wa Taasisi ya Mwalimu Nyerere Mzee Joseph Butiku, amekemea tabia inayokithiri sasa ya wanaume hata waliomo kwenye ndoa, kuzaa watoto ovyo na kuwatelekeza, huku jamii ikiwapa majina mabaya watoto hao kwa kuwaita 'watoto wa mtaani'.

Anashauri ifike hatua, uwepo utaratibu wa kisheria kuwatambua watoto wanaozagaa mitaani na waliotelekezwa na baba zao, huku wakikosa huduma muhimu ikiwamo huduma za lazima na kwamba sheria na haki isidhulumiwe kwa mtoto wa Kitanzania.

"Tunafahamu duniani Katiba inasema 'binadamu wote ni sawa, wana haki sawa.'Mbona watoto mnawaita wa mtaani?" anatamka Mzee, akiendelea: "Kwani mitaa ndio imezaa watoto hawa.Tuache unafiki na ubinafsi, watoto watambuliwe baba, mama zao hata kama ni wangu (Butiku), unafiki wangu usifanye mtoto akose haki, tunajenga taifa la aina gani."

Anasema jamii imejaa umma na hulka za namna tofauti huku wakifahamu kuna upande mwingine watoto wananyimwa haki zao, akitaja madhara ya wanakoelekea ni kuwapo watoto waliopotoka, vikiwamo vikundi vya 'panya road.'



Mkurugenzi wa Taasisi ya Mwalimu Nyerere, Mzee Joseph Butiku. **PICHA: MTANDAO.**

"Utakuta wanaume waliopo kwenye ndoa wanajificha kwenye kivuli cha ndoa, kumbe ana watoto nje kazaa kamtelekeza. Sawa ulikosea, basi lea!

"Mke kwenye ndoa naye anajua mumewe ana mtoto nje, anaogopa kusema tumlee, akihofia jamii kumuona mumewe kazaa nje ya ndoa, ubinafsi huo!" anatamka Butiku.

"Vijana nao ndio imegeuka kama utaratibu, wanazaa watoto wanatelekeza, hawaoi! Jiulize, miaka ijayo kutakuwa na watoto wangapi wa aina hii? Hakuna utaratibu, tabia hii tuiache ni tatizo kubwa kimalezi! Ubaguzi huu haufai, mtoto huyu wa mtaani na wazazi wapo.

"Nani anafurahia umekaa kwenye gari lako, unakuta mtoto anagonga kwenye dirisha la gari, ombaomba, unakuta na mama zao wamekaa pembeni. Kama wazazi hawana, uwepo utaratibu," analalamika.

**WAZIRI GWAJIMA**

Waziri wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum, Dk. Dorothy Gwajima, anachangia mada hiyo akisema kuwa maofisa ustawi wa jamii wanapaswa kufanya utambuzi wa watoto katika maeneo yao, ili kuzuia watu wanaowatumia kwa shughuli zisizofaa.

Dk. Gwajima akiwa jijini Dodoma, anawaambia wanataaluma katika mkutano wao kwamba, wataalam na wadau wa Ustawi wa Jamii, kila mmoja anapaswa kusimamia wajibu wake kuhusu watoto waliopo katika mazingira yasiyokuwa rasmi, ambao wamejiingiza katika kuomba mitaani.

Anawaagiza maofisa hao kuwa na daftari maalum la watoto, ambalo litaainisha changamoto za kila mmoja wao na wale wenye mahitaji maalum wasiokuwa na makazi, wapelekwe kwenye makazi maalum yaliyopo.

Hapo anafafanua adha walizo nazo watoto wa mtaani na namna ya maisha yao yanavyotumika kuwanufaisha wale wanaowatuma.

"Hawa watoto utakuta kwa siku anapata Sh. 10,000 au 15,000, kwa mitatu ni shilingi ngapi?" anahoji Dk. Gwajima, akiweka angalizo: "Unaweza kujiuliza wanaweka kwenye benki gani kama siyo kutumika kama miradi ya watu! "

Waziri Gwajima anasema vipo vituo 30 vya malezi vilivyojengwa na wadau nchini, ambavyo vimekuwa msaada mkubwa kwa jamii na kwamba serikali inaendelea kutafuta fedha ili kujenga vituo vigine zaidi.


---

## CHEMSHABONGO NA -00 41 00-

Na Felix Magezi
felixmagezi@gmail.com

Dondoo: Kulia
1. taarifa
5. hali ya kutokuwepo hatari
6. hali ya mtu kuwa tayari kuifia nchi yake
8. Boflo
9. kata
10.Maksi


Chini:
1. hali ya kutotawaliwa na mtu au nchi nyingine
2. uadua
3. shina la mtama
4. soka
7. fahamu au jua
8. ugonjwa ulioko kichwani



Kamilisha jedwali kwa kujaza maneno yafuatayo:

MWAKA MPYA
MAWAZIRI
AMA
ASKARI
INIKA: ISI
AILA : MTI
AMUA: ITA
PASUKA
ABADANI
WAKILISHA
AMANA
ZARI
AKIA

maoni SMS: 0787 00 97 94



Majibu toleo lililopita

| | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| M | A | L | K | I | A | | D |
| K | | O | | | M | B | U |
| A | S | M | A | R | A | | A |
| L | | E | D | E | N | I | |
| I | | | A | J | A | B | U |
| M | E | M | B | E | | A | |
| A | | B | U | S | A | R | A |
| N | | W | | H | U | A | |
| I | | A | D | A | A | | |

| | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| M | U | N | Y | U | | P | |
| E | | Y | | N | | A | |
| N | Y | A | N | Y | A | S | A |
| Y | | M | | A | D | A | |
| A | L | A | | M | A | D | A |
| | H | | T | A | M | A | A |
| T | A | B | U | | U | | L |
| | S | | M | | | | I |
| K | A | L | E | N | D | A | |



# Kairuki alipongeza JHPIEGO utekelezaji miradi maendeleo

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

WAZIRI wa Nchi, Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), Angellah Kairuki, amelishukuru Shirika la Kimataifa la Jhpiego kwa ushirikiano wanaoutoa kwa serikali kwenye utekelezaji wa miradi ya maendeleo kwenye sekta afya hususani afya ya msingi.

Alitoa shukrani hizo jana alipofanya mazungumzo na Ofisa Mtendaji Mkuu wa Shirika la Jhpiego Duniani, Dk. Lesile Mancuso katika ofisi yake ya jijini Dodoma.

Kairuki alishukuru shirika hilo kwa kutoa usaidizi wa kitaalamu kwenye vituo vya kutolea huduma za afya nchini tangu mwaka 1990 kwenye maeneo ya afya ya uzazi, ukimwi, kifua kikuu, malaria, uimarishaji wa mifumo ya afya ikiwamo utoaji wa vifaa na vifaa tiba.

Mafunzo kwa watumishi wa sekta ya afya kuhusu uzazi salama na upasuaji salama upatikanaji wa taarifa za kimkakati za kuboresha utoaji wa huduma za afya uimarishaji wa utoaji wa huduma za afya mtandao na kusaidia kwenye mapambano dhidi ya corona.

Aidha, alieleza vipaumbele muhimu kuwa ni ujenzi wa vituo vya afya katika maeneo ya kimkakati, ujenzi wa nyumba za mama ngojea kwenye maeneo ambayo vituo vipo mbali na wananchi, upatikanaji wa vifaa tiba kwenye vituo vipya 250 vya kutolea huduma za afya ambavyo vimekamilika.

"Na mafunzo ya watumishi wa sekta ya afya katika utoaji wa huduma bora za afya ikiwamo upasuaji salama kwenye vituo vya kutolea huduma za afya nchini.

"Ninafarijika kwa ujio wako na ni ishara nzuri ya mahusiano mazuri yaliyoko baina ya Jhipiego na Ofisi ya Rais -TAMISEMI na serikali yetu kwa ujumla, naamini yatasaidia kuboresha sekta ya afya ya msingi nchini,"alisema Kairuki.

Naye Mtendaji Mkuu wa Shirika la Jhpiego, Dk. Lesilie Manicuso, alipongeza serikali kwa ushirikiano wanaoupata kwenye utekelezaji wa miradi ya afya nchini na kufurahishwa na vipaumbele vyake kwa kuwa vimewekwa kwenye utekelezaji wa mipango yao ya kuboresha sekta ya afya nchini.

Hata hivyo, aliahidi kuendeleza mahusiano hayo kwa maslahi mapana ya Watanzania.



Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais, Muungano na Mazingira, Selemani Jafo (kulia), akishuhudia Ofisa Mkuu Idara ya Fedha wa Benki ya Exim, Shani Kiswaga (aliyechuchumaa), Meneja Masoko na Mawasiliano wa benki hiyo, Stanley Kafu (wa pili kushoto) na Katibu Mtendaji wa Taasisi ya Habari Development Association, Bernard Mwanawile (kushoto), wakipanda miti kwenye soko la Machinga Complex, jijini Dodoma juzi, ikiwa ni sehemu ya maadhimisho ya Miaka 59 ya Mapinduzi ya Zanzibar sambamba na kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi. Benki hiyo, imefadhili upandaji wa miti 6,000 katika maeneo mbalimbali ya jiji hilo. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Aweso akunwa kasi ujenzi jengo la Wizara ya Maji

**Na Mwandishi Wetu,** DODOMA

WAZIRI wa Maji, Jumaa Aweso, amesema ameridhishwa na maendeleo ya ujenzi wa jengo la ofisi za Wizara ya Maji lililoko katika eneo la Mtumba jijini Dodoma, ambalo limegharimu Sh. bilioni 22.9.

Akiwa katika eneo la ujenzi wa jengo hilo, Aweso aliishukuru serikali kwa kutekeleza ujenzi wa majengo ya ofisi za wizara zote na hususani Ofisi ya Wizara ya Maji litakalokuwa na uwezo wa kuhudumia watu takribani 518.

Alisema ujenzi wa majengo hayo ni muhimu na kwamba yatachangia kuongeza ufanisi kwa watumishi katika utendaji wao wa kazi.

Aidha, alimpongeza mkandarasi anayejenga jengo hilo ambao kwa sasa umefikia asilimia 82.

Kwa upande wake, msimamizi wa ujenzi wa jengo hilo, Mhandisi Mwajuma Waziri, kutoka Wizara ya Maji alisema mradi wa jengo hilo unatarajiwa kukamilika ifikapo Machi mwaka huu na kazi inaenda kutekelezwa usiku na mchana.

"Huu ni mwendelezo wa utaratibu wa Waziri Aweso wa ukaguzi na usimamizi wa miradi mbalimbali inayosimamiwa na kutekelezwa na Wizara ya Maji ili kuona thamani ya fedha na kuhakikisha miradi hiyo inaleta tija kwa Watanzania," alisema.

# Viongozi wa dini watakiwa kutoitwisha mzigo serikali

**Na Peter Mkwavila,** MTERA

MAASKOFU na wachungaji wametakiwa kutokuwa chanzo cha kuitwisha mzigo serikali katika kutatua migogoro na mifarakano ambayo imekuwa ikitokea katika makanisa.

Rai hiyo ilitolewa na Mchungaji wa Kanisa la Pentecostal Holiness Association Mission Tanzania (PHAM T) Mtera Aswile Mwandambo alipokuwa akizungumza na waandishi wa habari kuhusu kuibuka kwa migogoro katika makanisa mengi nchini.

Alisema viongozi wa dini wanatakiwa kuiombea serikali amani na watu wake na siyo kupelekewa kesi za migogoro ya makanisa inayosababishwa na maaskofu na wachungaji.

Alisema pamoja na madhehebu ya dini kufanya kazi na serikali bado kuna maeneo ambayo yanategemea kutatuliwa kwa kumwomba Mungu pale inapohitajika kufanya hivyo.

Pia alisema moja ya kazi ya serikali ni kuangalia ulinzi wa taifa na watu wake, hivyo maaskofu na wachungaji kupitia waumini wao wanatakiwa kushirikiana katika kuhakikisha amani hiyo inadumu ndani ya nchi.

"Serikali siyo kazi yake kutatua migogoro na kesi zinazosababishwa na mifarakano ya viongozi wa makanisa, bali serikali yenyewe inategemea kanisa kama sehemu kubwa ya kukimbiliwa kwa ajili ya kuomba mahitaji mbalimbali kama vile kuombea uchumi, amani na hata magonjwa yanayotishia maisha ya watu.

Alisema viongozi wa dini wanatakiwa kufanya kazi za wito walioitwa wa kuwatumikia watu kiroho, kijamii, kiafya na kielimu na siyo kuwa watu wa kusababisha vurugu na hata kufikia hatua ya kupelekana serikalini.

Alisema ndiyo maana serikali inapokuwa na jambo ambalo ni zito wanawageukia viongozi wa dini ili wafanye dua na sala na hatimaye Mungu kujibu haraka na kama ni magonjwa hutoweka.

Mchungaji huyo aliwataka waumini kufanya kazi kwa bidii ili kujiongezea kipato pamoja na kuliombea Bwawa la Mtera ili samaki wapatikane kwa wingi.

Hivyo aliwataka kuzitumia vizuri mvua zinazoendelea kunyesha, kujikita kwenye kilimo kupata chakula cha kutosha ambacho watajiwekea akiba ya kutosheleza.






Mkuu wa Wilaya ya Morogoro, Wakili Albert Msando (wa tano kushoto), akipokea kompyuta kutoka kwa Mkurugenzi wa Rasilimali Watu wa Kiwanda cha Kusindika Tumbaku cha Alliance One, Blasius Lupenza, katika hafla ya kupokea msaada wa vifaa vya upasuaji wa mifupa kwa ajili ya Hospitali ya Rufani ya Mkoa wa Morogoro na kompyuta kwa Jeshi la Polisi mkoani humo. Wengine ni Mkuu Polisi Wilaya ya Morogoro, SSP Samson Cornel (wa pili kushoto), Msemaji wa kampuni hiyo, John Magoti (kulia) na Daktari wa kampuni, Mossi Makau. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Ofisi ya Waziri Mkuu yatoa msaada waathirika mafuriko

**Na Grace Mwakalinga,**
MBEYA

OFISI ya Waziri Mkuu imetoa msaada wa mahitaji mbalimbali kwa waathirika wa mafuriko yaliyosababishwa na mvua jijini Mbeya.

Mvua hiyo ilinyesha usiku wa Januari 7 mwaka huu na kusababisha madhara ikiwamo uharibifu wa miundombinu ya barabara, madaraja na mali za wananchi.

Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu anayeshughulikia Sera, Bunge na Uratibu, George Simbachawene jana aliambatana na Kamati ya Ulinzi na Usalama ya Mkoa wa Mbeya na Mbunge wa Mbeya Mjini, Dk. Tulia Ackson, kukabidhi misaada ya vitu mbalimbali kuwasaidia waathirika wa mafuriko.

Miongoni mwa misaada iliyotolewa ni tani 50 za mahindi, magodoro 300, mablanketi 1,200, mikeka 550, madumu ya maji 600, sufuria, vikombe, sahani.

Simbachawene aliwaeleza wananchi kuhusu hatua mbalimbali zilizochukuliwa na Serikali ikiwa ni pamoja na kuboresha miundombinu ya Jiji la Mbeya pamoja na kuwahudumia waathirika hao kwa kuwapatia chakula kwa kipindi cha miezi mitatu mfululizo.

"Serikali inatoa pole sana kwa janga hili la mafuriko, tumeona kwenye vyombo vya habari namna mlivyopata madhara ya mali na samani zenu kusombwa na maji, nyumba zenu kubomoka na kukosa makazi, tumekuja kujionea hakika hali ni mbaya, tumewaletea msaada kidogo ambao naamini utawasaidia kusukuma siku wakati serikali ikiendelea na jitihada za kutafuta suluhu ya kudumu juu ya miundombinu maeneo yenu," alisema Simbachawene.

Mkuu wa Mkoa wa Mbeya, Juma Homera, aliwataka wananchi kuendelea kuwa watulivu katika kipindi hiki kigumu wakati serikali ikiendelea na jitihada za kuwahudumia, lakini aliwatahadharisha kuepuka kujenga makazi katika maeneo oevu.

Mbunge wa Mbeya Mjini, Dk. Tulia Ackson, aliishukuru serikali kwa kuchukua hatua za haraka kuwasaidia wananchi wake na zaidi aliomba kulitazama kwa upekee jimbo hilo ambalo limekuwa na tatizo kubwa la miundombinu ya barabara.

# Afikishwa kortini kwa tuhuma za kumnajisi mtoto

**Na Grace Mwakalinga,**
MBEYA

MKAZI wa Kata ya Nzovwe, Halmashauri ya Jiji la Mbeya, Isaya Nswila (36), amefikishwa katika Mahakama ya Hakimu Mkazi Mkoa wa Mbeya kwa tuhuma za kumnajisi mtoto wa miaka 12 (jina limehifadhiwa).

Mwendesha Mashtaka wa Serikali, Wakili Emannuel Bashome, ndiye anayeendesha shauri hilo namba tano ya mwaka huu mbele ya Hakimu Mkuu Mwandamizi, Paul Ntumo.

Akizungumza mahakamani hapo jana, Wakili Bashome alisema mshtakiwa Nswila ambaye ni mlinzi wa kampuni moja mkoani Mbeya alitenda tukio hilo kati ya Januari mosi 2022 hadi Novemba 30 katika eneo la Nzovwe jijini Mbeya.

Alisema kitendo hicho ni kinyume na Kifungu Namba 130 (1) (2) e na Kifungu Namba 131 (1) cha Sheria ya Kanuni ya Adhabu Sura ya 16 iliyofanyiwa marekebisho mwaka 2022.

Hata hivyo baada ya mshtakiwa kusomewa mashtaka hayo na upande wa Jamhuri, alikana kuhusika na madai hayo hivyo upande wa mashtaka unalazimika kuwasilisha ushahidi ili kuthibitisha ikiwa kweli mtoto huyo alibakwa.

Katika kesi hiyo, upande wa Jamhuri uliieleza mahakama kuwa upelelezi wa shauri hilo bado haujakamilika, hivyo uliomba kuahirishwa kwa shtaka hilo hadi wakati mwingine kwa ajili ya kusomwa kwa hoja za awali.

Hakimu Mkuu Mwandamizi katika Mahakama ya Hakimu Mkazi Mbeya, Paul Ntumo, aliahirisha kesi hiyo mpaka Januari 17, 2023 kwa ajili ya uchambuzi wa hoja za awali.

Uchambuzi huo unalengo la kujua namna mshtakiwa alivyotekeleza ubakaji huo kama inavyodaiwa na Jamhuri na baadaye kesi itaanza kusikiliza, hivyo mshtakiwa alirudishwa mahabusu hadi tarehe tajwa.

# Prof. Mkenda: Ma-RC, DC, wapeni motisha walimu

**Na Grace Mwakalinga,**
MBEYA

WAZIRI wa Elimu, Sayansi na Teknolojia, Prof. Adolph Mkenda amewaagiza wakuu wa mikoa na wilaya kushirikiana na viongozi wa elimu kuanzia ngazi ya kata kutoa motisha kwa walimu ili watimize vema majukumu yao.

Alitoa agizo hilo kupitia hotuba ambayo ilisomwa na Mkuu wa Mkoa wa Mbeya, Juma Homera kwenye kikao cha kujadili matatizo ya sekta ya elimu na kuongeza ufaulu kwa wanafunzi mkoani Mbeya.

Alisema wazazi wanapaswa kuhamasishwa kuwathamini walimu kwa vitendo pamoja na kushirikiana vizuri na walimu katika suala la malezi na maendeleo ya taaluma kwa watoto wawapo nyumbani na shuleni.

"Kila kiongozi wa elimu kuanzia ngazi ya kata, wilaya na mkoa ahakikishe anafuatilia ufundishaji wa elimu ya darasani pamoja na kutatua kero za walimu badala ya kukaa maofisi, lakini pia wanafunzi wote wahudhurie shuleni ili kukomesha utoro," alisema Homera.

Aliongeza kuwa kila mwalimu anapaswa kujiwekea malengo yake binafsi katika somo analofundisha na kuhakikisha hakuna mwanafunzi anayeshindwa kupata alama zilizokusudiwa katika somo lake ifikapo mwisho wa mwaka.

Naibu Katibu Mkuu wa Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia, Dk. Charles Msonde, alisema ili kuondokana na vikwazo vya elimu nchini wanapaswa kuangalia namna jamii inavyomuunga mkono mwalimu katika kutimiza majukumu waliyopewa katika malezi ya wanafunzi.

Alisema ikiwa mwalimu atawezeshwa ipasavyo na kuthaminiwa hadhi yake inawezekana kutengeneza taifa la wasomi wenye ujuzi na maarifa ambayo yataisaidia nchi kwenye shughuli mbalimbali za maendeleo.





Kamishna wa Polisi Zanzibar, Hamad Khamis Hamad (kushoto), akizungumza na maofisa, wakaguzi na askari wa chini wa jeshi hilo, jijini Zanzibar jana, kuhusu wajibu wao katika kusimamia mikutano ya hadhara ya kisiasa. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Majaliwa: Mapinduzi Zanzibar yameleta mageuzi kiuchumi

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

WAZIRI Mkuu, Kassim Majaliwa, amesema Mapinduzi ya Zanzibar ya mwaka 1964 yamefungua milango ya mageuzi makubwa ya kiuchumi na uwekezaji katika sekta ya utalii.

Aliyasema hayo jana wakati akifungua Hoteli ya Kitalii ya Kilindini yenye hadhi ya nyota tano iliyoko eneo la Pwani Mchangani Mkoa wa Kaskazini Unguja.

Alisema mapinduzi hayo yamesaidia kubadilisha maisha ya wananchi hasa wanaoishi pembezoni mwa bahari kuwa bora.

Majaliwa alisema serikali zote mbili zinaendelea kufanya juhudi kubwa katika kuitangaza sekta hiyo, huku akiitaja Filamu ya Royal Tour iliyotayarishwa na Rais Dk. Samia Suluhu Hassan moja ya sehemu ya mageuzi ya kuifungua nchi katika utalii.

"Serikali zenu zimejipanga kuleta mageuzi makubwa katika sekta ya utalii kwa ajili ya kuongeza pato la taifa kama juhudi zilizofanywa na Rais Dk. Samia Suluhu Hassan katika uzinduzi wa Filamu ya "Royal Tour" ambayo imeitangza Tanzania kimataifa," alisema.

Alisema Tanzania ina kila sababu ya kuifanyia kazi sekta hiyo kutokana na kuwa na aina mbalimbali ya vivutio vinavyoshawishi wageni kutembelea, hivyo aliwataka watendaji kuongeza nguvu katika kuitangaza nchi katika mataifa mingine ili kufikia lengo hilo la uwekezaji. Alisema serikali inaendelea kushughulikia vikwazo vya kibiashara na uwekezaji ili kuona vikwazo hivyo vinaondoka kwa kuruhusu uingiaji wa bidhaa zote zinazozalishwa kuingizwa katika maeneo yote ya nchi hali itakayotanua fursa za kibiashara.

Aidha, Majaliwa aliwapongeza wananchi wa Zanzibar katika kulinda na kudumisha amani na utulivu ambao ndiyo kwa kiasi kikubwa uliowezesha kufikiwa kwa mafanikio katika sekta ya uwekezaji.Alisema miongoni mwa sifa kubwa za Tanzania ikiwamo Zanzibar ni wananchi wake kudumisha amani na utulivu pamoja na ukarimu ambao ni moja ya sifa ya kuifanya nchi kuwapo kwa ushawishi mkubwa wa uwekezaji pamoja na kutembelewa kwa wageni wengi.

"Miongoni mwa mafanikio makubwa ambayo Zanzibar imeyafikia hivi sasa katika sekta ya uwekezaji na utalii ni kuimarika kwa utulivu wa kisiasa na amani ambayo baadhi ya nchi nyingine imekosekana," alisema.

Majaliwa aliipongeza Mamlaka ya Vitega Uchumi na Uwekezaji (ZIPA) kwa kuweka mazingira mazuri ya uwekezaji ikiwamo sheria nzuri na sera ambazo zimejenga mazingira ya kuvutia wawekezaji na kuondosha urasimu. "Nimefurahishwa na kuwapo kwa sheria nzuri na marekebisho ya mamlaka ya vitega uchumi na uwekezaji ZIPA ambazo kwa kiasi kikubwa zimeondosha urasimu na kujenga mazingira mazuri kwa wawekezji kuwekeza nchini," alisema.

Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Kazi na Uwekezaji, Mudrik Ramadhan Soraga, alisema wamejipanga kuimarisha maeneo huru ya uchumi yalioko Micheweni kwa upande wa Pemba na Fumba kwa Unguja ili kuwavutia wawekezaji zaidi kuwekeza.

Alisema wamejipanga kuyafanya maeneo huru ya uwekezaji huko Fumba kuwa eneo la kituo cha uwekezaji wa miundombinu ya mawasiliano ya mtandao ambapo tayari wawekezaji kutoka nchi za nje wameanza kupiga hodi.

Mkurugenzi Mtendaji Mkuu wa ZIPA, Sharif Ali Sharif, alisema tayari mamlaka hiyo imefanikiwa kusajili zaidi ya miradi ya vitega uchumi 1,225 yenye kugharimu jumla Dola za Marekani milioni 16.4, huku kati ya miradi hiyo 452 sawa na asilimia 37 inatokana na uwekezaji katika hoteli za kitalii.

Aidha, alisema hoteli 38 zimekuwa na hadhi ya nyota tano ambazo zipo katika maeneo mbalimbali ya Mkoa wa Kusini na Kaskazini Unguja zikitoa huduma pamoja na kuajiri wafanyakazi wa maeneo hayo.

Mwekezaji wa hoteli hiyo, Michael Raben alisema amefurahishwa na ushirikiano mkubwa aliyoyapata kupitia taasisi za uwekezaji pamoja na wananchi hatua ambayo imesaidia kufanikisha mradi wake. Aidha, alisema katika mradi wa ujenzi wa Hoteli ya Kilindini kipaumbele cha ajira kimelenga kwa wananchi wa maeneo hayo kwa kuajiri wafanyakazi 62 na wageni wawili.

# 'Wanawake tengenezeni batiki mjikomboe kiuchumi'

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

WAZIRI wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, Riziki Pembe Juma, amewataka wanawake wa Zanzibar kujifunza utengenezaji wa batiki ili kupata kipato na kujikomboa kiuchumi.

Alisema hayo jana katika maadhimisho ya Siku ya Batiki Zanzibar iliyofanyika katika viwanja vya maonesho Maisara Mjini Unguja. Alisema wanawake wanapaswa kupewa mafunzo juu ya utengenezaji wa batiki ili kuwawezesha kujikwamua na kuisaidia serikali katika kuongeza mapato.

Waziri Pembe alisema ni vyema kupewa ujuzi kwa wanawake hao ili kuwaunganisha na kuwa wamoja na kutengeneze batiki za kiwango cha hali ya juu na zilizokuwa na ubora.

Aidha, aliziomba tasisi za serikali na binafsi kuweka oda za batiki wanapokuwa na shughuli zao mbalimbali kwa lengo la kuwaunga mkono wafanyabiashara wadogo na kuletea maendeleo.

Katibu Mkuu Wizara ya Biashara na Maendeleo ya Viwanda, Ali Khamis Juma alisema soko la batiki kwa Zanzibar ni kubwa kwa wafanyabiashara watakaoweza kutengeneza batiki.

Alisema wapo wafanyabiashara wengi wadogo wanajiunga na ujasiriamali lakini wengi wao siyo wajasiriamali bali hufuata mkombo. Hivyo aliwataka wajasiriamali wadogo kujitahidi kutengeneza batiki na kuuza kwa watalii ili kujiingizia kipato.

Mkurugenzi Mkuu wa Moro Batiki Group, Dk. Herriet Mkanga, aliwataka wanawake kujishughulisha na ujasiriamali kwa kujiunga na vikundi ili kujikomboa na umaskini. Alisema lengo lao ni kutoa ajira kwa wanawake na vijana ili kumudu mahitaji yao ya kila siku na kuitangaza Tanzania katika nchi za kimataifa.

# Othman ahimiza utangazaji wa bidhaa kitaifa, kimataifa

**Na Mwandishi Wetu**

MAKAMU wa Kwanza wa Rais wa Zanzibar, Othman Masoud Othman, amezitaka taasisi za mafunzo ya amali (ufundi), watoa huduma, pamoja na wajasiriamali nchini kuzitangaza shughuli wanazofanya ili kufahamika ndani na nje ya nchi.

Aliyasema hayo jana katika Viwanja vya Maisara Mjini Zanzibar, alipotembelea Maonyesho ya Biashara ya Tisa ya Mapinduzi Zanzibar.

Alisema zipo shughuli nyingi nzuri na zenye manufaa makubwa zinazofanywa na wajasiriamali, utaalamu kutoka taasisi za elimu pamoja na shughuli za watoa huduma lakini hazifahamiki ipasavyo kutokana na kutotangazwa vyema.

Alisema kuwapo kwa maonyesho hayo ni fursa muhimu za kutangaza na kuonesha hatua kubwa za utaalamu na uzalishaji wa bidhaa zilizofikiwa kutoka taasisi mbalimbali nchini na kwamba kutangazwa ipasavyo kutasaidia vyema kueleweka na wenye mahitaji kuzitumia. Aidha, alizitaka taasisi za elimu na hasa vyuo vya ufundi na wazalishaji bidhaa za biashara kuzalisha bidhaa zenye kukubalika katika masoko ya ndani na nje, sambamba na kuzalisha wataalamu wanaokubalika na kukidhi matakwa ya soko.

Mkurugenzi wa Idara ya Utafiti wa Mifugo Zanzibar, Talib Ali Suleima, alisema malighafi nyingi zinazotumika kutayarisha na kuzalisha chakula cha mifugo zinatoka nje ya Zanzibar jambo ambalo linaongeza gharama kwa bidhaa hizo.

Ofisa Mwandamizi kutoka Idara ya Utafiti wa Mifugo, Zuhera Karim Zam, alisema asilimia kubwa ya chakula cha mifugo kinatokana na bidhaa za kilimo, huku wakulima wengi wa Zanzibar wakizalisha bidhaa chache na kulazimika kununua nje ya nchi jambo linaloongeza gharama za bidhaa hizo.

Mkurugenzi Mtendaji wa Mamlaka ya Vyuo vya Amali, Dk. Bakari Ali Silima, alisema kwamba mamlaka hiyo inawasiliana na watumiaji wataalamu wa sekta ya utalii ambao ni wamiliki wa hoteli ili kueleza aina na haja ya wataalamu wanaowahitaji.

Alisema kwa mujibu wa wamiliki hao, hoteli nyingi zinahitaji wataalamu wenye ujuzi mchanganyiko katika fani za utaalamu zaidi ya mbili ili kuajirika na kutumika vyema kwenye ajira wanazopewa.




Mkurugenzi Mtendaji wa LG, William Cho akizungumza wakati wa mkutano mkuu wa LG na vyombo vya habari uliofanyika kwenye maonyesho ya Consumer Electronics (CES) 2023 yanayoendelea jijini Las Vegas, Marekani jana. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

## Aliyeuawa madai kuchapwa viboko kuzikwa leo

**Na Cynthia Mwilolezi,** ARUSHA

MKAZI wa Wilaya ya Arumeru, mkoani Arusha, Nelson Mollel (32) aliyefariki dunia juzi, baada ya kuchapwa fimbo 280 kwa sheria za kimila, akituhumiwa kumtusi mama yake mzazi matusi ya nguoni, anatarajiwa kuzikwa leo nyumbani kwao Sanawari.

Akizungumza na Nipashe jana, dada wa marehemu Jackline Mollel, alisema mdogo wake atapumzishwa kwenye makaburi ya nyumbani kwao.

"Hakika inauma sana kwa mazingira ya kifo hiki kilichotokea, marehemu tutampumzisha kwenye nyumba yake ya milele leo hapa hapa nyumbani," alisema.

Wakati familia ikiwa imeamua kumzika Nelson baada ya mvutano, Kamanda wa Polisi Mkoa wa Arusha, Justine Masejo, alisema makachero wa jeshi hilo wanaendelea na msako wa kutafuta wahusika wa tukio hilo, akiwamo baba mdogo wa marehemu anayetuhumiwa kuongoza ukatili huo.

Juzi, Jackline alinukuliwa na Nipashe, akisema mdogo wake alifikwa na mauti, baada ya kuchapwa fimbo 280 badala ya 70 zinazotakiwa kuchapwa kwa mujibu wa mila na desturi za mila ya Kabila la Kimasai.

# Vifaa mradi SGR vilivyohujumiwa vyakutwa vichakani

**Na Idda Mushi,** SIMIYU

JESHI la Polisi Kikosi cha Reli kwa kushirikiana na polisi mikoa ya Simiyu, Shinyanga na Mwanza, limekamata vifaa na mafuta vilivyohujumiwa kwenye mradi wa Reli ya Kisasa (SGR), kipande cha Mwanza.

Baadhi ya vitu hivyo ni mafuta ya dizeli lita 700, pikipiki zaidi ya 20, baiskeli nane, madumu tupu 120 na mipira 22 ya kunyonyea mafuta, vikiwa vimetelekezwa vichakani na wahalifu.

Pia watu 21 wamekamatwa na kufikishwa mahakamani kwa nyakati tofauti mwaka jana, waliokutwa na hatia ya kuhujumu miundombinu ya SGR na kuhukumiwa vifungo.

Kamanda wa Kikosi cha Polisi Reli Tanzania, Kamishna Msaizidi wa Polisi, (ACP) Sebastian Mbutta, alisema uhalifu huo umefanywa katika kipindi cha mwezi mmoja uliopita.

Alisema tukio la hivi karibuni ni la Januari 9, mwaka huu majira ya saa 8:50 mchana katika eneo la Seke kwenye barabara ya ujenzi ya SGR, alikutwa Abel Luekila (22), mkazi wa Ngudu Kwimba, akiwa na lita 180 za dizeli zilizohifadhiwa kwenye madumu tisa, amezipakia kwenye pikipiki isiyokuwa na namba za usajili.

Kwa mujibu wa Mbutta, katika kipindi cha Januari hadi Novemba mwaka 2021, walikamata lita 5,820 za mafuta ya dizeli yenye thamani ya Sh. milioni 18.3.

Alisema kipindi kama hicho mwaka jana walikamata lita 13,922 zenye thamani ya Sh. milioni 43.6.

"Jumla ya mafuta yote kwa hivyo vipindi viwili yana thamani ya Sh. milioni 61.9, hii ni thamani ya kabla ya matukio hayo mengine mapya niliyotaja," alisema Mbutta.

Alisema ni muhimu Watanzania wakalinda mradi huo ambao ni wao kuliko kuhujumu kwa kuwa kwa kufanya hivyo ni kukwamisha jitihada za nchi kwenye maendeleo ya mtu mmoja mmoja na taifa kwa ujumla.

Aliwaasa wenyeviti wa vitongoji, mitaa na viongozi wengine kuanzia ngazi za chini kushirikiana na wananchi ili kila mmoja awe mlinzi wa mwenzake na kutoa ushirikiano wa hali ya juu kuhakikisha muda wote reli hiyo inakuwa salama.

Makamanda wa Polisi mikoa ya Mwanza, SACP Wilbrod Mutafungwa, Shinyanga ACP Janet Magomi na Simiyu ACP Blasius Chatanda, jana waliungana na Kamanda wa Polisi Reli, Mbutta kutembelea kambi kuu ya ujenzi wa kipande cha reli cha Mwanza-Isaka, eneo la Malampaka wilayani Maswa mkoani Simiyu.

Lengo la ziara hiyo ni kufahamu hali ya ulinzi na usalama na kukubaliana hatua zaidi ya kuchukua kukomesha uhalifu.

Kamanda wa Polisi Mkoa wa Mwanza, Mutafungwa aliongoza kikao cha majadiliano na mkandarasi wa Kampuni ya China Civil Engineering Construction Corporation (CCECC), mwajiri Shirika la Reli Tanzania (TRC) na kutangaza operesheni ya pamoja kukomesha uhalifu huo.

"Hatutakuwa na mipaka kwamba huku anasimamia huyu au yule, wahalifu wakae chonjo na nawashauri wakatafute kazi nyingine za kufanya," alionya Mutafungwa.

Alieleza kuridhishwa na taarifa ya mkandarasi na mwajiri kuwa hali ya ulinzi na usalama ni shwari isipokuwa matukio hayo madogo ya udokozi ambayo aliahidi wataendelea kuyatatua kadri mradi utakavyoendelea kujengwa.

Mutafungwa alisema nia ya operesheni hiyo ni kuhakikisha wanaendesha msako mkali kuwakamata watu wote wanaoiba au kupokea mali za wizi kutoka katika mradi huo ikiwamo mafuta na vifaa.

Kamanda wa Polisi mkoani Shinyanga ACP, Janet Magomi alisema operesheni hiyo ni endelevu ili kuwadhibiti wahalifu.

Naye Kamanda wa Polisi mkoani Simiyu, ACP Chatanda alisema kufanya kazi huko kwa pamoja kuliwawezesha siku moja kukamata lori likiwa na vifaa vya wizi na kwamba vikao vyao vitakuwa endelevu.

Ofisa Rasilimali Watu Mwandamizi wa TRC, Cornell Kyai, alisema hali ya usalama inaridhisha.

Mhandisi Wang Chao alisema hivi karibuni wanakusudia kuongeza kambi zaidi na vifaa vingi zaidi vya mradi na kwamba vingine vitaendelea kuwapo porini na kuwaomba polisi waendelee kuimarisha ulinzi.


**UNITED REPUBLIC OF TANZANIA**
**MINISTRY OF LANDS, HOUSING AND HUMAN SETTLEMENT DEVELOPMENT**
**REGISTRATION OF DOCUMENTS ACT, (CAP 117)**

**DEED POLL**



The documents presented for registration on the **30-12-2022** at **1:00PM** herewith the original of the above mentioned documents registration having under folio/s **2018** and serial/s **03/2023** knowledge receipt of the enclosures here to.

**URES:**

**ESTHER HEZRON MWAKALILE**

**SIGNED AND DELIVERED BY SAID ESTHER HEZRON MWAKALILE**
Who is known to me personally
Identified to me by....the letter being known to me personally.
This **30** day of **12 / 2022.**

**BEFOR ME:**

BEFORE ME
Qualification: COMMISSIONER FOR OATHS

DEPONENT

1172226902

**KUPOTEA UMILIKI WA KIWANJA**

**Justina Benedicto** Anatangaza kupotelewa na nyaraka ya umiliki wa kiwanja namba **100 kitalu "FF"** kilichopo **Ngokolo Manispaa ya Shinyanga.**

Kwa yeyote atakaeiona atoe taarifa kituo cha Polisi kilichopo karibu au awasiliane na Justina Benedicto kwa simu namba **0744-999278.**

Taarifa ya Polisi **SHI/SHI/RB/16276/2023.**

Musa J Makungu
AFISA ARDHI
MANISPAA YA SHINYANGA

Nakala; Club ya waandishi wa habari, Shinyanga.

1172226702

**DEED POLL CHANGE OF NAME**
**(UNDER CAP.117.R.E.2002)**

By this deed 1,**RUKIA NASSORO MFAUME** an adult, Moslem and resident of **LIZABONI - SONGEA MUNICIPALITY** , do hereby sworn ,Affirm and state as follows:

1.That , I hereby absolutely renounce and abandon the use of former name of **MBAWALA RUKIA NASSORO** and in place thereof do assume and adopt the name of **RUKIA NASSORO MFAUME.**

2.That,in pursuance of such change of name as aforesaid I do hereby declare that ,I shall at all material times hereinafter in all records ,deed and instruments in writing and in actions , proceedings and transactions and upon all accasion whatsoever use and sign the name of **RUKIA NASSORO MFAUME** as the name in place of the former name of **MBAWALA LUKIA NASORO** renounced as aforesaid .

3.That ,I further authorizes and request all people to designate and address me by such assumed name of **RUKIA NASSORO MFAUME.**

I make this declaration consciously believing the same to be in accordance with the provisions of Oaths and Statutory Act ,1966 .

Signed and addressed by the said **RUKIA NASSORO MFAUME** formally known as **MBAWALA LUKIA NASORO** this **02ND** day of **JANUARY**, 2023.

DEPONENT



BEFORE ME:

COMMISSIONER FOR OATHS.

1172226802

HABARI KIMATAIFA

## Mawaziri Ufaransa, Ujerumani wazuru Ethiopia

**ADDIS ABABA,** ETHIOPIA

MAWAZIRI wa mambo ya kigeni wa Ufaransa na Ujerumani wamefanya ziara nchini Ethiopia kwa lengo la kuunga mkono makubaliano ya amani yaliyotiwa saini mwaka jana.

Ziara ya Waziri Catherine Colonna wa Ufaransa na Annalena Baerbock wa Ujerumani, imeanza siku moja baada ya waasi wa Tigray kutangaza wanaanza kusalimisha silaha zao nzito, ikiwa ni kipengele muhimu cha muafaka wakusitisha mapigano kaskazini mwa Ethiopia.

Wakati wa ziara yao ya siku mbili, mawaziri hao watakutana na Waziri Mkuu Abiy Ahmed na mawaziri wengine pamoja na maofisa wa Umoja wa Afrika na wanaharakati wa haki za binadamu.

Pia viongozi hao watatembelea kituo cha usambazaji cha Shirika la Umoja wa Mataifa la Mpango wa Chakula Duniani.

Duru ya kidiplomasia imesema mawaziri hao wanapeleka ujumbe kutoka kwa Umoja wa Ulaya kuwa uko tayari kushirikiana upya na Ethiopia mradi wa mpango wa usitishwaji mapigano unaheshimiwa. **DW**

## Iran yamuhukumu kifo waziri wa zamani

**TEHRAN,** IRAN

IRAN imemuhukumu kifo aliyekuwa naibu waziri wa ulinzi ambaye ana uraia wa nchi mbili kwa tuhuma za ujasusi kwa Uingereza.

Vyombo vya habari vimesema Alireza Akbari ambaye ana uraia pia wa Uingereza, kifo chake kimechochewa kisiasa na kutaka aachiliwe huru.

Akbari alikuwa mshirika wa karibu wa Ali Shamkhani, ambaye kwa sasa ni katibu wa Baraza Kuu la Usalama la Taifa la Iran na aliwahi kuwa Waziri wa Ulinzi kutoka 1997 hadi 2005, wakati Akbari alipokuwa naibu wake.

"Alikuwa mmoja wa maofisa muhimu zaidi wa Idara ya ujasusi ya Uingereza nchini Iran ambaye alikuwa anaweza kufikia maeneo muhimu na nyeti sana nchini," Wizara ya Ujasusi ya Iran ilisema.

Iliongeza "Akbari alikuwa amewapa taarifa kikamilifu kwa Idara ya huduma ya kijasusi ya adui."

Waziri wa Mambo ya Nje wa Uingereza James Cleverly, alitaka Akbari aachiliwe huru.

"Iran lazima isitishe kunyongwa kwa raia wa Uingereza, Alireza Akbari na kumwachilia mara moja," alisema Cleverly kupitia ukurasa wake wa Twitter.

**BBC**

# Poland, Uingereza kupeleka vifaru Ukraine

**LONDON,** UINGEREZA

NCHI za Poland na Uingereza huenda zikawa za kwanza kuhamisha vifaru vikubwa vya vita hadi Ukraine kwa ajili ya kusaidia vita dhidi ya Russia.

Uamuzi wa mwisho haujafanywa, lakini wakuu wa nchi hizo tayari wanazungumza waziwazi juu ya uwezekano huo.

Rais wa Poland, Andrzej Duda, alisema jana kwamba serikali yake itaipa Ukraine vifaru kadhaa aina ya Leopard 2, lakini suala hili bado linahitaji kuafikiwa na washirika.

Uhamisho wa vifaru vya Leopard 2 vya Poland vinavyoundwa nchini Ujerumani na kutumika na wanajeshi unahitaji ushirikiano na Berlin.

Msemaji wa Waziri Mkuu wa Uingereza, Rishi Sunak, aliwaambia waandishi wa habari kwamba nchi yake itaongeza msaada wake wa kijeshi kwa Kyiv na kuipatia Ukraine silaha mpya zaidi za kisasa ambazo zingeisaidia kushinda vita.

Msemaji huyo pia aliongeza kuwa vifaru hivyo vinaweza kuwasaidia Waukraine kuleta mabadiliko mbele katika uwanja wa vita na kwamba Uingereza ilikuwa inafikiria kutuma mizinga ya Challenger 2 kwa Ukraine.

Uingereza hailazimiki kuratibu usafirishaji kama huo na mtu yeyote, kwani mizinga hii iliundwa na kujengwa nchini Uingereza.

Ingawa masuala kama hayo yanajadiliwa na washirika wa NATO.

Wakati huo huo, Rais wa Russia Vladimir Putin, amemwondoa kamanda mkuu aliyekuwa anaongoza vita nchini Ukraine, miezi mitatu tu baada ya kuteuliwa.

Mkuu wa Majeshi, Jenerali Valery Gerasimov, sasa ataongoza kile ambacho Putin anaita "operesheni maalum ya kijeshi".

Jenerali Gerasimov alichukua nafasi ya Sergei Surovikin, ambaye amesimamia mashambulizi ya hivi karibuni dhidi ya miundombinu ya nishati ya umeme.

Mabadiliko hayo yanakuja huku Warussia wakidai kuwa wanapiga hatua mashariki mwa Ukraine.

Jenerali Gerasimov, ambaye amekuwa kwenye wadhifa huo tangu 2012, ndiye mkuu wa wafanyakazi wakuu wa Russia aliyekaa madarakani muda mrefu zaidi tangu enzi ya Soviet.

Jenerali Surovikin amepewa jina la "Jenerali Armageddon" kutokana na mbinu zake za kikatili katika vita vya awali, ikiwa ni pamoja na operesheni za Russia nchini Syria na mashambulizi makubwa ya mabomu katika mji wa Aleppo.

Muda mfupi baada ya kuteuliwa kuongoza operesheni hiyo mwezi Oktoba, Russia ilianza kampeni yake ya kuharibu miundombinu ya nishati ya Ukraine na kuwaacha mamilioni ya raia wa Ukraine bila umeme au maji ya bomba kwa muda mrefu.

Pia alisimamia kujiondoa kwa Russia kutoka mji wa kusini wa Kherson.

Hatima ya Soledar

Rais wa Ukraine, Volodymyr Zelensky, alisema mapigano bado yanaendelea katika mji muhimu wa mashariki mwa nchi hiyo wa Soledar ambao mamluki wa kundi binafsi la ulinzi kutoka Russia Wagner wamesema wameukamata. Rais Zelensky alisema Russia na washirika wake wanajaribu kueneza propaganda kwa madai ya kuukamata mji huo lakini ukweli ni kwamba mapambano bado yanaendelea.

Pande zote mbili zilisema mapigano ya kuwania udhibiti wa mji huo ni makali na yamechukua muda mrefu huku Russia ikitahadharisha kuhusu madai ya ushindi wa mapema yanayotolewa na kundi la Wagner.

Mji wa Soledar ulioko mkoa wa Donetsk unaofahamika kwa uzalishaji mkubwa wa chumvi, unapatikana kiasi maili tisa kutoka mji mwingine wa Bakhmut ambao vikosi vya Russia vimekuwa vikijaribu pia kuukamata.

**BBC**



Msafara wa malori ya Kamati ya Kimataifa ya Msalaba Mwekundu (ICRC) yakipeleka vifaa vya matibabu Mekelle katika jimbo la Tigray nchini Ethiopia juzi. **PICHA: DW**

# DRC yaishutumu Rwanda kuwatumia wakimbizi kama ngao ya kisiasa

**KINSHASA,** DRC

JAMHURI ya Kidemokrasia ya Congo (DRC) imeilaani Rwanda kwa kauli yake ya kutowapokea wakimbizi wanaokimbia vita katika eneo la mashariki mwa nchi hiyo.

Siku moja baada ya Rais wa Rwanda, Paul Kagame, kutoa kauli tata kuhusu wakimbizi kutoka DRC kuingia Rwanda, Msemaji wa nchi hiyo amekanusha na kutupia lawama vyombo vya habari kwa kutoa habari zisizo sahihi.

Yolande Makolo alisema kuwa vyombo vya habari vimepotosha hotuba ya Kagame.

Msemaji wa serikali ya Congo, Patrick Muyaya, alisema matamshi ya Rais Kagame yanathibitisha kuwa haki za binadamu hazina thamani kwake.

Aliishutumu serikali ya Rwanda kwa kuchafua jumuiya ya kimataifa kwa kutumia wakimbizi kwa madhumuni ya kisiasa.

Alisema ingawa Rais Kagame alijaribu kurejea maoni yake kuhusu suala hilo, tayari amefichua nia yake ya kweli.

Zaidi ya Wakongo 70,000 wamevuka hadi Rwanda, wakikimbia mzozo kati ya serikali na waasi wa M23, ambao jumuiya ya kimataifa inasema inaungwa mkono na Rwanda.

Rwanda inakanusha madai hayo. **BBC**

# MAYANGA KUIBEBA MTIBWA LIGI KUU TANZANIA IKIREJEA

**Na Adam Fungamwango**

BAADA ya kupisha mashindano ya Kombe la Mapinduzi, Ligi Kuu Tanzania Bara inarejea tena leo kwa Mtibwa Sugar kuikaribisha KMC kwenye Uwanja wa Manungu Complex, ulioko Turiani, Morogoro.

**Straika mpya, Vitalis Mayanga aliyesajiliwa kutoka Polisi Tanzania anatarajiwa kukiongoza kikosi cha wenyeji.**

Msemaji wa Mtibwa Sugar, Thobias Kifaru, alisema mechi hiyo inatarajiwa kuwa ngumu kwa sababu wametoka kupoteza michezo mwili mfululizo, wakifungwa mabao 3-1 dhidi ya Ihefu na goli 1-0 dhidi ya Yanga.

Kifaru alisema wamejipanga imara kuhakikisha hawarudii tena makosa ya kupoteza pointi katika mechi hiyo ya nyumbani.

"Tunawaalika KMC, na kama utakumbuka tumepoteza mechi mbili mfululizo zilizopita, hatukubali tena, lakini najua mechi itakuwa ngumu kwa sababu KMC ina wachezaji sita wa kikosi cha kwanza ambao wameshawahi kupitia katika timu yetu kwa nyakati tofauti, hivyo watataka kutuonyesha wao bado wana viwango," alisema Kifaru.

Msemaji huyo pia alithibitisha klabu hiyo kumsajili Mayanga akitokea Polisi Tanzania kwa ajili ya kukiongezea nguvu kikosi chao.

"Mwalimu Salum Mayanga alipendekeza mambo mengi, ikiwamo kusajili mshambuliaji mwenye uzoefu katika soka la Tanzania, na tumefanikiwa kunasa saini ya mchezaji huyo na ninavyozungumza yupo hapa kwa wiki nzima sasa akijiandaa na mechi za ligi, hata hivyo bado leo (jana) tunamalizana na silaha nyingine mbili, nazo tukikamilisha tutazitangaza," alisema Kifaru.

Mtibwa Sugar itashuka dimbani leo ikiwa katika nafasi ya nane baada ya kujikusanyia pointi 24 kwenye mezi 19 walizocheza huku KMC yenye pointi 22 ipo nafasi ya tisa.

Ligi hiyo itaendelea tena kesho kwa Geita Gold kuwakaribisha Dodoma Jiji FC wakati Polisi Tanzania itawafuata Namungo kwenye Uwanja wa Majaliwa uliopo Ruangwa mkoani, Lindi.

# Ni Singida Big Stars, Mlandege

**Na Saada Akida,** ZANZIBAR

SINGIDA Big Stars inafikiria kusaka ushindi na kutwaa ubingwa wa mashindano ya Kombe la Mapinduzi wakati Mlandege FC imejipanga kulibakisha kombe hilo katika fainali ya michuano hiyo itakayofanyika leo kwenye Uwanja wa Amaan.

Kocha Mkuu wa Singida Big Stars, Hans Pluijm, aliliambia gazeti hili jana anatambua mchezo huo utakuwa mgumu lakini wapo tayari kwa mapambano.

Pluijm alisema maandalizi kuelekea mechi hiyo ya fainali yako tofauti na walivyokuwa wakijiandaa na mechi zilizopita ambapo leo watacheza kwa tahadhari kubwa.

"Hii ni fainali maandalizi yake tofauti ya mechi zilizopita, tumejiandaa kushinda na tunaingia na mbinu tofauti kwa ajili ya kuhitaji kuondoka na kombe. Tunaingia kwa tahadhari kubwa na kuwaheshimu wapinzani wetu," alisema Pluijm.

Kocha huyo alisema walishinda mabao 4-1 dhidi ya Azam FC, ushindi huo wanaubeba kama changamoto kwa wachezaji wao ili kupata matokeo ya mazuri na hatimaye kutwaa ubingwa huo.

Kocha Mkuu wa Mlandege, Abdallah Mohammed 'Bares', alisema mechi itakuwa ngumu kulingana na ubora wa timu zote mbili lakini wanahitaji kuvua joho la unyonge kwa timu za Zanzibar kwa kubeba taji hilo.

Bares alisema anaiheshimu Singida Big Stars, anajua ni timu nzuri na yenye ushindani, tayari wamefanya maandalizi mazuri na wachezaji wako fiti kwa ajili ya fainali hiyo.



Winga wa Fountain Gate Princess, Winifrida Gerald (kulia), akifunga bao la kwanza katika mechi ya Ligi Kuu ya Wanawake Tanzania dhidi ya Alliance Girls iliyofanyika kwenye Uwanja wa Jamhuri jijini Dodoma juzi. Fountain Gate Princess ilishinda mabao 4-0. **PICHA: MTANDAO**

# Polisi TZ kushusha mastraika watatu

**Na Adam Fungamwango**

IKIWA mkiani katika msimamo wa Ligi Kuu Bara, Polisi Tanzania imesajili mastraika wapya watatu kwa ajili ya kuongeza nguvu katika kikosi chake na kujinusuru na janga la kushuka daraja msimu huu.

Makamu Mwenyekiti wa Polisi Tanzania, Robert Munisi, alisema baada ya kumsajili Kelvin Sabato, wameinasa saini ya Ibrahim Hilika na wako katika hatua za mwisho za kukamilisha mazungumzo ya kumleta nchini straika mwingine kutoka Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo (DRC).

Munisi alisema nyota hao wapya wamesajiliwa ili kurejesha makali na heshima ya Polisi Tanzania ambayo kesho itawavaa wenyeji Namungo FC kwenye Uwanja wa Majaliwa ulioko Ruangwa, mkoani Lindi.

"Katika dirisha hili dogo tumemsajili Sabato ambaye kwenye mechi mbili tu amefunga mabao mawili, halafu kwa sasa tumemsajili Hilika, tutakamilisha usajili wa straika mmoja kutoka DRC na ukumbuke tumeshawasajili Ramadhani Chombo 'Redondo' na Mohamed Banka hii yote ni mikakati," alisema Munisi.

Kuhusu kuachana na Vitalis Mayanga ambaye ametimkia Mtibwa Sugar alisema klabu yao siku zote haing'ang'anii mchezaji ambaye anataka kuondoka klabuni hapo.

# First Lady riadha yavutia mikoa 23

**Na Shufaa Lyimo**

MIKOA 23 imethibitisha kushiriki mashindano ya riadha ya Wanawake maarufu First Lady yatakayofanyika Januari 21 na 22, mwaka huu kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa, Dar es Salaam imefahamika.

Akizungumza na gazeti hili jijini jana, Msemaji wa Chama cha Riadha Tanzania (RT), Uliza John, alisema mashindano hayo yatashirikisha mikoa ya Tanzania Bara pamoja na Visiwani Zanzibar.

Uliza aliitaja baadhi ya mikoa ambayo imethibitisha kushiriki ni Mwanza, Iringa, Mbeya, Dodoma, Arusha na wenyeji wa mashindano Dar es Salaam.



"Maandalizi kuelekea katika mashindano hayo yanaendelea vizuri, tunashukuru mwaka huu mikoa mingi imethibitisha kushiriki, hii inaonyesha jinsi mchezo huu unavyozidi kushika kasi," alisema kiongozi huyo.

Aliongeza kila mkoa utawakilishwa na wanariadha sita na kuwaomba wanawake wajitokeze kwa wingi siku hiyo ili kuona vipaji vitakavyokuwa vinaonyeshwa na wanawake wenzao.

## ZISIKUPITE

### KYLE ANUKIA UNITED

MANCHESTER United na Chelsea inafikiria kumnunua beki wa kulia wa Southampton na Timu ya Taifa ya England, Kyle Walker-Peters, mwenye umri wa miaka 25. (***Talksport***)

### MENDY ATAJWA WEST HAM

WEST Ham imefanya mazungumzo na Klabu ya Amiens ya Ufaransa kwa ajili ya kumsajili beki wa kati wa kimataifa wa Timu ya Taifa ya Senegal, Formose Mendy, mwenye umri wa miaka 22. (***The Athletic***)

### MARSEILLE YAIGOMEA VILLA

OMBI la Aston Villa la kumnunua kiungo wa Marseille, Matteo Guendouzi mwenye umri wa miaka 23 limekataliwa. Mchezaji huyo wa kimataifa wa Ufaransa alicheza chini ya kocha, Unai Emery, akiwa Arsenal. (***Mirror***)

### LEEDS YAMFUATA RUTTER

KLABU ya Leeds United imepiga hatua katika mpango wa kumnunua mchezaji wa kimataifa wa Ufaransa chini ya umri wa miaka 21 wa Hoffenheim, Georginio Rutter mwenye miaka 20. (***The Athletic***)

### SPURS YAMCHUNIA MOURA

KLABU ya Tottenham Hotspur imeamua kutofanyia kazi kipengele katika mkataba wa mshambuliaji wa Brazil, Lucas Moura mwenye umri wa miaka 30, kuongeza muda wake wa kusalia zaidi msimu huu. (***Telegraph***)

### LEMINA ATAKIWA WOLVES

KLABU ya Wolves imeongeza mazungumzo kuhusu mkataba wa pauni milioni 10 ili kumrejesha kiungo wa kati wa zamani wa Southampton na Fulham, Mario Lemina mwenye umri wa miaka 29. (***Sun***)

### FELIPE AINGIA SOKONI

WOLVES pia wanataka kumsajili beki wa kati wa Timu ya Taifa ya Brazil, Felipe, mwenye umri wa miaka 33 kutoka Atletico Madrid. (***Reuters***)

### SOYUNCE ATAJWA ATLETICO

KLABU ya Atletico Madrid inaweza kumnunua mchezaji wa Leicester na Uturuki, Caglar Soyuncu, mwenye umri wa miaka 26, kama mbadala wa Felipe. (***Matteo Morretto, via Twitter***)


### WEST YAMBANIA ANTONIO

KLABU ya West Ham inazuia uwezekano wowote wa kununuliwa kwa mshambuliaji wa Jamaica, Michail Antonio, mwenye umri wa miaka 32 ambaye anavutiwa na Wolves. (***Express & Star***)

### PELLISTRI ANUKIA WATFORD

KLABU ya Watford inataka kumsajili winga wa kimataifa wa Uruguay, Facundo Pellistri, mwenye umri wa miaka 21 kutoka Manchester United. (***Telegraph***)

### AUBAMEYANG KUREJEA BARCA



MSHAMBULIAJI wa Gabon, Pierre-Emerick Aubameyang mwenye umri wa miaka 33 anataka kuondoka Chelsea na kurejea klabu yake ya zamani ya Barcelona. (***AS***)

# DONDOO ZA SOKA MAGAZETI YA ULAYA



# GUARDIOLA APANGA KUIMALIZA UNITED

## ●●● Asema bado anaendelea 'kuisoma' ili kujihakikishia ushindi katika mechi yao...

**MANCHESTER,** England

PEP Guardiola ana mipango ya kimbinu 'ya ajabu' inayozunguka kichwani mwake kabla ya mechi ya Jumamosi dhidi ya Manchester United.

Manchester City wanaweza kuwa nyuma kwa pointi mbili dhidi ya vinara wa Ligi Kuu England maarufu EPL, Arsenal endapo watapata ushindi kwenye Uwanja wa Old Trafford, ambapo Guardiola ameshinda mara sita katika mechi tisa za nyuma.

Kocha huyo wa City alifanya kazi na viungo wawili huku mmoja wakati wa ushindi mkubwa wa Kombe la Carabao dhidi ya United miaka mitatu iliyopita, ambapo Kevin De Bruyne alidai alitumia dakika 15 pekee kumaliza mchezo.

**Guardiola hachukii kubadili mambo, huku Joao Cancelo, akianza kama winga wa kulia wakati wa mechi za ugenini huko Liverpool na Chelsea msimu huu na anaweza kuandaa mshangao mwingine kwenye mkono wake.**

"Lakini bado sikutazama mechi zao za mwisho. Lazima nione jinsi wanavyocheza nyumbani na ikiwa watabadilisha kitu. Bado inabidi niikague. Ndiyo maana sina safu ya wazi dhidi ya United."

"Inategemea kama anaweza kupigana na Rodri - klabu kubwa zinapaswa kuwa na hii," aliongeza.

"Lazima apambane na Rodri kwa manufaa yetu sote. Rodri hawezi kuteleza kwa kuhisi ana mtu wa karibu naye.

"Kwa pambano hasa, Kalvin anaelewa wakati mpira unakuja na ana nguvu hewani. Ana ubora wa kuvunja mistari, Anatakiwa kuboresha upokeaji wa mpira kutoka kwa mabeki wetu wa kati na hili ni suala la muda.

"Ni mchezaji wa timu ya taifa. Alicheza kwa kushangaza kwenye Euro. Ana mawazo, uthabiti, mapigano - sifa nyingi ambazo zilimaanisha angeweza kutulia nasi na nina hakika itatokea.'

SCAN HAPA KUPAKUA APP YETU!
SUPA JACKPOT KWA 1000/- 1,065,5
MECHI KALI
NAPOLI
VERSUS
JUVENTUS
1 | 1.92
X | 3.37
2 | 3.82
KUWEKA PESA:
- PIGA *150*87#, CHAGUA 4
- WEKA PESA.
tigo pesa vodacom m-pesa halopesa airtel money
SEND
SportPesa
SPORTPESA.CO.TZ
PIGA *150*87#
GBT:0249 HUDUMA KWA WATEJA MASAA 24, PIGA: 0764115588, 0677115588 0685115588
18+
@TZSportPesa @SportPesaTZ @tzsportpesa



# COURTOIS: RONALDO AMEIKUZA LIGI YA SOKA SAUDI ARABIA

**RIYADH,** Saudi Arabia

GOLIKIPA namba moja wa Timu ya Taifa ya Ubelgiji na Real Madrid, Thibaut Courtois, amesema anaamini Cristiano Ronaldo ameipa thamani Ligi ya Saudia Arabia.

Ronaldo amejiunga na klabu ya Al Nassr ya Saudia Arabia wiki kadhaa zilizopita na kufanikiwa kuwa mchezaji anayelipwa ghali zaidi duniani.

Baada ya kujiunga na Al Nassr alifanikiwa kuongeza ushawishi na umaarufu wa timu hiyo.


Courtois amezungumza na wanahabari akiwa Saudia ambapo klabu yake ya Real Madrid inacheza michuano ya Kombe la Hispania la Super nchini humo.

"Usajili wa Ronaldo unaonyesha kwa kiasi gani nchi hii inataka kukua kimichezo, Ronaldo kuwa hapa ni uamuzi wake lakini inaonyesha Saudia inataka kuimarika," alisema.

Courtois anaamini ujio wa Ronaldo kwenye ligi hiyo utaimarisha michezo nchini humo, lakini pia amekwenda kuikuza ligi ya nchi hiyo kutokana na nguvu ya ushawishi ambayo amekua nayo.

Kocha Ancelotti naye alizungumza kuhusu Ronaldo huku akisema "Cristiano amekua mchezaji mzuri sana, tunamtakia kila la heri. Yeye ni gwiji wa klabu hii kama Gareth Bale ambaye amestaafu, watakua kwenye mioyo ya wana Madrid milele."

# Ramsey atakiwa kubaki Wales



**LONDON,** England

KOCHA wa Timu ya Taifa ya Wales, Rob Page, amesema anatarajia kiungo wa timu hiyo, Aaron Ramsey, atabakia kwenye kikosi hicho baada ya Gareth Bale kutangaza kustaafu.

Bale ametangaza kustaafu kucheza soka rasmi majuzi akiwa na umri wa miaka 33.

Nyota huyo ameamua kuachana na mpira kwa ujumla kuanzia ngazi ya klabu mpaka timu ya taifa.

Kocha huyo anaamini Ramsey atasalia ndani ya timu hiyo ili kujiandaa na michuano ya kufuzu Euro 2024 itakayoanza Machi, mwaka huu.

Kocha huyo amesema anaamini Ramsey mwenye umri wa miaka 32 ana vitu vingi bado vya kujitolea kwa Wales.

Lakini akisisitiza kiungo huyo ni mchezaji mzuri na anaweza bado kujitoa kwa nchi yake.

505,647/-

# WASHIRIKI WA KILI MARATHON WATAKIWA KUJISAJILI MAPEMA




Pamela Kikuli

**Na Mwandishi Wetu**

WADHAMINI wakuu wa mbio za kimataifa za Kilimanjaro Premium Lager 2023 wametoa wito kwa washiriki wajisajili mapema kwa sababu muda uliobakia ni mchache kabla ya mbio hizo maarufu ndani na nje ya nchi zitakazofanyika Februari 26, mwaka huu Moshi mkoani Kilimanjaro.

Meneja wa bia ya Kilimanjaro, Pamela Kikuli, alitoa rai hiyo wakati akizungumzia maandalizi ya mbio hizo za mwaka huu.

"Tunatoa wito kwa washiriki wajisajili kupitia Tigopesa kwa kubonyeza *150*01# na kufuata maelekezo au kwa kupitia www.kilimanjaro-marathon.com kwani usajili bado unaendelea lakini utafungwa wakati wowote nafasi zikijaa hata kabla ya tarehe ya mwisho Februari 6, 2023," alisema na kuongeza kujisajili mapema kutawasaidia waandaaji kufanya maandalizi ya mambo muhimu mapema kama maji, ulinzi barabarani na huduma ya kwanza.

Kikuli alisema wamejiandaa na kampeni maalumu inayojulikana kama 'tatu zetu kwa gwara yako' ambapo mteja anaweza kununua bia tatu za Kilimanjaro zenye ujazo wa mililita 375 kwa Sh. 5,000.

Kilimanjaro Premium Lager imekuwa mdhamini wa mbio hizi tangu kuanzishwa kwake mwaka 2003 huku wadhamini wengine ni Tigo - (kilomita 21), Grand Malt (kilomita tano), TPC Sugar, Simba Cement, Maji ya Kilimanjaro, Total Energies wasambazaji rasmi ni GardaWorld Security, Hoteli ya Keys, Kibo Palace na CMC Automobiles.

Wakati huo huo, waandaaji wa mbio hizi wametangaza kufuatia maelekezo ya Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Kassim Majaliwa, sasa mbio hizo zitajulikana kama Kilimanjaro Premium Lager International Marathon.

Waandaaji hao walisema hatua hii itasaidia kuongeza washiriki hasa kutoka nje ya nchi na pia kuchangia katika shughuli za utalii kama vile upandaji wa Mlima Kilimanjaro, kutembelea mbuga za wanyama kama Serengeti na Ngorongoro na Visiwa vya Zanzibar, kutembelea mbuga za wanyama kama Serengeti na Ngorongoro na Visiwa vya Zanzibar.

Kwa sasa mbio hizo hushirikisha wanariadha kutoka zaidi ya nchi 55 duniani.

Kwa mujibu wa taarifa ya waandaaji hao, mbio hizo zimekidhi viwango vyote vya mbio za kimataifa ikiwamo kuzingatia viwango vilivyowekwa na Chama cha Riadha cha Dunia pamoja na wenyeji Chama cha Riadha Tanzania (RT).

## Kambi ya Simba Dubai imenoga

INATOKA UK. 24

kuwatia nguvu ili kuendelea kuipambania Simba.

"Ninaamini mkijituma na kupambana, ubingwa wa msimu huu utarejea, lakini ninamatumaini uwezo wa kufika mbali mnao," Talib alisema.

Ikirejea nchini, Simba itawakaribisha Mbeya City katika mechi ya Ligi Kuu Tanzania Bara itakayochezwa Januari 18, mwaka huu kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa, Dar es Salaam.

## Yanga, Ihefu na usiku wa kisasi

INATOKA UK. 24

tibua sherehe ya kufikisha mechi 50 bila kufungwa.

Yanga ilifungwa mechi hiyo ikiwa haijapoteza mechi 49, lakini shughuli iliharibika kwa kupoteza dhidi ya timu hiyo ambayo wakati huo ilikuwa inaburuza mkia katika msimamo wa ligi.

"Tumejiandaa kikamilifu, hatutaki kupindisha maneno, tuko kwenye maandalizi ya 'usiku wa kisasi', hatutaki kupindisha kona kona, Ihefu tuna deni nao, wajiandae vizuri, hakuna sehemu ambayo tutafanya mzaha. Sisi tuliwapongeza, lakini maneno yao, karaha zao, mashabiki wao wakawa wengi wakatupa huzuni na hasira," Kamwe aliongeza.

Naye Kaimu Kocha Mkuu wa Ihefu, Zuberi Katwila, alisema kwa sasa wapo kambini wakijiandaa kikamilifu kuelekea mechi hiyo ambayo anafahamu itakuwa ngumu, lakini ikiwa na pointi tatu kama nyingine wanazocheza.

Alisema kuwa mambo yakienda vyema basi anaweza kuchezesha baadhi ya wachezaji wapya ambao wamesajiliwa katika kipindi hiki cha dirisha dogo.

## SUPA JACKPOT MECHI WIKI HII

### BASHIRI KWA USAHIHI MECHI ZOTE

| TAREHE | MUDA | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 01. 14/01/23 | 18:00 | Nottingham Forest vs Leicester City | 2.80 | 3.30 | 2.46 |
| 02. 14/01/23 | 18:00 | Wolverhampton Wanderers vs West Ham United | 2.65 | 3.20 | 2.65 |
| 03. 14/01/23 | 18:00 | Luton Town vs West Bromwich Albion | 2.95 | 3.20 | 2.40 |
| 04. 14/01/23 | 18:00 | Preston North End vs Norwich City | 2.95 | 3.25 | 2.38 |
| 05. 14/01/23 | 18:00 | Reading FC vs Queens Park Rangers | 2.46 | 3.25 | 2.80 |
| 06. 14/01/23 | 18:00 | Sunderland AFC vs Swansea City | 2.49 | 3.25 | 2.75 |
| 07. 14/01/23 | 18:00 | DR Congo vs Uganda | 2.39 | 2.75 | 3.45 |
| 08. 14/01/23 | 18:15 | Girona FC vs Sevilla FC | 2.40 | 3.25 | 2.90 |
| 09. 14/01/23 | 20:15 | KAS Eupen vs St. Truidense VV | 2.80 | 3.35 | 2.42 |
| 10. 14/01/23 | 20:45 | FC Volendam vs RKC Waalwijk | 2.65 | 3.50 | 2.46 |
| 11. 14/01/23 | 21:00 | Ivory Coast vs Senegal | 2.85 | 2.95 | 2.65 |
| 12. 14/01/23 | 23:00 | Real Sociedad San Sebastian vs Athletic Bilbao | 2.50 | 3.15 | 2.80 |
| 13. 15/01/23 | 16:00 | Getafe CF vs Espanyol Barcelona | 2.50 | 2.95 | 2.95 |
| 14. 15/01/23 | 16:30 | Go Ahead Eagles vs FC Utrecht | 2.80 | 3.50 | 2.35 |
| 15. 15/01/23 | 17:00 | Angers SCO vs Clermont Foot 63 | 2.42 | 3.40 | 2.75 |
| 16. 15/01/23 | 17:00 | Montpellier HSC vs FC Nantes | 2.45 | 3.40 | 2.70 |
| 17. 15/01/23 | 17:00 | Stade Reims vs OGC Nice | 2.55 | 3.20 | 2.75 |

## MECHI ZA USHINDI

"1" NI TIMU YA NYUMBANI KUSHINDA "X" NI TIMU KUTOKA SARE "2" NI TIMU YA UGENINI KUSHINDA.

### IJUMAA - 13/01/2023

| MUDA | GAME ID | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 14:00 | 1281 | Mohammedan SC vs Aizawl FC | 1.80 | 3.51 | 3.85 |
| 15:45 | 5046 | Aswan vs Haras EL Hodood | 1.99 | 2.99 | 4.19 |
| 16:00 | 1684 | Ahi Nazareth vs Nazareth Ilit | 1.99 | 3.40 | 3.65 |
| 16:00 | 2082 | El Fahem vs Maccabi Jaffa | 2.05 | 3.36 | 3.51 |
| 16:00 | 2836 | Ironi Hasharon vs Ironi Tiberias | 2.85 | 3.20 | 2.44 |
| 16:00 | 2883 | Hapoel Afula vs Hapoel Kfar Saba | 2.28 | 3.29 | 3.04 |
| 16:00 | 2926 | Hapoel Petah Tikva vs Bnei Yehuda | 1.92 | 3.55 | 3.75 |
| 16:00 | 3885 | Hapoel Rishon Lezion vs Maccabi Petach Tikva | 2.95 | 3.40 | 2.29 |
| 16:00 | 4166 | Hapoel Ramat Gan vs AS Ashdod | 2.18 | 3.40 | 3.15 |
| 16:00 | 5233 | SC Kfar Qasem vs Hapoel Acre | 2.51 | 3.06 | 2.91 |
| 17:00 | 2424 | Kayserispor vs Sivasspor | 2.28 | 3.38 | 2.94 |
| 18:00 | 1407 | Qatar vs United Arab Emirates | 2.05 | 2.96 | 3.64 |
| 18:00 | 2958 | Bahrain vs Kuwait | 2.01 | 3.02 | 3.70 |
| 18:00 | 4719 | Farco FC vs Ceramica Cleopatra | 4.00 | 2.95 | 2.06 |
| 18:00 | 5324 | Al Khaleej Club vs Al Wehda | 3.35 | 3.15 | 2.21 |
| 20:00 | 1179 | Ismaily SC vs Arab Contractors | 2.79 | 2.74 | 2.84 |
| 20:00 | 4464 | Galatasaray vs Hatayspor | 1.28 | 5.57 | 8.56 |
| 20:00 | 4691 | Denizlispor vs Eyupspor | 5.06 | 3.84 | 1.56 |
| 20:30 | 4817 | Amazulu vs Kaizer Chiefs | 2.80 | 3.00 | 2.65 |
| 21:00 | 3125 | Zwickau vs VfB Oldenburg | 2.03 | 3.41 | 3.41 |
| 21:00 | 4641 | Algeria vs Libya | 1.50 | 3.94 | 6.78 |
| 21:00 | 5968 | Moreirense vs Mafra | 1.78 | 3.54 | 4.14 |
| 21:30 | 1706 | Sedan vs Saint Brieuc | 2.02 | 3.20 | 3.60 |
| 21:30 | 2871 | Le Mans vs Villefranche Sur Saone | 2.04 | 3.31 | 3.41 |
| 21:30 | 3699 | Avranches vs FC Versailles 78 | 3.95 | 3.31 | 1.89 |
| 21:30 | 4303 | Red Star vs Chateauroux | 1.98 | 3.26 | 3.65 |
| 21:30 | 4426 | Orleans vs Dunkerque | 2.67 | 3.11 | 2.57 |
| 21:30 | 4468 | Paris 13 Atletico vs Cholet | 2.45 | 3.11 | 2.81 |
| 21:30 | 4644 | Le Puy vs Nancy | 3.21 | 3.01 | 2.27 |
| 22:00 | 2057 | De Graafschap vs Jong Ajax | 1.74 | 3.89 | 3.94 |
| 22:00 | 3566 | Roda Kerkrade vs FC Oss | 1.41 | 4.45 | 6.53 |
| 22:00 | 4236 | FC Martigues vs Bastia Borgo | 1.40 | 4.53 | 6.70 |
| 22:00 | 4803 | Telstar vs Jong AZ Alkmaar | 2.04 | 3.39 | 3.34 |
| 22:00 | 4879 | ADO Den Haag vs Maastricht | 1.69 | 3.96 | 4.15 |
| 22:00 | 5138 | Helmond Sport vs NAC Breda | 2.67 | 3.26 | 2.47 |
| 22:45 | 1198 | Dijon vs Valenciennes | 2.12 | 3.17 | 3.42 |
| 22:45 | 1497 | Hearts vs St Mirren | 1.86 | 3.49 | 3.99 |
| 22:45 | 1572 | Annecy FC vs Paris FC | 2.90 | 3.10 | 2.50 |
| 22:45 | 1796 | Laval vs Rodez Aveyron | 2.06 | 3.37 | 3.37 |
| 22:45 | 2315 | Bordeaux vs Amiens | 1.88 | 3.37 | 3.96 |
| 22:45 | 2438 | Guingamp vs Grenoble Foot | 2.14 | 3.17 | 3.37 |
| 22:45 | 3084 | Metz vs US Quevilly Rouen | 2.04 | 3.27 | 3.52 |
| 22:45 | 3470 | KVC Westerlo vs OH Leuven | 2.01 | 3.59 | 3.34 |
| 22:45 | 4863 | Bastia vs PAU FC | 2.07 | 3.17 | 3.56 |
| 22:45 | 5705 | Le Havre vs Nimes | 1.62 | 3.65 | 5.60 |
| 22:45 | 5758 | Napoli vs Juventus | 1.92 | 3.37 | 3.82 |
| 23:00 | 2148 | Real Oviedo vs Alaves | 2.78 | 2.73 | 2.83 |
| 23:00 | 3608 | Celta Vigo vs Villarreal | 2.77 | 3.22 | 2.51 |
| 23:00 | 4241 | Aston Villa vs Leeds | 1.92 | 3.48 | 3.68 |
| 23:15 | 3491 | Portimonense vs Santa Clara | 2.07 | 3.19 | 3.59 |

CHEZA KWA WAJIBU. KIWANGO CHA MAKATO YA SIMU KUZINGATIWA.

Michezo
Ijumaa Januari 13, 2023
Nipashe

UKURASA 21



Guardiola apanga kuimaliza United



Kocha Mkuu wa Simba, Roberto Oliveira 'Robertinho' (kulia), akimweleza jambo mshambuliaji wa timu hiyo, Kibu Denis (kushoto), katika mazoezi yanayoendelea huko Dubai kwa ajili ya kujiandaa na mechi za Ligi Kuu Tanzania Bara, Kombe la FA na hatua ya makundi ya mashindano ya kimataifa ya Ligi ya Mabingwa Afrika. **PICHA: SIMBA SC**

## Yanga, Ihefu na usiku wa kisasi

**Na Saada Akida,** ZANZIBAR

KATIKA kuhakikisha inalipiza kisasi kwenye mchezo wao wa Ligi Kuu Tanzania Bara dhidi ya Ihefu SC utakaochezwa Jumatatu, viongozi wa Yanga wamesema wako katika hatua za kukamilisha usajili wa beki wa kati kutoka Mali, Mamhadou Doumbia, imeelezwa.

Doumbia ni nahodha wa Timu ya Taifa ya Mali ambaye anakiongoza kikosi hicho wakati wote wanaposhiriki mashindano ya Kombe la Mataifa ya Afrika kwa Wachezaji wa Ndani (CHAN).

Taarifa zilizopatikana jijini kutoka Yanga zinasema wanaamini beki huyo atakubali ofa yao na kutimiza mapendekezo ya Kocha, Nesreddine Nabi, ambaye alihitaji huduma ya nyota huyo.

"Taratibu zote za usajili zimekamilika na muda wowote watatambulishwa wachezaji wetu wapya akiwamo mshambuliaji, Kennedy Musonda na beki wa kati ambaye ni raia wa Mali, " kilisema chanzo chetu.

Ofisa Habari wa Yanga, Ali Kamwe, amekiri wanashusha beki wa kati mwenye kiwango kizuri ambaye anatumia mapigo ya kona na kufunga.

"Wanayanga wanatakiwa watulie wasiwe na presha juu ya usajili, tayari viongozi wameshakamilisha usajili, bado kutambulisha tu, msimu huu wapinzani wajiandae vizuri, " alisema Kamwe.

Ofisa Habari huyo alisema usajili uliofanywa ni kwa ajili ya kuimarisha kikosi chao kwa ajili ya kusimamisha nchi lakini kubwa ni kusaidia timu yao kufikia malengo wanayotarajia katika michuano ya kimataifa ya Kombe la Shirikisho Afrika.

Aliongeza kikosi cha timu yao kiliingia kambini jana kwa ajili ya kujiandaa kuwakabili Ihefu katika mchezo ambao utakuwa na lengo la kulipiza kisasi baada ya kufungwa walipokutana kwenye mzunguko wa kwanza huko Mbarali.

"Tunataka kupata idadi kubwa ya mabao ili kupunguza maumivu ya kuharibiwa Unbeaten yetu katika ligi, ni mechi muhimu na tunahitaji kuwapelekea mvua ya mabao, tunataka kushangilia tutakapowafunga kuanzia mabao matano, tukifunga bao la kwanza hatutashangilia," Kamwe alisema.

Aliongeza mechi hiyo wameibatiza itakuwa ni ya 'usiku wa kisasi' kwa sababu hawajasahau maumivu waliyoyapata kwenye mechi iliyo-

INAENDELEA UK. 23

# KAMBI YA SIMBA DUBAI IMENOGA

## Mo Dewji asisitiza haondoki Msimbazi, Talib aenda kuongeza mzuka wa...

**Na Adam Fungamwango**

WAKATI kikosi cha Simba kilichoweka kambi yake katika Falme za Kiarabu leo kitacheza mechi ya kirafiki dhidi ya wenyeji Al Dhafra ya Abu Dhabi, Kocha Mkuu wa timu hiyo, Roberto Oliveira 'Robertinho', amempa zawadi mshambuliaji, Kibu Denis, kutokana na kufanya vyema kwenye mazoezi.

Meneja Habari na Mawasiliano wa Simba, Ahmed Ally, aliliambia gazeti hili mechi hiyo itachezwa kuanzia saa 11:00 jioni kwa saa za huko sawa na saa 10:00 hapa nyumbani Tanzania.

Ahmed alisema Robertinho alihitaji kupata mechi mbili za kuwapima nguvu vijana wake na kufahamu kama mazoezi ambayo amewapa yamewasaidia.

"Alitaka mechi moja nyepesi na nyingine ngumu. Hawa Al Dafra ukiingalia haifanyi vyema kwenye ligi ya kwao, na hiyo ndiyo tutaanza nao na Jumapili tutacheza mechi kubwa dhidi ya CSKA Moscow ya Urusi, ni timu kubwa na mashabiki wengi wa soka nyumbani wanaifahamu, ipo hapa nayo pia kwa kambi ya muda mfupi," alisema Ahmed.

Aliongeza Robertinho amempa zawadi Kibu kutokana na kujituma mazoezini.

"Kwa siku ambazo yupo hapa amekuwa akifanya vyema na kujituma mazoezini. napenda mtu anayejituma sana, nimemnunulia zawadi," alisema kocha huyo.

Al Dhafra inashiriki Ligi ya Falme za Kiarabu yenye timu 14, kwa sasa inakamata mkia ikiwa na pointi nne tu baada ya kucheza mechi 12, ikishinda moja, sare moja na kupoteza michezo 10 wakati CSKA Moscow iliyoanzishwa mwaka 1911, ni timu maarufu sana katika michuano ya Ligi ya Mabingwa Ulaya na Kombe la UEFA ambapo imekuwa ikishiriki mara kwa mara.

Kwa sasa inashika nafasi ya tano kwenye msimamo wa Ligi Kuu Urusi, ikiwa na pointi 29 kwa michezo 17 iliyocheza mpaka sasa, ikishida mechi nane, sare tano na kupoteza nne.

Imetwaa ubingwa nchini Urusi mara 13, mara ya mwisho ikiwa ni 2017/18 na mafanikio yake makubwa Ulaya ni kutwaa Kombe la UEFA msimu wa 2004/05 na kufika fainali ya UEFA Super Cup 2005.

Wakati huo huo, Rais wa Heshima wa klabu hiyo, Mohammed Dewji 'Mo Dewji' amesema kamwe hataondoka ndani ya Simba kwa sababu ndio timu pekee anayoipenda hapa duniani.

Mo Dewji aliwaambia wachezaji wa timu hiyo wanatakiwa kuendelea kupambana kusaka ushindi katika kila mechi kwa ajili ya kuipa heshima na pale inapopoteza mchezo yeye huumia sana.

"Simba ikifungwa ninasikia maumivu yake ni makali mnoo na ikishinda furaha yake haina mfano, mimi nimekuja Simba kwa sababu ya mapenzi, hakuna chakunitoa Simba, mapenzi hayaishi," alisema Dewji.

Aliongeza kwa kuwataka wachezaji wafanye kazi yao kwa ubora mkubwa na kupuuza 'kelele' za watu kwamba yeye anaondoka, jambo ambalo haiwezekani.

"Niende wapi, nitafanya kila kitu kuhakikisha natimiza ndoto yangu ya kutwaa ubingwa wa Afrika siku moja," bilionea huyo alimaliza.

Katika hatua nyingine, kambi ya timu hiyo jana ilitembelewa na Talib Hilal, mchezaji na kocha wa zamani wa timu hiyo ambaye aliwataka wachezaji kurejesha ubingwa walioupoteza msimu uliopita lakini pia wapambane na kufika hatua ya nusu fainali ya mashindano ya kimataifa ya Ligi Mabingwa Afrika.

Talib, beki wa kati wa timu hiyo miaka ya 1980, na mmoja wa makocha aliyeiwezesha Simba kutinga hatua ya makundi, Ligi ya Mabingwa Afrika kwa kumtoa Zamalek mwaka 2003 kwa sasa anaichi Oman alisema lengo lake kuwatembelea wachezaji na

INAENDELEA UK. 23

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >